

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Hamsini na Mbili – Tarehe 25 Juni, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tano, Kikao hiki cha leo ni cha Hamsini na Mbili, Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, tunaanza na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali la kwanza litauliza na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi. Mheshimiwa Mukasa, tafadhalii kwa niaba yake nimekuona Mheshimiwa Shangazi.

Na. 447

**Mahitaji ya Ardhi na Upangaji wa Makazi – Mamlaka ya Mji  
Mdogo Biharamulo**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI (K.n.y. MHE. OSCAR R.  
MUKASA)** aliuliza:-

Kata ya Biharamulo Mjini imetangazwa kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo hivi karibuni; kwa sasa kuna mahitaji makubwa ya upangaji wa ardhi na makazi hasa katika hadhi ya kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo:-

Je, Serikali ipo tayari kuwaunga mkono wananchi wa Biharamulo Mjini wakati huu ambapo wao wenyewe wanaendelea na jitihada za ndani kuhakikisha wanakuwa na upangaji wa makazi unaoendana na hadhi mpya ya Mamlaka ya Mji Mdogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kuwaunga mkono wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo Biharamulo katika upangaji wa makazi ya mji huo. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imekamilisha michoro elfu tisa ya mipango miji yenye jumla ya viwanja 6,356 vyenye ukubwa wa ekari 8,753.7 kati ya viwanja hivyo, viwanja 2,337 vimepimwa na upimaji unaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha. Mpango wa baadaye ni kujenga barabara ya lami yenye urefu wa mita 700 ili kuboresha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, upangaji na upimaji wa makazi unawawezesha wananchi kupata faida mbalimbali ikiwemo kuongeza thamani ya ardhi, kupunguza migogoro ya ardhi, wananchi kupatiwa hati miliki ambazo zinawawezesha kuzitumia kupata mikopo katika taasisi za fedha na kuwawezesha wananchi kuishi kwenye makazi yaliyopangwa hivyo kurahisisha uwekaji wa huduma kama barabara, umeme na maji. Nazielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kuhamasisha wananchi na kuwashirikisha katika upangaji, upimaji na urasimishaji wa ardhi na makazi yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, nilikuona.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza,

Mheshimiwa Waziri, hivi karibuni alikuja Lushoto ambako kulikuwa na tatizo la upangaji wa ardhi katika Mji Mdogo wa Mnazi ambapo pesa ambazo zimetumika vibaya nje ya utaratibu na ulitoa maagizo. Sasa nataka kujua ni kwa kiasi gani jambo lile Ofisi ya Rais, TAMISEMI imelishughulikia?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Mji Mdogo wa Lushoto umeshatangazwa takribani miaka tisa, lakini mpaka sasa mamlaka ile bado haijaanza kazi, bado inapatikana ndani ya Halmashauri ya Lushoto. Sasa je, ni lini sasa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Lushoto itaanza kufanya kazi? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, asante. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shangazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nilifanya ziara katika Wilaya ya Lushoto, Mkoa wa Tanga na nikakuta kuna matumizi mabaya ya fedha shilingi zaidi ya milioni 300. Nikatoa maelekezo kwa Mkuu wa Wilaya, namshukuru uchunguzi umeshafanyika, tumeshapokea taarifa ile watu wote waliohusika namhakikisha Mheshimiwa Mbunge watashughulikiwa kwa mujibu wa tararibu za kisheria, tunalifanya kazi jambo hilo, naomba tupeane muda, tuvute subira kidogo.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Mheshimiwa Mbunge anaulizia habari ya Mji Mdogo ambao ultangazwa na haujawa mamlaka kamili. Nimejibu maswali haya mara kadhaa, nirudie tu kusema kwamba kama jambo hili haliongezi gharama za kuendesha Serikali, tumeelekeza na ni msimamo wa Serikali kwamba kwa sasa tujielekeze kuboresha maeneo na kukamilisha maeneo ambayo yalishaanzishwa kabla ya kuanzisha maeneo mengine ya mji.

Mheshimiwa Spika, sasa kama hili linaongeza gharama, kuongeza watumishi, majengo ya Serikali na bajeti kuongezeka, kwa kweli Serikali haitakuwa tayari kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo ndiyo majibu ya Serikali na Mheshimiwa Mbunge aendelee kutoa ushirikiano. Kadri tutakavyopata fedha ya kutosha, yale maeneo ambayo yameshaanzishwa yakaimarishwa vizuri kwa kupeleka huduma muhimu, vifaa, watendaji wa kutosha, basi maeneo mengine mapya yataanzishwa ili kupeleka huduma karibu na wananchi wetu. Ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea bado tupo Wizara hiyo hiyo na swali la Mheshimiwa Mbunge wa Chilonwa, Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga uliza swali lako.

Na. 448

**Barabara Inayounganisha Kijiji cha Mbelezungu na  
Kijiji cha Majeleko**

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitengeneza kwa kiwango cha kupitika muda wote wa mwaka barabara inayounganisha Kijiji cha Mbelezungu na Kijiji cha Majeleko vyote vikiwa ndani ya Kata ya Majeleko?

**SPIKA:** Majibu ya swali la Wanamajeleko, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA  
SERIKALI ZA MITAA (MHE. MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)  
alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbelezungu – Majeleko yenye urefu wa kilometra 10 imeingizwa kwenye mtandao wa barabara zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (*TARURA*) na hivyo kukidhi vigezo vyta kufanyiwa matengenezo kupitia fedha za Mfuko wa

Barabara. Aidha, tathmini ya barabara hiyo imefanyika na kubaini zinahitajika shilingi milioni 288.9.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuifanyia matengenezo barabara hiyo kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwaka.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kutohana na vyanzo vyetu vya fedha na kutohana na mipango kazi iliyopo, je, ni lini hasa Serikali inafikiri barabara hii itafanyiwa kazi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; barabara hii inahuisha uwekaji wa makalavati kadhaa. Je, Serikali haionti kwamba ni vema basi kutohana na vyanzo vya fedha vilivypopo, kazi zikagawanywa katika makundi kwamba labda itengenezwe barabara kwanza na makalavati baadaye au makalavati kwanza barabara baadaye, Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la wananchi wa Mbelezungu hadi Majeleko, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, majibu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi, nimeonesha mpaka kiasi cha fedha ambazo zinatakiwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa, naomba nirudie ni shilingi milioni 288.9. Tafsiri yake ni kwamba tayari tumeshabaini hata vivuko vinavyotakiwa kuwekwa na kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Spika, pia kwa wakazi wa Dodoma na Waheshimiwa Wabunge wa Dodoma, naomba niwaondoe hofu kama kuna sehemu ambayo Serikali imeamua kuwekeza

kuhakikisha kwamba miundombinu ipo ya uhakika ni pamoja na Dodoma. Hivi karibuni ukitafuta kwenye bajeti hutaiona lakini kuna jumla ya kama shilingi bilioni 84 tumeamua kuwekeza kuhakikisha kwamba *ring road* zinaanza kujengwa *immediately*.

**SPIKA:** Ahsante. Bado tuko TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwemba, Mbunge wa Kavuu, kwa niaba yake nimekuona Mheshimiwa Mtemi Chenge.

Na. 449

**Kodi ambazo ni Kero kwa Wananchi**

**MHE. ANDREW J. CHENGE (K.n.y. MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE)** aliluliza:-

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akitemea sana baadhi ya kodi ambazo zimekuwa ni kero kwa wananchi:-

Je, ni kwa nini baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikikaidi agizo hilo la Mheshimiwa Rais?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kodi kero zilifutwa na Serikali kuitia marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 mwaka 2017. Hivyo, Halmashauri yoyote inayoendelea

kuwatoza wananchi kodi ambazo zilifutwa na Serikali kwa mujibu wa sheria ni kukiuka maelekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuziagiza Halmashauri kuacha kutoza kodi ambazo zimefutwa kwa mujibu wa sheria. Ofisi ya Rais, TAMISEMI haitasita kuchukua hatua za kisheria kwa Halmashauri ambayo itabainika kuwatoza wananchi kodi ambazo zimefutwa kwa mujibu wa sheria. Aidha, endapo Mheshimiwa Mbunge anazo taarifa za Halmashauri inayotoza kodi zilizofutwa, tunaomba taarifa hizo ili Seriali iweze kuchukua hatua. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Andrew Chenge nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu ya Serikali, hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, Ofisi ya Rais, TAMISEMI haiwezi ikatoa waraka kwa halmashauri zetu zote nchini ikiainisha kodi zote za kero ambazo zilifutwa na Bunge hili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa vitambulisho vya wajasiriamali pamoja na nia njema iliyo nyuma yake, utekelezaji wake bado ni kero kubwa nchini. Je, Serikali pia haiwezi ikatoa maelekezo ya jinsi ya kutekeleza zoezi hilo ili tuwe na usare nchi nzima kuliko hali ilivyo sasa? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, la kuhusu vitambulisho mlishaahidi kwamba mtaleta huo waraka. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, anauliza kama Serikali inaweza ikatoa waraka ambao unaainisha kodi za kero ambazo zilifutwa na Bunge hili Tukufu.

Naomba tupokee ushauri huo na naomba niahidi kwamba waraka huu utatengenezwa na utasambazwa nchi nzima na Waheshimiwa Wabunge watapata nakala wa kuonesha kodi ambazo ni kero zilizofutwa na Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameuliza habari ya vitambulisho vya wajasiliamali. Ni kweli kama ambavyo wewe mwenyewe umeongezea, nilitoa tamko la Serikali katika Bunge hili Tukufu ulinipa fursa hiyo, lakini vilevile pamoja na waraka wetu ambao umetolewa nchi nzima na maelezo uliyotoa mara kadhaa katika Bunge hili, bado inaonesha kuna changamoto katika utekelezaji wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, tulisema tunapoanza *1<sup>st</sup> July*, mwaka wa fedha mpya wa 2019/2020, tutaoa waraka mahsusni na Waheshimiwa Wabunge watapata nakala ukianisha nani anapaswa kutozwa kodi ya wajasiri amali na nani anapaswa kupewa kitambulisho. Kwa kweli baada ya kutoa waraka huo, wale wote ambao watakiuka wakaienda kinyume na maelekezo haya ambayo kimsingi siyo matamanio ya Serikali na siyo matakwa ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais alimaanisha kuwasaidia wajasiri amali wadogowadogo wasipate usumbufu mtaani kwao wanapofanya biashara ndogondogo ya kujikimu kutozwa kodi kubwa na watu wa *TRA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania waendelee kuvuta subira, jambo hili tunalfanyia kazi na kwa kweli baada ya hapo itakuwa ni utekelezaji, hakutakuwa na msalia Mtume. Watu wote wafanye shughuli zao bila kuvunja sheria lakini wasipate bughudha ambazo kwa kweli ni kero. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Babati Mjini.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Ninavyofahamu mimi, *service levy* haichajiji kwa mfanyabiashara mmoja ambaye amefungua duka lake na

amelipa leseni na kodi ya mapato, lakini wafanyabiashara wadogowadogo kwenye baadhi ya Halmashauri wanachajiwa *service levy*, nini kauli ya Serikali juu ya hili?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii, Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Babati Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, ulipaji wa kodi ni kwa mujibu wa sheria na taratibu na sheria zipo na wasimamizi wanatakiwa kufuata taratibu hizo. Sasa Mheshimiwa Mbunge kama kuna maeneo ambayo watu wanachanganya analipa *service levy* ambayo imeelekezwa na bado anatzwa kodi nyingine, nafikiri tupate maelekezo yake na taarifa muhimu tuweze kulifanyia kazi.

Hata hivyo, kodi italipwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na sheria ipo, tunaomba hao wote wanaosimamia jambo hili watende haki na wasikilize watu na kutoa elimu ya umma. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest.

Na. 450

### **Likizo ya Uzazi kwa Wanaopata Watoto Mapacha au Njiti**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** Aliuliza:-

Je, ni likizo ya muda gani wamekuwa wakipewa wazazi (watumishi wanawake na wanaume) pale wanapopata watoto mapacha zaidi ya wawili au watoto njiti.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni H. 12(2) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, mtumishi wa umma mwanamke anapojifungua mtoto hupewa likizo ya uzazi ya muda wa siku 84 mara moja kila baada ya miaka mitatu. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni H. 12(3) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009, mtumishi husika anapojifungua watoto zaidi ya mmoja hupewa siku 14 zaidi za likizo ya uzazi na hivyo kuweza kuwa siku 98. Kanuni tajwa haikubanisha muda wa likizo ya uzazi kwa mtumishi anayejifungua mtoto njiti.

Mheshimiwa Spika, matukio ya uzazi wa mapacha zaidi ya wawili (*triple*) na watoto njiti ni nadra kutokea mara kwa mara. Hivyo, Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 hazikuainisha masharti ya likizo ya uzazi kwa matukio kama hayo. Hivyo, natoa wito kwa waajiiri na wasimamizi wa rasilimaliwtu katika utumishi wa umma kutoa taarifa kwa Katibu Mkuu wa Utumishi na kuomba kibali cha kuongezewa muda wa likizo ya uzazi kwa watumishi wa umma walio chini yao pindi wanapojifungua watoto mapacha zaidi ya wawili au watoto njiti.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni H.13 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009, Mtumishi wa Umma mwanaume hupewa likizo ya uzazi ya angalau siku tano kuanzia siku ya kuzaliwa mtoto ili aweze kuhudumia familia yake. Hata hivyo, iwapo kuna sababu za msingi zinazomlazimisha kuendelea kuhudumia familia kwa

ukaribu, mtumishi husika anaweza kuomba ridhaa kwa mwajiri wake ya kuongezewa ili siku kadhaa kuhudumia familia.

Mheshimiwa Spika, hivyo, inapotokea mtumishi wa umma kajifungua watoto mapacha zaidi ya wawili au watoto njiti na kulazimika kuwa na muda wa zaidi wa kuhudumia watoto hao, mwajiri wake anapaswa kuwasilisha hoja kwa Katibu Mkuu (Utumishi) ilia toe kibali cha kuongeza muda wa likizo ya uzazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali la kwanza, Serikali imekiri kwamba matukio ya kujifungua watoto njiti au mtoto zaidi ya mmoja hayakuwa makubwa hapo awali ila tunaongea kujifungua watoto njiti na mtoto zaidi ya mmoja ni matukio ambayo yamezidi kuongezeka.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutengeneza kanuni ya kuongeza siku kwa familia ambayo inapata hususan watoto njiti au watoto zaidi ya mmoja kwa sababu changamoto yake ni kubwa badala ya kuacha ilivyo leo inakuwa kama *amnesty* ya kupewa hiyo nafasi ya kulea hao watoto? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa wanaume ni kiungo muhimu katika familia na hasa familia inavyopitia changamoto ya kupata watoto njiti au watoto zaidi ya mmoja. Serikali haioni umuhimu pia wa kubadilisha kanuni ya kumruhusu mwanaume kukaa nyumbani kusaidiana na familia kwa si chini ya zaidi ya wiki mbili mpaka tatu ukizingatia kwamba hiyo likizo inatolewa mara moja kwa miaka mitatu ili akaisaidie familia pia? Nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa huyo mwanaume atakaa pale apakate mtoto au afanyeje? Wiki tatu nzima yaani mwanaume anakaa hapo. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu ya maswali hayo muhimu, wanaume wanahitaji likizo zaidi. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya mdogo wangu Mheshimiwa Anatropia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana kwa kuona umuhimu wa *maternity* na *paternity* kwa watumishi wa Umma. Hata hivyo, kama nilivyojibu kwenye swalilam singi ni kwamba katika kile kifungu cha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma cha 12(3) kama Serikali tumeongezea siku 14 zaidi kwa wale wamama wote wazazi ambao wanajifungua watoto ya wawili.

Mheshimiwa Spika, hii ni kuonesha umuhimu kwa mama mzazi kwa sababu sote humu ndani ni wanawake na wanaume, tumezaliwa tumelelewa na wanawake na tunajua kabisa huyu mama mzazi anapo jifungua anakuwa na *complications* nyingi lakini vilevile ndiyo anayenyonyesha watoto hata afya ya yule mama inahitaji kuimarika. Ndiyo maana kwa msingi huo tumeweza kuongeza siku 14 zaidi kwa mama mzazi huyu ambaye atajifungua watoto zaidi ya wawili.

Mheshimiwa Spika, katika swalilaki la pili kuhusu *paternity*; vilevile nimeshajibu kwenye jibu langu la msingi kwamba katika kifungu kile cha 13 cha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma baba mzazi na yeye anatambuliwa kuwa ni baba wa mtoto na ndiyo maana tumetoa kile kifungu kisheria kabisa kwamba angalau siku tano maana siku tano zile za mwanzoni mama akijifungua ndiyo kipindi hatarishi ambacho mama naye anamuhitaji baba awepo nyumbani.

Mheshimiwa Spika, vilevile huyu baba endapo mazingira kutokana na ile familia hayaruhusu, basi anaweza akaomba kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi kuititia kwa mwajiri wake. Ahsante.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Hawa Mchafu, swalilam singi ya nyongeza kwenye eneo hili.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kanuni za Utumishi wa Umma hazikuainisha waziwazi mtumishi mwanamke anayezaa watoto zaidi ya wawili ama mtoto njiti anaongezewaje siku; na kwa kuwa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini imetoa fursa ya kuingia mikataba ya hali bora mahali pa kazi, je, Serikali haioni umefika sasa wakati kwa kutumia hii fursa ya kutengeneza ama ya kuingia mikataba ya hali bora ya kazi kwa watumishi wanawake wanaopata watoto zaidi ya wawili ama kwa mwanamke anayezaa mtoto njiti? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja dogo la nyongeza la Mheshimiwa mdogo wangu Mheshimiwa Hawa Mchafu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Anatropia nimesema kwamba Serikali inatambua na inajali wanawake wote ambao wanajifungua watoto zaidi ya wawili na ndiyo maana kama Serikali tumeweza kuongezea zile siku 14 ili kwa pamoja ziweze kuwa siku 98 kwa sababu likizo ya uzazi ni siku 84. Kwa maana hiyo wale wote wanaojifungua watoto njiti au watoto zaidi ya wawili tumewaongezea siku 14. Hii iko kisheria ili kuthibitisha na kuhakikisha kwamba huyu mama mzazi anastahili kupewa haki yake.

Mheshimiwa Spika, hili jambo naomba niwaambie Wabunge wote kwamba liko kisheria na tumeongeza hizo siku 14 zaidi kwa ajili ya akina mama wote wanaojifungua mtoto zaidi ya mmoja. Ahsante.

**SPIKA:** Makamu Mwenyekiti wa *TWPG*.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka pia kujua, kwa kuwa nchi yetu tuna watumishi wa umma na watumishi katika sekta binafsi na siku zote tumekuwa tukihamasisha *PPP*, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kama kuna hilo tatizo waajiri wawasiliane na Katibu Mkuu Utumishi.

Je, wale wafanyakazi au watumishi wanawake wenye matatizo hayohayo lakini wanafanya kwenye sekta binafsi, wao watasaidiwaje kwa sababu nchi ni moja? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu tafadhalli.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma kwa majibu mazuri aliyoatoa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004, kifungu cha 33 kimeweka masharti ya kuhakikisha kwamba huduma bora kwa akina mama wote wajawazito, wanaojifungua na wanaume kwa maana ya waume wa akina mama hao kwenye *private sector* na wao wanapewa haki sawa na stahili katika kuhakikisha kwamba suala la uzazi linapewa kipaumbele pia kwa watumishi wa sekta binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa wito kwa waajiri wote nchini kuhakikisha wanatekeleza matakwa hayo ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2014 na hivyo kuwafanya wanawake wote wa Tanzania waweze kuthaminiwa katika suala hili muhimu sana la kukuza uhai katika dunia hii. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nami nitoe wito kwa wanaume wanaopata hii likizo ya uzazi wakae wapakate watoto, siyo wanaishia baa. (*Makofi/Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Kweli.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando.

Na. 451

### **Mpango wa Kujitathmini Katika Utawala Bora Afrika**

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI** aliuliza:-

Lengo kuu la Mpango wa Kujithathmini Kiutawala Bora Barani Afrika (*APRM*) ni kuziwezesha nchi za Afrika kuimarisha utawala bora kwa kuwawezesha wananchi wake kubainisha changamoto:-

Je, ni hatua gani ambazo zinachukuliwa na Tanzania katika kutekeleza mpango huo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, tafadhalii.

### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mionganini mwa nchi 38 kati ya nchi 54 Barani Afrika zinazoshiriki katika Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika (*APRM*) ambapo ilijunga mwaka 2004 na Bunge la Tanzania liliridhia

makubaliano hayo mwaka 2005. Hii ni kutokana na imani kubwa iliyonayo katika lengo kuu la Mpango wa *APRM* ambalo ni kuziwezesha nchi za Kiafrika kujitathmini kwa vigezo vinavyokubalika vya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya tathmini hizo ni kubaini changamoto zilizopo ili ziwekewe mikakati ya kugeuzwa kuwa fursa za maendeleo na pia kubaini maeneo ambayo nchi inafanya vizuri ili kuyaimarisha pamoja na kuigwa mataifa mengine. Tathmini hiyo hufanywa katika maeneo ya siasa na demokrasia, usimamizi wa uchumi, uendeshaji wa mashirika ya biashara na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilikabidhiwa jukumu la kuwezesha utekelezaji wa *APRM* hapa Tanzania. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara iliandaa semina na uhamasishaji juu ya Mpango wa *APRM* ili kuwaandaa wananchi kushiriki kikamilifu katika mpango huo na pia kuwawezesha kuchagua Wajumbe watakaowakilisha makundi yao katika Baraza la Usimamizi la Taifa. Hivyo, mwaka 2006 Wizara iliwezesha kuundwa kwa Baraza la Usimamizi la Taifa lenye Wajumbe 20 kutoka kwenye taasisi za Serikali na taasisi zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la Baraza ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za mpango na kuhakikisha kuwa zinafanya kwa uwazi, uadilifu na zisiingiliwe kisasia. Kwa kushirikiana na Wizara, Baraza liliajiri Sekretarieti inayofanya shughuli za *APRM* za kila siku na taasisi nne za kufanya utafiti katika kila eneo la tathmini.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka 2019, *APRM* imekwishaandaa taarifa mbili za utawala bora, taarifa ya ndani ya nchi na taarifa ya nje ya nchi. Pamoja na taarifa hizo, umeandalika mpango kazi wa *APRM* wenye lengo la kutatua changamoto za utawala bora zilizobainishwa kwenye taarifa zilizotajwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa taarifa za APRM kimeundwa kikosi kazi cha APRM chenyeh jukumu la kuandaa taarifa za utekelezaji wa kila mwaka na taarifa hizo huunganishwa kuwa taarifa moja ya nchi. Serikali imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili ya kazi za APRM kila mwaka na kulipa michango yake kwa taasisi hii kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Wizara na taasisi za Serikali pamoja na sekta binafsi inaendelea kutatua changamoto za utawala bora kama ilivyoelekezwa kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na kuainishwa kwenye mpango kazi wa APRM.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Gando, swali la nyongeza.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa mujibu wa maelezo ya Serikali ni kwamba APRM Tanzania inafanya shughuli zake chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kwa sababu hiyo basi, itawezaje kuismamia Serikali na kutoa majibu yaliyo sahihi kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, moja kati ya masharti ya APRM kwa wanachama wake ni kwamba mwanachama anatakiwa akubali kufanyiwa tathmini na wanachama wenza. Je, ni mara ngapi Serikali ya Tanzania imewahi kufanyiwa tathmini hii na wanachama wenzake?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote,

napenda kumpongeza Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando kwa maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ukisoma mkataba ambao umeanzisha APRM, inaongozwa na Baraza la Usimamizi la Taifa ambalo ni huru, linachaguliwa kutoka kwa watu mbalimbali, asasi za Kiserikali, vyama vya kisiasa na watumishi wa upande wa Serikali. Baraza hilo ni huru katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha mkataba huo na kwamba iko chini ya Wizara lakini muundo na utendaji wake unawahakikishia kwamba baraza hilo liko huru na wala haliwezi kuingiliwa na mtu yeoyote.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili la kuweza kuhakikiwa au kufanyiwa tathmini na wanachama wenza. Naomba tu nimkumbushe Mheshimiwa Othman Omar Haji kwamba APRM ilianzishwa na nchi za Kiafrika ili kuweka viwango vya kujitathmini ambavyo vinakubalika na Afrka na nchi za Kiafrika. Kwa hiyo, Tanzania imeruhusu nchi nyingi za Afrika, SADC na Afrika Mashariki kuweza kushiriki kwenye tathmini na kuweza kuzitathmini kwa mara nyingi zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendeleee na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swalii la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, umeruka swalii.

**SPIKA:** Basi tutarudi, tuendeleee Mheshimiwa Mgeni.

Na. 453

### **Kuokoa Watoto Wenye Mazingira Magumu**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kuna kundi kubwa la watoto wenye mazingira magumu ambao wanazurura tu na hivyo kukosa haki zao za msingi ikiwemo elimu na malezi bora:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuokoa kizazi hicho ambacho kinapotea?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutohana na sababu mbalimbali ikiwemo kufiwa na wazazi, migogoro ya familia na kutengana kwa wazazi, vitendo vya unyanyasaji na ukatili na umaskini katika ngazi ya kaya vimesababisha ongezeko la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utafiti wa Watoto Wanaoishi na Kufanya Kazi Mitaani uliyofanywa na Wizara mwezi Mei, 2018 uliohusisha Mikoa sita nchini ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Arusha na Iringa, jumla ya watoto wapatao 6,393 wakiwemo wa kiume 4,865 na wa kike 1,528 wanaoishi na kufanya kazi mitaani walitambuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2018 hadi mwezi Machi, 2019, jumla ya watoto 2,702 walipatiwa huduma mbalimbali katika Mikoa ya Arusha (330), Dar es Salaam (475), Dodoma (337), Iringa (313), Mwanza (770) na Mbeya (447). Huduma zilizotolewa ni pamoja na huduma za afya, chakula, malazi, kurudishwa shulen, stadi za ufundu, stadi za maisha, kuunganishwa na familia pamoja na msaada wa kisaikolojia na jamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa malezi na ulinzi wa watoto wakiwemo walio katika mazingira hatarishi, pia itaendelea kuwajengea uwezo wazazi na walezi

kwenye eneo la stadi za malezi na ulinzi wa mtoto. Aidha, Serikali itaendelea kufanya tafiti ili kubaini kiini cha tatizo na kupanga mipango mabsusi ya kupambana na kutokomeza tatizo la watoto wa mitaani nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kutoa rai kwa jamii kuhakikisha jukumu la matunzo, malezi na ulinzi wa mtoto linatekelezwa ipasavyo. Vilevile nizitake Mamlaka za Serikali za Mitaa ziandae mipango na mikakati madhubuti ikiwemo kutenga rasilimali za kutosha katika kukabiliana na tatizo hili la watoto wanaishi na kufanya kazi mitaani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgeni, nimekuona.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri lakini bado kundi hili ni kubwa mno. Ukienda masokoni watoto wanabeba mizigo, bandarini watoto wanapara samaki na wengine wanatumiwa kuuza madawa ya kulevyia, kwa hiyo, bado Serikali inatakiwa kufanya kazi na ina mkakati gani wa makusudi kuliondosha kabisa tatizo hili ili watoto wetu warudi katika malezi mazuri na wapate elimu? Hilo ni swali la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, vilevile kuna wanawake ambao wanajihuisha na udhalilishaji wa watoto, wanawatoa vijijiini na kuwapeleka mjini na kuwafanyisha biashara ya ukahaba na ni kundi kubwa tu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuunda Kamati Maalum kuwafuatilia wanawake hawa na wanatakapopatikana wapewe adhabu ya kutosha ili iwe ni fundisho kwa wengine ili suala hili la kudhalilisha watoto liondoke kabisa? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, tafadhalli.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, ambaye naye amekuwa anafuatilia sana masuala

ya ustawi na maendeleo ya watoto, nimpongeze sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, nianze kujibu maswali yake mawili. Tuna Sera ya Maendeleo ya Mtoto lakini tuna Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 ambazo zimeainisha haki za msingi za motto. Mtoto ana haki ya kutunzwa, kuendelezwa na kutofanyishwa kazi nzito. Kwa hiyo, hizi sheria zipo na ziko wazi na pale mzazi au mlezi anapokiuka basi hatua za kisheria zinachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe tu jamii na sisi kama Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuyasemea haya. Sisis kama Wizara tutaendelea kuchukua hatua pale tunapobaini na mashauri yale yanapofika katika ngazi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili ameongelea suala la watoto kufanyishwa kazi za kingono na baadhi ya walezi. Niseme tu katika Mpango Mkakati wa Serikali wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/2018 ambao utaisha mwaka 2021/2022, tumeelekeza kuanzishwa kwa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto. Kamati hizi zimeanzishwa katika ngazi ya taifa mpaka katika ngazi ya kijiji na tunaendelea kuziimarisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pale tunapopata taarifa kwamba kuna matukio kama haya zile Kamati zina wajibu wa kuyafuatilia matukio hayo na sisi kama Serikali tunafuatilia na kuchukua hatua stahiki.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Goodluck Mlinga, swalil la nyongeza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Uwepo wa kundi kubwa la watoto wazururaji kunasababishwa na wazazi kutofuata njia bora ya uzazi wa mpango. Njia bora kabisa ya uzazi wa mpango isiyo na madhara yoyote ni matumizi ya mipira ya kike na ya kiume.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa katika jamii yetu kumekuwa na tatizo kubwa la watu kutotumia mipira ya kike na ya kiume licha ya watengenezaji kuweka vionjo mbalimbali katika dhana hii kwa mfano *strawberry*, ndizi, *chocolate* na hivyo kusababisha siyo tu kuwa na watoto wa mitaani bali ongezeko kubwa la magonjwa ya zinaa na *HIV*. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu inayoendana na wakati ya watu kutumia mipira hii ya kiume ili kuondokana na changamoto hii ya watoto wa mitaani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna *correlation* kati ya watoto wa mitaani na mipira ya kiume na kike? Majibu tafadhalii. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, moja ya kisababishi ambacho kinapelekea kuwepo na watoto wa mitaani, ni wazazi kutojijandaa kupata watoto na labda na lingine ni moja ni kwamba watu kupata ujauzito wakiwa na umri mdogo pasipokuwa na uwezo wa kulea.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tumekuwa tunahimiza sana suala la uzazi wa mpango na katika suala hili la uzazi wa mpango kuna njia mbili, kuna matumizi ya dawa, lakini hata hii mipira ya kiume kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema.

Mheshimiwa Spika, kKwa hiyo rai yangu kwa jamii ni kwamba kabla hatujaanza kuingia katika suala la kupata watoto ni muhimu ni vizuri tukajitafakari katika masuala mazima ya malezi na matunzo ya watoto. Suala siyo kuzaa tu ila ni kuhakikisha kwamba watoto wale tunaweza tukawalea na kuwapa matunzo ambayo yanastahiki na njia zote hizi tunazo ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa kondomu tunazo za kutosha ndani ya nchi

**SPIKA:** Tunaendelea bado tuko Wizara ya Afya, swalii la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 454

### **Bima ya Afya kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Watu wenye ulemavu wamekuwa wakipata adha kubwa katika kupata matibabu ikiwemo kukosa fedha kwa ajili ya matibabu:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha inawapatia bima ya afya watu wenye ulemavu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya mapitio ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 na kuandaa mapendekezo ya Sera mpya ya Afya. Katika mapitio ya Sera ya Afya ya Mwaka 2007, changamoto mbalimbali za matibabu kwa makundi ya msamaha ziliibiliwa na watoa huduma pamoja na watumiaji wa huduma hizo. Moja ya changamoto iliyojitokeza ni hospitali zetu kuwa na wagonjwa wengi wa misamaha na hivyo kushindwa kuboresha huduma za afya. Kutokana na changamoto hiyo ya kuwa na makundi mengi ya msamaha, Wizara iliona ni vyema ikaboresha utaratibu wa misamaha kwa kuhakikisha kuwa wananchi wasio na uwezo tu ndio wanaopatiwa msamaha.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya Sera mpya ya Afya kila mwananchi mwenye uwezo atapaswa

kugharamia huduma za afya. Sera pendekezwa inaainisha njia mahsusizi zitakazowezesha Serikali kubaini wananchi wote wenye uwezo ili waweze kuchangia gharama kabla ya kupokea huduma, kwani ni wazi kuwa si kila mlemavu ana kipato duni. Hivyo, wananchi watakaothibitika katika maeneo yao kuwa hawana uwezo wa kuchangia ikiwemo walemavu, wataendelea kupatiwa matibabu bila kuchangia gharama za matibabu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inatambua changamoto za uchangiaji wa huduma za afya na inaandaa utaratibu wa bima ya afya kwa Watanzania wote ikiwa ni pamoja na kundi la walemavu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu ya Waziri naomba kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, afya ni jambo la msingi sana, Serikali ilikuwa imeshauri kwamba kila halmashauri iweze kutenga asilimia nne, wanawake; nne, vijana; na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu ili waweze angalau kujimudu kiuchumi, lakini halmashauri nyingi zimeshindwa kutenga fedha hizo kwa sababu vyanzo vingi vya mapato vimekwenda Serikali Kuu ikiwemo halmashauri yangu ninayotoka mimi ya Iringa DC. Swali la kwanza, je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hawa watu wenye ulemavu wanapata matibabu bila vikwazo ikiwemo wale wenye bima unakuta hata wakiwa katika bima vifaa tiba kama *sun screen lotion* inakuwa ni shida, haipatikani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni lini sasa Serikali italeta huo Muswada wa Bima ya Afya kwa Watu Wote (*Universal Health Coverage*) ili tuupitishe na watu hawa wenye ulemavu waweze kupata huduma hii ya afya bila matatizo? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ndugulile, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali tuliweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunatenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya vijana, wanawake na asilimia mbili kwa ajili ya walemovu na hili ni takwa kwa kila halmashauri ambalo wanapaswa wazingatie na kuhakikisha kwamba hii mikopo inafika na inapatikana pasipo kuwa na riba.

Mheshimiwa Spika, nikiongelea suala la matibabu, hakuna mwananchi ambaye anahitaji matibabu atayakosa kwa sababu ya hali yake ya maumbile. Kwa hiyo hilo nataka niliweke wazi na sisi kama Serikali tutaendelea kutoa matibabu kwa walemovu ambao wanastahilli kwa mujibu wa taratibu ambazo tunazo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameongelea ni lini Serikali italeta Muswada wa mabadiliko ya sheria ama sheria inayohusiana na bima ya afya kwa wananchi wote, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge mpango wetu sisi Serikali ni kuleta katika Bunge la Septemba.

**SPIKA:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Amina Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, watu wenye ulemavu hasa wanaishi vijijini hata hizo fursa ni vigumu sana kuzipata. Naomba kujua mkakati wa Serikali hasa kwa walengwa wenye ulemavu kule vijijini ambako hawajui hata wapi pa kwenda ili basi hizi huduma zinazotolewa na wao waweze kupata? Mkakati rasmi ndiyo ninaoutaka.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Mollel. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, kwa majibu ya kimsingi kabisa ambayo yanaonesha ni kwa namna gani Serikali imejikita kuwashudumia watu wenye ulemavu na kuhakikisha afya zao zinakuwa bora, tunaishukuru sana Serikali lakini hasa Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la pili la uwezeshaji wananchi kiuchumi Ofisi ya Waziri Mkuu imepewa dhamana ya kuhakikisha kwamba masuala yote ya uwezeshaji wananchi kiuchumi yanakuwa *inclusive*, yanawagusa pia wenye ulemavu wote nchini. La kwanza ni hilo ya Mifuko hiyo ya Vijana, Wanawake na Wenye Ulemavu, lakini tunazo program za mkakati wa kukuza ujuzi katika nchi ya Tanzania. Program hizo ziko tano na zimeanza kutekelezwa.

Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Amina Mollel chini ya ushauri wa Naibu Waziri anayehudumu kwenye eneo la wenye ulemavu, dada yangu lkupa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ujumla program zote ambazo zitakwenda kutekelezwa mpaka vijijini za kuwawezesha wananchi kiuchumi, tunasimamia kuhakikisha na wenye ulemavu wanakuwa ni *party* program hizo. Jambo hili limeweza kuanza kuonekana kwa mfano, sasa hivi tuna program maalum ya *green house* tumeamua na wenye ulemavu wanakuwa ni sehemu ya matunda hayo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika Taifa letu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunarudi sasa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Issa Mangungu.

Na. 452

**Ujenzi wa Barabara ya Kilwa Eneo la Rangi Tatu – Kongowe  
– Mikwambe, Dar es Salaam**

**MHE. MARY P. CHATANDA (K.n.y. MHE. ISSA A. MANGUNGU)** aliuliza:

Barabara ya Kilwa eneo la Rangi Tatu – Kongowe – Mikwambe inaharibika na ni finyu sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga barabara hiyo kwa njia nne?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimia Elias Kwandikwa, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ipo katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara ikiwemo Barabara Kuu ya Kilwa kuanzia eneo la Rangi Tatu – Kongowe – (kilomita 3.8) na barabara ya Mkoa kuanzia Kongowe – Mikwambe – Kibada – Mji Mwema hadi Kivukoni (kilomita 17.55). Lengo ni kupunguza tatizo sugu la msongamano wa magari na ajali barabarani.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilwa kuanzia Mbagala Rangi Tatu hadi Kongowe yenyе urefu wa kilometra 3.8 inatarajiwа kупанулиwa toka njia mbili na kuwa njia nne kazi ambayo inahusisha pia upanuzi wa daraja la Mzinga. Kazi ya usanifu wa kina inaendelea na inatarajiwа kуkamilika mwishoni mwa mwezi Julai, 2019.

Mheshimiwa Spika, kazi ya upanuzi na matengenezo maalum kwa sehemu korofi ya barabara ya Kongowe – Mikwambe – Kibada – Mji Mwema hadi Kivukoni ilitekelezwa awamu kwa awamu kadri fedha zilivyopatikana. Kazi ya upanuzi awamu ya mwisho kwa barabara hii imekamilika mwezi Desemba, 2018 ilifanyika katи ya Mikadi na Kivukoni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mary Chatanda, nimekuona swali la nyongeza.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROAD* wamekuwa wakifanya kazi ya kuweka alama za *X* kwenye maeneo ambayo wanakusudia kufanya upanuzi wa barabara, lakini kazi hiyo ambayo wamekuwa wakiifanya hawawahusishi wananchi wa maeneo husika kwa kuwaarifu kwamba wanakusudia kufanya hivyo, watu wanawaona tu wanaweka alama za *X*. Je, kwa nini wanafanya kazi hiyo bila kuwahusisha wananchi ili waweze kuwafahamu na kuondoa tataruki ambazo zinajitokeza katika kuwekewa alama za *X*? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chatanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza pongezi alizozitoa nazipokea kwa moyo mnyoofu, lakini pili niseme kwamba zoezi la kuweka alama za *X* kwamba inawezekana labda kuna baadhi ya maeneo wananchi hawakujulishwa labda hili litakuwa ni tatizo, lakini kimsingi tunavyoweka alama za *X* barabarani inaenda sambamba na kutoa elimu na kuwafahamisha wananchi juu ya alama hizo kwa sababu yako maeneo ambayo ni uvamizi, wananchi wamevamia lakini yako maeneo ambayo labda saa nyingine mradi unawafata wananchi na wanastahili kulipwa fidia, kwa hiyo suala la elimu linatakiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii tu nielekeze maeneo yote nchini pale ambapo tuna miradi ya barabara na miradi yoyote inayosimamiwa na Wizara na

taasisi zingine kwa maana ya *TANROADS, TARURA* na maeneo mengine kwamba kwamba wananchi lazima wahuishwe kikamilifu na viongozi walioko maeneo hayo. Sambamba na hilo elimu itolewe ili wananchi wafahamu nini wanatakiwa kufanya na pia wafahamu haki zao. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Niwakumbushe Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo usafiri wa kutoka mjini Dar es Salaam kuelekea Mbagala ni kizungumkuti kweli kweli. Tunaomba hebu wasaidieni wale wananchi, ni msongamano mkubwa sana sana yaani ni adha kubwa sana, pia Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hebu liangalieni kipekee hili jambo la usafiri wa kwenda Mbagala, kwa akinamama, watoto na wazee ni hatari kabisa.

Nilikuona Mheshimiwa mama Salma Kikwete, swalii la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niulize swalii la nyongeza kutokana na swalii la msingi. Kwanza tunaishukuru Serikali kwa kutupatia fedha kwa kukarabati barabara tajwa ya Kilwa eneo la Rangi Tatu – Kongowe - Mikwabe na kadhalika. Barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya mkoa wa Dar es Salaam na maeneo yake ya jirani, barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Mtwara na kuelekea maeneo mengine. Sasa kwa kuwa barabara hii inajengwa nyakati za mchana na sasa hivi mkandarasi yuko kazini na imekuwa ni kero kubwa juzi wakati tukiwa Misri dunia sasa hivi ni kiganja tukiwa Misri tumepata taarifa na tumeona jinsi watu wa maeneo ya Dar es Salaam wale wanaokwenda Lindi na Mtwara wamekaa zaidi ya masaa manne wakisubiri kwa kuwa mkandarasi yuko barabarani. Sasa kwa nini kusiwe na utaratibu badala ya kujenga barabara hii mchana ijengwe jioni au usiku ili watu mchana waendelee na kazi zao kwa ajili ya kujipatia maendeleo hayo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo muhimu, ndiyo msisitizo ambao hata mimi niliuweka sasa hivi kuelekea Mbagala ni mtihani kweli kweli. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, mama yangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru pia kwa maelekezo yako kwa sababu na wewe nafikiri jambo hili umeliona, niseme tu kwamba, kwanza nilipokee kama ushauri kwamba tutafanyia kazi ili wananchi wasipate adha wakati wa matengenezo yanavyoendelea. Hata hivyo, niseme tu kwamba, matengenezo yanayoendelea nia yake kubwa ni kuhakikisha kwamba tunapunguza ule muda wananchi wanakaa barabarani tutapunguza msongamano, lakini pia tunapunguza ajali. Niseme tu kwamba tutalismamia jambo hili kwa sababu suala la kujenga usiku na mchana tutaliangalia, lengo kwanza mradi huu ukamilike haraka ili wananchi waweze kupata hii huduma muhimu.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na mjadala mrefu kidogo na Mheshimiwa Mbunge wa Mkuranga na tulikuwa tumezungumza juu ya suala hili, kuna baadhi ya mambo ambayo tayari tumeyatolea maelekezo. Hii ni pamoja na kuangalia kwamba tunapokuwa na matengenezo hasa hasa katika Jiji la Dar es Salaam tuone pia *alternative route* zingine ambazo zinaweza zikapunguza watumiaji wa barabara ili msongamano usiwe shida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutaliangalia kwa umakini na nitalifuatilia ili sasa tuone kwamba kwanza mradi unafanyaika kwa haraka, zoezi linakamilika kwa haraka, lakini ile adha wanayoipata wananchi iweze kuondoka. Kwa hiyo, nashukuru tutalichukua hili kwa umakini mkubwa na tutalismamia kama Serikali ili shida hii iweze kuondoka kabisa.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu hayo mazuri.

Tunahamia Wizara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Anthony Calist Komu, Mbunge wa Moshi Vijijini, hayupo, Mheshimiwa Selasini kwa niaba yake.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa bado una mpira wa Misri kichwani. Naomba sasa swali la Mheshimiwa Komu namba 455, sasa lipatiwe majibu.

Na. 455

**Shamba la Miwa la TPC**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. ANTONY C. KOMU)** aliuliza:-

Shamba la miwa la *TPC* lina eneo lenye ukubwa wa zaidi ya hekta 6,000 ambalo halifai kwa kilimo cha miwa lakini zipo taarifa kiuwa wawekezaji wanataka kulitumia eneo hilo kuanzisha hifadhi ya wanyamapori:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali inaruhusu mwekezaji huyo kuanzisha mradi tofauti kabisa?

(b) Je, ni kwa nini Serikali isitoe eneo hilo kwa wananchi wanaozunguka shamba hilo kwa ajili ya malisho ya mifugo yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Omari Tebweta Mgumba, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anthony Calist Komu, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijiji, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *TPC* ina takribani hekta 13,000 ambapo hekta 8,500 zimeendelezwa kwa kilimo cha miwa na eneo hekta 4,500 ambazo zipo kusini mwa Kiwanda cha *TPC* katika Vijiji vya Mawala na Mikocheni halina udongo wa kuwezesha kilimo cha miwa ya sukari kutokana na hali ya udongo kuwa na magadi. Tangu mwaka 1936 ambapo shamba hilo lilikuwa linamiliikiwa na Serikali kabla

ya ubinafsishwaji, eneo hilo la hekta 4,500 halikuwahi kulimwa zao lolote. Aidha, eneo hilo lilikuwa ni korido ya wanyamapori waliokuwa wakihama kutoka Tarangire kuititia Msitu wa Tembo kwenda hadi Ziwa Jipe. Ilipofika mwaka 2014 Serikali illipatia Kampuni ya *TPC* leseni Na.1 ya kuanzisha shamba la wanyamapori (*Certificate of Game Ranching*) baada ya kukubali maoni ya *TPC*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maendeleo ya kazi za binadamu katika vijiji vilivyoopo Kata ya Msitu wa Tembo wilaya ya Simanjiro, Vijihi vya Kahe, Mawala, Chemchem na Mikocheni Wilaya ya Moshi Vijihi vimesababisha korido hizo kuvunjika na wanyama kuendelea kuwepo katika maeneo hayo. Kwa hali hiyo, ili kuzuia uharibifu wa misitu na uwindaji holela wa wanyamapori, kiwanda cha *TPC* kilipewa leseni ya eneo hilo kwa ajili ya kuendeleza hifadhi ya mazingira ikiwemo misitu pamoja na wanyamapori wallomo katika eneo hilo. Aidha, ikumbukwe kwamba uamuzi huo wa Serikali ulizingatia umuhimu wa hifadhi ya maliasili iliyoko katika eneo hilo, pamoja na ukweli kuwa udongo katika eneo hilo usingeweza kutumika kwa kilimo hata kama sehemu hiyo ingekabidhiwa kwa wenyeji wa vijihi vinavyozunguka eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini swalii la nyongeza, tafadhali.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kutokana na utaalam ambao Serikali iliufanya eneo lile halifai kulima miwa lakini haina maana kwamba halifai kwa kilimo cha mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, Wilaya ya Moshi Vijihi ni kati ya maeneo yenyeye uhaba mkubwa sana wa ardhi, je, ni kwa nini Serikali isitoe eneo hili kwa wananchi ili walitumie kwa ajili ya kilimo cha mazao mengine badala ya kuendelea kukaa mikononi mwa *TPC* kwa sababu *TPC* wanaonyesha kwamba hawakuwa na programu wala utayari wa kulitumia hili eneo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wakati eneo hili likitolewa na nakumbuka ilikuwa wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu kuliwa na programu ya kulingawa eneo hili kwa wananchi ili litumike kwa ajili ya makazi. Ni kwa nini Serikali isirejee uamuzi au mipango yake ile ya awali ya kuligawa hili eneo kwa wananchi ili walitumie kwa makazi badala ya *TPC* kulihodhi tu bila kuwa na jambo lolote ambalo wanalifanya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini, hata Serikali ikikubali wazo hilo, hivi kule Moshi unamgaia nani unamwacha nani? (*Makofi*)

Majibu Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Mguma, je, Serikali inaweza ikagawa eneo hilo kwa wananchi Kilimanjaro kule?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selasini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anasema kwamba lile eneo kwa mujibu wa utafiti na tathmini ya udongo limeonekana halifai kwa kilimo cha miwa lakini linafaa kwa mazoa mengine. Sasa anataka kujua kwa nini Serikali tusiwape wananchi eneo lile ili waweze kulima mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, kwanza eneo lile kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi ni eneo ambalo Serikali tulishalibinafsisha kwa kampuni binafsi, ni eneo la taasisi au kampuni nyingine. Kwa hiyo, kwa mujibu wa sheria na kanuni mbalimbali huwezi kuchukua mali ya mtu mwengine ukaigawa kwa watu wengine. Kwa hiyo, kwa sasa hivi *TPC* baada ya kuona kwamba hawawezi kulitumia eneo hilo kwa kilimo cha miwa na ni mali yake ameamua kuliendeleza kwa ajili ya hifadhi ya misitu na mbuga ya wanyama na watavutia watalii na kuigiza mapato Serikalini ya kigeni na mapato mengine.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anasema Serikali zamani ilikuwa na malengo kulirudisha lile eneo kwa

wananchi ili liwe eneo la makazi kwa ajili ya wananchi wa Moshi. Kama nilivyojibu kwenye swalii msingi lile eneo ni mali ya mtu na tulimpa kwa mujibu wa sheria haiwezekani kumpokonya na kumpa mtu mwingine.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Maji, swalii la Mheshimiwa David Ernest Silinde, kwa niaba yake Mhehimiwa Mwakajoka.

Na. 456

### **Mpango wa Kutatua Kero ya Maji – Momba**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA (K.n.y MHE. DAVID E. SILINDE)** aliuliza:-

Je, ni upi mpango wa sasa wa kutatua kero ya maji katika Jimbo la Momba?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo, Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Aweso, tafadhalii.

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Mheshimiwa Maziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa sasa wa Serikali wa kutatua kero ya maji katika Jimbo la Momba ni kuitia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*) ambayo inatekelezwa pia katika Halmashauri zote nchini. Programu hiyo imelenga kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na endelevu ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, kuitia programu hiyo, tayari katika Wilaya ya Momba Serikali imekamilsha miradi ya maji mitano katika vijiji vya Namtambala, Itumbula, Iyendwe, Mnyuzi na Chilulumo ambapo jumla ya wananchi 20,271 wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Momba imetengewa kiasi cha Sh.1,744,000,000 kwa ajili ya uchimbaji wa visima, usanifu na ujenzi wa miundombinu ya maji. Utekelezaji wa miradi hiyo uko katika hatua mbalimbali ambapo mradi wa maji katika Kijiji cha Tindingoma, mkandarasi amesaini mkataba kwa ajili ya ujenzi; Mradi wa maji katika Kijiji cha Kitete upo kwenye hatua za manunuzi; na kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi katika Kijiji cha Ikana upo kwenye hatua ya usanifu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo zilizochukuliwa, Serikali pia ipo katika hatua ya manunuzi ya kumpata makandarasi wa kupima na kuchimba visima katika vijiji saba (7) vya Mpapa, Samang'ombe, Kasinde, Namsinde, Chole, Nkangamo na Itelefya. Vilevile, mkandarasi huyo atafanya usanifu wa mradi wa maji utakaotumia chanzo cha Mto Momba kwa kuhudumia vijiji 21 vya Ivuna, Lwate, Mkomba, Ntungwa, Kalungu, Sante, Tontela, Kaonga, Nsanzya, Chuo, Namsinde I, Kasanu, Masanyinta, Senga, Mweneemba, Makamba, Naming'ongo, Yala, Muuyu, Usoche na Makao Makuu ya Wilaya ya Momba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, nimekuona swali la nyongeza.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba vijiji vitano mpaka sasa hivi vimeshakamilika kupata maji katika Jimbo la Momba ambapo jumla ya vijiji vilivycopata maji sasa hivi vitakuwa ni saba (7) lakini jimbo hili lina vijiji 82 ina maana kati ya vijiji 82 ni vijiji saba (7) tu ndio vyenye maji ya bomba. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba katika bajeti hii ambayo imetengwa ya shilingi bilioni 1.7 inapelekwa kama ambavyo imetengwa ili kwenda kupunguza tatizo la maji kwenye Jimbo la Momba?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mwaka 1973 katika Mji wa Tunduma uliazishwa mradi wa maji wa mserereko katika Kata za Mpemba na Katete. Mradi ule sasa hivi umekuwa ukitoa maji kidogo sana kutokana na kutokukarabatiwa kwa muda mrefu. Serikali ina mpango gani kukarabati mradi ule ili uwahudumie wananchi wa kata hizo mbili?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri. Kikubwa ambacho nataka kusema ni kwamba llani ya Chama cha Mapinduzi inatutaka itakapofika 2020 tuwe na 85% ya upatikanaji wa maji vijiji na 95% upatikanaji wa maji mijini.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, sisi kama Wizara ya Maji tukaona chanzo pekee ambacho kinaweza kutatua tatizo la maji katika Mji wa Mombasa ni kutumia Mto Mombasa. Sasa hivi tupo kwenye hatua ya usanifu, mradi ule utakapoanza utaweza kuhudumia zaidi ya vijiji 21. Kwa hiyo, tunamhakikisha Mheshimiwa Mbunge tutafanya usanifu ule kwa haraka kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuchukua maji Mto Mombasa na kuweza kuhudumia vijiji 21.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ukarabati wa mradi wa maji kwa ajili ya kuhudumia Kata ya Mpemba, sisi kama Wizara ya Maji tutaongea na Wahandisi wetu Maji pale Tunduma kuhakikisha wanafanya ukarabati huo ili wananchi wawze kupata huduma hii maji. Maji ni uhai, sisi kama viongozi wa Wizara hatupo tayari kupoteza uhai wa wana Tunduma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na Mheshimiwa Aisharose Matembe.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kama lilivyo tatizo la maji katika Jimbo la

Momba kwenye Jiji la Mbeya sasa hivi tatizo la maji tunaweza tukasema ni janga. Bonde lote la Uyole maji ni tatizo, ni kukavu kabisa, wananchi wanyonge wanunua maji mpaka ndoo Sh.500, maisha haya yalivyokuwa magumu. Maeneo ya Mwakibete na Ilomba, kote maji ni tatizo. Tumeshauri ili kutatua tatizo la maji Mbeya tutoe maji Mto Kiwira iwe kama *source*.

Mheshimiwa Spika, cha ajabu akija Rais au Waziri Mkuu maji Mbeya yanatoka, hayakatiki, wakiondoka maji yanakatika. Tatizo nini hasa ambalo linafanya changamoto hii ya maji katika jiji la Mbeya lisitatulike wakati vyanzo vya maji tunavyo na miundombinu ipo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu kaka yangu Mheshimiwa Mbilinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo nataka kusema ni kwamba Jiji la Mbeya sasa hivi limekuwa na ongezeko kubwa sana la watu. Kwa hiyo, mahitaji na uzalishaji wetu umezidiwa kutoka na ongezeko kubwa la watu.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Naibu Waziri wa Maji nilifika Mbeya na nimejionea hali halisi na kweli nimefika katika chanzo cha Mto Kiwira tumeona hiki ni chanzo pekee ambacho kinaweza kikatumika na kutatua tatizo la maji la Mbeya. Tumekubaliana sisi kama Wizara kuangalia namna ya kufanya usanifu ili sasa tuweze kutumia chanzo cha Mto Kiwira katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji katika Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Spika, lakini haki ya mwananchi ni kupatiwa huduma ya maji. Niwaagize Wakurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mbeya kuhakikisha inatoa huduma hii maji, kwa uchache wake, lakini kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma muhimu na

bora si mpaka kiongozi aweze kufika. Cha msingi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara tumejipanga kuhakikisha tunatatua tatizo hili la maji katika Jiji la Mbeya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aisharose Matembe.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Changamoto ya ukosefu wa maji iliyopo Momba inafanana kabisa na changamoto ya ukosefu wa maji iliyopo Manyoni Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mradi wa Kintinku - Lusilile utekelezaji wake umekuwa ukisucasua, je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupeleka fedha za kutosha ili kukamilisha mradi huo hasa ikizingatiwa kwamba kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha zaidi ya wakazi wa vijiji kumi? Nashukuru.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Maji Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda nijibu swali la dada yangu Mheshimiwa Aisharose, kwanza, ni mionganini mwa Wabunge akina mama wafuatiliaji suala zima la maji katika Mkoa wa Singida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kikubwa nachotaka kusema utekelezaji miradi ya maji unategemea na fedha. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara ya Maji tutawaangalia kwa namna ya kipekee katika kuhakikisha wakandarasi wanao-*rise certificate* ya utekelezaji wa mradi wa pale Manyoni Mashariki tunawalipa kwa wakati na utekelezaji wake uendelee na wananchi waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge pamoja na Manyoni kuwa na changamoto ya maji lakini sisi kama serikali na tunamshukuru

Mheshimiwa Rais zaidi ya dola milioni 500 tulizopipata kwa ajili ya kutatua tatizo la maji nchi zaidi ya miji 28 Tanzania Bara na mji mmoja Zanzibar, sasa hivi Mkoa wa Singida miji mitatu tunaenda kutatua tatizo la maji. Wahandisi Washauri wameshapatikana, nataka nimhakikishie itakapofika mwezi September wakandarasi watakuwa *site* katika kuhakikisha tunakwenda kutatua tatizo la maji na sisi kama Wizara ya Maji tumejipanga vizuri sana.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa wa Chumbuni, Mheshimiwa Pondeza.

Na. 457

**Kufungwa kwa Vituo Vidogo vya Polisi Mjini  
Magharibi Unguja**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI** aliuliza:-

Vituo vingi vidogo vya Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja vimefungwa na kuwapa wakati mgumu wananchi wanapohitaji huduma ya polisi wakati vilikuwa vinasaidia kupambana na uhalifu kwa wakati muafaka:-

(a) Je, ni kwa sababu gani vituo hivyo vimefungwa na wananchi kulazimika kupata huduma katika vituo vikubwa kinyume na malengo ya kuanzishwa kwake?

(b) Je, ni kwa nini vituo vya Kilimani, Mkunazini, Mlandege pamoja na vituo vingine vimefungwa na wananchi kulazimika kufuata huduma umbali mrefu?

(c) Je, hatua ya kufunga vituo hivyo inasaidia vii katika kupambana na uhalifu hasa katika maeneo ya katikati ya mji wa Zanzibar na Serikali ina mpango gani na majengo yake?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Eng. Masauni, tafadhalii.

## **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Vituo vya Polisi vimegawanyika katika madaraja matatu, ambayo ni Daraja A, B na C. Utendaji kazi wa vituo hivi unazingatia Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi (*POG*). Mathalani, kwa mujibu wa *PGO* 287(2), vituo Daraja A na B vinatakiwa kufunguliwa na kufanya kazi saa 24 na vituo Daraja C vinatakiwa kufunguliwa na kufanya kazi saa 12 tu kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi 12.00 jioni.

(b) Mheshimiwa Spika, vituo ambavyo havitumiki kwa sasa ikiwemo vituo vidogo vya Mwembeladu, Shaurimoyo na Forodhani inatokana na sababu mbalimbali ikiwemo uchakavu, vipaumbele kwenye mgawanyo wa rasilimali watu na kadhalika.. Aidha, kwa sasa maeneo hayo ambayo yalikuwa yanahudumiwa na vituo hivyo yanahudumiwa na vituo vikuu ya polisi vilivyo karibu.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inapambana na vitendo vya uhalifu maeneo ya katikati ya Mji wa Zanzibar kwa kuimarisha ulinzi, misako na doria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pondeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, amesema kuna upungufu wa maaskari lakini katika Jimbo langu la Chumbuni tuna matatizo sana ya kupatiwa kituo cha polisi. Kuna kituo kidogo cha Polisi ambacho kinahudumia majimbo zaidi ya manne ya Shaurimoyo, Mwera, Mto Pepo na Chumbuni yenyewe ambaao watu wanaoishi pale ni zaidi ya 67,000.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiuliza zaidi ya mara saba au nane humu ndani ya Bunge na nimepata ahadi mara nyingi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri au Wizara kuwa watafanya matengenezo au watakiboresha kituo kile kidogo. Je, yupo tayari kuniahidi au kuiahidi hadhara hii kuwa watakijenga kituo kile kwa kushirikiana na Mbunge?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, mpo tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge kujenga kituo Chumbuni?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhamira yake ya dhati ya kushiriki katika ukarabati wa kituo hicho. Nimhakikishie kwamba tupo tayari kushirikiana naye kuhakikisha kwamba kituo hiki kinafanyiwa matengenezo ili kiweze kutumika vizuri zaldi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay nilikuona, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Yaeda Chini kimejengwa na wananchi mpaka kufikia mwisho, kilichobaki ni nyumba za askari. Je, Serikali ipo tayari kuleta fedha za kujenga nyumba za askari ili kituo hicho kifunguliwe?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei, Mbunge wa Mbulu Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Flatei kwa jitihada zake kubwa sana. Niliwahi

kwenda huko tukashirikiana naye katika kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto hii na ameichukua kwa haraka sana na kufanya kazi, amejenga kituo kizuri tu.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Flatei kwamba Serikali inazithamini sana jitihada zake na za wananchi wa jimbo hilo na hivyo basi katika mkakati wetu wa nyumba za askari nchi zima, tutakapokuwa tumefanikiwa kupata uwezo basi tutashirikina naye vilevile kutatua tatizo hilo la makazi ya askari ili kituo hicho kiwezi kufanya kazi vizuri zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Swalii la mwisho kwa siku ya leo ni la Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini.

Na.458

**Polisi Wanaosumbua Vijana wa Bodaboda wa Nguruka na Uvinza**

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA** aliuliza:-

Vijana wengi wa maeneo ya Nguruka na Uvinza kwa ujumla biashara zao ni pikipiki na Polisi wamekuwa wakiwakamata na kuwatoza faini nyingi vijana hao bila utaratibu:-

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati wa kulielekeza Jeshi la Polisi kuacha mara moja kuwasumbua vijana hao wa bodaboda ambao wanajipatia kipato kuititia bodaboda?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hasna

Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pikipiki za matairi mawili (bodaboda) na matatu (bajaji) zilanza kutumika kubeba abiria kuanzia mwaka 2008 Tanzania Bara na mwaka 2009 Bunge la Jamhuri ya Muugano wa Tanzania iliridhia vyombo hivyo vitumike kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua biashara inayofanywa na pikipiki za kubeba abiria na inathamini mchango wao katika kutoa huduma hiyo ambayo imesaidia sana katika kutoa ajira katika mikoa yote Tanzania Bara. Hata hivyo, si wote ambao wanakiuka Sheria za Usalama Barabarani na Kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limekuwa likichukua hatua dhidi ya waendesa bodaboda wote ambao wamekuwa hawazingatii sheria, kanuni na masharti ya leseni za usafirishaji ikiwa ni pamoja na wapanda pikipiki wa maeneo ya Nguruka na Uvinza. Aidha, Serikali imekuwa ikiendelea kutoa mafunzo kwa waendesa bodaboda juu ya matumizi bora ya barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasna Mwilima, swalii la nyongeza.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini, sambasamba na majibu yake ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, tunatambua kwamba bodaboda baadhi yao ni kweli huwa wanafanya makosa barabarani na wanapofanya makosa barabarani wanatozwa faini ya Sh.30,000, lakini hata magari pia wanapofanya makosa barabarani ambako ni matairi manne pia hutozwa faini ya Sh.30,000. Sasa kwa kuwa tozo hizi zinatokana na Kanuni na Mheshimiwa Waziri anayo mamlaka ya kubadilisha Kanuni wakati wowote, swalii langu, kwa nini

sasa Waziri asibadilishe Kanuni ili bodaboda yenyе matairi mawili pamoja bajaji yenyе matairi matatu waweze kupunguziwa tozo hii ya Sh.30,000 na hatimaye ishuke chini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, tunafahamu kwamba *SUMATRA* huwa wanatoza tozo ya Sh.22,000 kwa bodaboda, lakini Sh.25,000 kwa *hiace* na Sh.120,000 kwa mabasi. Ada hii imekuwa ni kubwa sana kwa watu wa bodaboda ukigawanya 25,000 kwa *hiace* abiria wako 15, ukigawanya hiyo unaipata kila abiria mmoja wa *hiace* analipa 1,666 lakini kwa bodaboda wanalipa 22,000, ukiigawanya kwa dereva na abiria inakuwa analipa 11,000 sasa swali langu, ni kama hili la kwanza, kwa nini sasa hizi Kanuni zisibadilike ili *SUMATRA* waweze kuwatoza angalau 10,000 kwa mwaka badala ya 22,000? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Engineer Masauni, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili muhimu ya nyongeza ya Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nichukue nafasi hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu na umma kwa ujumla kwamba tupo katika hatua za mwisho katika Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani na tunatarajia mchakato huo utakapokuwa umekamilika sheria hiyo italetwa hapa Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge tuweze kuijadili na hatimaye kuipitisha na sheria hiyo itakapokuwa imekamilika itapelekea vilevile kutoa fursa kwa Mheshimiwa Waziri kufanya mabadiliko ya Kanuni kulingana na Sheria itakavyokuwa imepitishwa na Bunge. Katika mambo ambayo tumeona kwamba ni muhimu kuyabadilisha katika Sheria ya Usalama Barabarani, moja, tumeona kwamba Sheria iliyopo sasa hivi inachangia ama inakwaza mapambano dhidi ya kupunguza ajali za barabarani nchini

na moja katika jambo ambalo tuliona kwamba tutalipendekeza katika sheria hiyo ni juu yenu Waheshimiwa Wabunge kuona kama linafaa au halifai ni kuziangalia hizi tozo ambazo zinatozwa kwa hawa watu ambao wanafanya makosa ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, kama wataona kwamba tozo zilizopo sasa hivi ni ndogo na hivyo zinapaswa kuongezwa na kufanya hivyo pengine itasaidia kuwafanya waendesha vyombo hivi waogope, basi nijuu ya Waheshimiwa Wabunge na huo ndiyo mtazamo ambao nauona ni sahihi. Kwa mtazamo wangu mimi, nahisi kwamba baadhi ya waendesha vyombo vya moto wamekuwa wakifanya makosa kwa sababu wanaona wanaweza wakalipa hizi faini kwa kuwa ni kidogo na wanaweza wakalipa mara moja na wakaendelea na shughuli zao. kwa hiyo hili niseme kwamba kwa kuwa litakuja hapa Bungeni, tulipatie muda.

Mheshimiwa Spika, hili linakwenda sambasamba vilevile na swali lake la pili ambalo lilikuwa linazungumzia vilevile masuala ya tozo, ingawa hili la pili linahusiana na masuala ya *SUMATRA* ambayo kwa kuwa Serikali ni moja, basi nina hakika tutakaa pamoja na Wizara ya Uchukuzi ili kuona kwamba mambo haya mawili tutakwenda nayo vipi kwa pamoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mtaona muda hauko upande wetu na sababu ni kwamba leo maswali yalikuwa mengi kuliko kawaida, tunajaribu upunguza yale maswali ambayo yangeweza kuwa ni kiporo kuyaweka sawa.

Sasa Waheshimiwa Wabunge tuendelee na matangazo; mtaona *Gallery* yetu imekuwa ikijaa wageni wengi sana na tunawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kufanya uratibu, tumepata wageni kutoka nchi nzima, kila kona, wakati wote wa Bunge hili, kwa kweli ni wengi, ni wengi, ni wengi kabisa. Kwa Dodoma Bunge ni kivutio cha utalii namba moja, pamoja na kuwa kituo cha mafunzo. (*Makof!*)

Kwa hiyo, ningeendelea kutoa wito kwa Mabunge yajayo Watanzania watembelee hili ni Bunge lao, wafike wakati wowote waweze kujifunza mambo mbalimbali na nitakaa na Sekretarieti ya Bunge kuona namna gani bora zaidi ambayo Watanzania hawa watafaidika katika ujio wao. Wanapata *information* lakini hazitoshi, hazitoshi kabisa, hatuwatendei haki, itabidi lazima tutengeneze *museum* hapa ya historia ya Bunge, namna gani mambo haya ya Bunge yalianza na mpaka leo pamekuwa na nini ambacho kimekuwa kikiendelea na hasa wanafunzi ili wanapotoka hapa wale wa sekondari wakikuta swalii Bunge kwenye mtihani waweze kulifanya bila wasiwasi wowote.

Kwa hiyo tutajipanga ili jambo ili hili tuliweke vizuri, wanakuja kwa gharama kubwa, hatuwezi kuwaacha watu wetu wakija halafu wanaondoka bila kupata uzito wa Bunge ni nini.

Basi, wageni walioko katika jukwaa la Spika, nina wageni wangu kutoka kule Kongwa kwenye Kata ya Lenjulu wanaongozwa na Diwani wa Kata ya Lenjulu Mheshimiwa Sembuli Chilongola, ni wanafunzi 60, naomba wasimame pale walipo, simameni wote, ahsanteni sana, sana na karibu sana, sana. (*Makofi*)

Hawa wanatoka mbali kweli kweli kwenye kona kati ya Wilaya ya Gairo, Wilaya ya Kilindi, Wilaya ya Kiteto na Wilaya ya Kongwa, karibuni sana, karibuni sana mnawenza kukaa. (*Makofi*)

Tunao Wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika kutoka kule Jijini Mbeya wakiongozwa na ndugu Lightness Ndelwa hawa ni *Tulia's Mbeya Strong Women Team*, karibuni sana. Hicho ni kikosi kazi maalum kinaitwa *Tulia's Mbeya Strong Women Team*. (*Makofi/Vigelegele*)

Karibuni sana, karibuni sana kutoka Mbeya.

**MBUNGE FULANI:** Sugu umewaona?

**SPIKA:** Karibu sana kutoka Mbeya, karibuni sana. Ahsante, mnaweza kukaa sasa. Najua Selasini hataki lakini... (*Kicheko*)

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ni Mwenyekiti wa *Tanzania Awards International Limited* Ndugu Julius Deonatus Malegesi. Kribu sana pale ulipo. (*Makof*)

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ni Mwalimu Justine Helron Bake kutoka Nyamagana Jijini Mwanza. Mwalimu huyu ni mwandishi wa kitabu cha *Fast Swahili Course for English and French Speakers*. Karibu sana Mwalimu, karibu sana na hongera kwa kazi nzuri uliyofanya ya kuandika kitabu kwa wanaongea Kifaransa na Kiingereza ili waweze kuongea Kiswahili kwa urahisi. (*Makof*)

Wageni 89 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Waziri wa Kilimo ambao ni Walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Ilasi kutoka Vwawa, Mkoa wa Songwe wakiongozwa na Mwalimu Mkuu Ndugu Emmanuel Sewale. Wale wa kutoka Vwawa karibuni sana, sana, karibuni watoto wetu, karibuni sana, sana. (*Makof*)

Katibu wa Bunge ndiyo haya ninayosema, hebu fikiria watoto wametoka Vwawa hawa lazima wanapokuja hapa wapate kuhusu Bunge vizuri ili waweze kuelewa Bunge ni kitu gani, lazima tujipange vizuri zaidi, karibuni sana watoto wetu mbarikiwe sana na poleni kwa safari. (*Makof*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambao ni Viongozi wa Shirika la Kuhamasisha Kilimo Biashara cha Zao la Mhogo (*CAPAF*) kutoka Wilaya ya Illemela wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Dennis Lekela. Karibuni sana wale kule, hongereni sana kuhamasisha zao la mhogo, tunachotaka soko la mhogo, soko tu, mhogo utakuwa mwingi mpaka mtashindwa hata mahali pa kuupeleka, lakini tunawapongeza kwa vile mnashughulikia jambo hilo.

Ahsante sana Mheshimiwa Mabula kwa kutuletea watu hawa wema. (*Makofii*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Boniventura Kiswaga ambaao ni jamaa zake kutoka Magu, Mkoani Mwanza, Askofu Yohana Nhumba na ndugu Dominique Bubeshi. Karibuni sana Baba Askofu, karibu sana na Dominique. (*Makofii*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Anna Lupembe kutoka Kanisa la *EAGT* la Maranatha *Temple* lilioko Makambako Mkoa wa Njombe wakiongozwa na Mchungaji Yonah Mwakajaba. Karibuni sana wale wote kutoka Makambako. (*Makofii*)

Wageni 69 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambaao ni Kwaya ya Msifuni Emmanuel kutoka Singida wakiongozwa na Msaidizi wa Askofu Mchungaji Syprian Hilinti. Wanakwaya kutoka Singida, karibuni sana, sana majirani kutoka Singida. (*Makofii*)

Wageni 39 wa Mheshimiwa Joram Hongoli ambaao ni Kwaya ya Sinai ya Kanisa la KKKT Mkoa wa Njombe wakiongozwa na Ndugu Hans Luwanja, Njombe, karibuni sana wale wote mliotoka Njombe, karibuni sana, sana. Kwa kweli mtaona jinsi ambavyo Watanzania wanatoka kona zote za nchi yetu kuja kulitembelea Bunge letu, hii ni alama ya upendo mkubwa sana walionao. (*Makofii*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Joseph Mkundi ambaao ni ndugu zako kutoka Mkoa wa Shinyanga na Dodoma wakiongozwa na Ndugu Majuta Anthony wale kule, ahsanteni sana. (*Makofii*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ambaao ni Wawakilishi wa *Tanzania Village for Youths Development Association* kutoka Wilaya ya Chamwino hapa Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti Salim Mpandangido. Karibuni sana popote pale mlipo maana *gallery* zimejaa wengine inawezekana wamekosa nafasi. (*Makofii*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Mbarak Dau kutoka Taasisi ya kujitolea ya *ARASY RELIEF* ya nchini Malaysia wakiongozwa na Ndugu Abdulla Yazid ndugu zetu kutoka Malaysia, wale kule karibuni sana, karibuni sana kutoka Kuala Lumpur, karibuni sana, kweli hawa ni Wamalaysia, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Margaret Sitta kutoka Taasisi ya *Friends and Family Community Connection* iliyoko Jimbo la California nchini Marekani ambao ni walezi wa Kituo cha Watoto Yatima cha Huruma kilichoko Urambo, Mkao wa Tabora wakiongozwa na Rais wa Taasisi hiyo ndugu Phil Hariris, karibuni sana, sana ndugu zetu kutoka California nchini Marekani. (*Makofi*)

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Sebastian Kapufi ambao ni Madlwani kutoka Halmashauri ya Mji wa Mpanda Mheshimiwa Nestory Zacharia, Mheshimiwa Rajabu Iddi Mrisho na Mheshimiwa Remmy Matongo, karibuni sana wale wa kutoka Mpanda popote pale mlipo. (*Makofi*)

Wageni 10 wa Mheshimiwa Innocent Bilakwate ambao ni mtoto wake Ibrahim Innocent Bilakwate pamoja na marafiki zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada *Chapel* ya Bunge anawatangazia wale Waumini wa Kikristo kwamba kutakuwa na Ibada leo baada ya saa saba eneo la wazi la *basement* Mchungaji Yonah Mwakajaba wa kutoka Makambako Njombe Kanisa la *EAGT Maranatha Temple* ndiye atakayekuwa analisha neno.

Waheshimiwa Wabunge kundi la kwanza la Wabunge kama hamsini hivi lilitokwenda Misri wamerudi jana kutuwakilisha Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru sana kwa kazi kubwa waliyofanya ya kwenda kuwatia moyo vijana wetu. Mashindano yale ni makubwa ya Afrika, ni magumu, lakini Waheshimiwa hawa wamejitoa kwa gharama zao kwa kiasi kikubwa na niwaambie Watanzania hamna hela ya umma iliyotumika katika safari hii. Kwa hiyo tunawapongeza

sana kwa kazi kubwa ambayo wamefanya sana, sana, ya kuwapa moyo vijana wetu. (*Makofi*)

Wenzetu wako kule kwa *presence* kubwa na majirani zetu wa Kenya wanasubiri siku ya mechi ya Kenya na Tanzania nilikuwa na viongozi wao kule, wao wanaongozwa na Raila Odinga na Waziri wa Michezo na wengine wako pale na *presence* yao ni kubwa. Unajua katika Afrika Mashariki kuna wenzetu ambao huwa wana ile *pompous*, ile wakiwasili mahali unaona ile kwamba wamefika na sisi Watanzania tuna ile ya unyonge unyonge, sasa tunataka tuondokane na ile unyonge unyonge. Walipofika waliwakuta Watanzania nao wapo, pamoja juhudhi zilizofanyika Wabunge walishangilia timu yetu mwanzo mwisho kabisa, kabisa na lile jukwaa kuu kila mtu aliona kwamba Watanzania wapo katika jezi zao, katika rangi zao na bendera zetu, ni jambo limetia moyo sana, nawapongeza sana. (*Makofi*)

*Group* ya pili ya Wabunge thelathini inaondoka kesho kwenda Misri kwa ajili ya mechi mbili zinazofuata, kwa kweli nawapongezeni sana Waheshimiwa Wabunge mmejitoa kweli kweli kwa ajili ya timu yetu na hasa baada ya miaka karibu 40.

#### **MBUNGE FULANI:** Kweli.

**SPIKA:** Kutokopata nafasi kama hii lazima fursa kama hii inapotokea tuishike kwa mikono miwili na niwaombe Watanzania wengine ambao wana uwezo wa kwenda Misri hapa wala si ghali kihivyo, waweze kwenda kule, tuipe moto timu yetu, tuishaingilie, hii itatufanya hata wakati ujao tuweze kufanya vizuri zaidi. Yako mambo ya kuweka sawa tutaongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, yako mambo mawili, matatu ambayo kidogo hayako vizuri, lakini ni ya kurekebisha hapa na pale kwa upande wa kule kule kwa kadri tulivyoona na maoni yetu yatakavyokuwa.

Kwa hiyo, nawatachia hawa wa *batch* ya pili na wenywewe waende salama, warudi salama na baada ya

hapo itatusaidia Waheshimiwa Wabunge katika eneo la michezo kwa bajeti zinazokuja mwakani na kadhalika naamini tutajipanga vizuri zaidi. Huko tunakokwenda kwa upande wa timu ya Taifa, Waziri wa Fedha na Mipango, ni lazima atenye pesa kwa ajili ya Timu ya Taifa. Kabisa, mwakani hapa hatuelewani, baada ya makundi makubwa namna hii ya Wabunge kwenda halafu mwakani pawe hakuna hela kwenye michezo, kwa maana ya Timu ya Taifa, haiwezekani! (*Makofi/Vigelegele/Kicheko*)

Hawawezi kuwa wanatutambia kiasi hicho, hatusemi tupange kama za kwao, lakini *at least* kiasi fulani hivi lazima tutenye, tuimarishe michezo, michezo ndiyo inajenga zaidi Utaifa, inajenga sana uUzalendo, inatangaza nchi hata kiutalii na kadhalika. (*Makofi*)

Nchi ya Misri wanategemea michezo hii itawaletea uchumi wa wastani wa dola milioni 40 kwa *tournament* hizi tu zinazofanyika wakati huu. Kwa hiyo michezo ni ajira, michezo ni chanzo cha mapato, michezo ina mchango wake mkubwa sana katika maendeleo ya Taifa. (*Makofi*)

Basi baada ya hapo, naomba sasa tuendelee.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**SPIKA:** Mwongozo ni mmoja tu karibu, ni Mheshimiwa nani?

**MBUNGE FULANI:** Chacha.

**SPIKA:** Ooohhh sawa, Mheshimiwa Chacha nimekuona tafadhali.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) lakini Kanuni ile ya 42(1), Kanuni ya 42(1) naomba niisome inasema; wakati swali linalohusika litakapofikiwa katika orodha ya shughuli Spika

atamwita Mbunge mwenye swalii hilo, au kama hayupo Spika atamuita Mbunge mwengine yeote aulize swalii hilo kwa niaba ya Mbunge mwenye swalii, Mbunge mwengine yeote.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na *tendency* au kautaratibu kwa Wabunge wa CHADEMA ambao hawapo wanauliziwa swalii au maswali yao na Mbunge mmoja tu kila siku, kila siku Mbunge mmoja na ilihali CHADEMA ina Wabunge wengi.

**MBUNGE FULANI:** Enhe!!

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, sasa nikataka nijue kwa mujibu wa Kanuni hii je, huu siyo, si kuvunja utaratibu wa Kibunge? Ahsante. (*Kicheko*)

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Mbona kwanza....

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** 68(7) Piga hiyo, sawa eheheh.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Jamani mbona hamkuwepo mwanzoni, sasa tena miongozo inatoka wapi? Ni kwa hili hili au mna miongozo mingine? (*Kicheko*)

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Hapana, mwongozo mingine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere ni Mwongozo mwengine, sawa. Mheshimiwa Sugu ni Mwongozo mwengine au huu huu?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Subiri kwanza Mheshimiwa. Mheshimiwa Sugu ni lingine au hili hili?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ni lingine.

**SPIKA:** Ni lingine, sawa, ahsante, kaa basi.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda...

**SPIKA:** Ngoja kidogo sijakupa nafasi. Mheshimiwa Selasini ni Mwongozo mwingine au hili hili?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, mwingine.

**SPIKA:** Sawa. Haya, basi nawaruhusu ninyi watatu tu asiongezeke mwingine. Tunaanza na Mheshimiwa Selasini maana ni *Chief Whip* huyu.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, Timu ya Taifa inahitaji uhamasishaji kutoka kwa watu na taasisi mbalimbali kwa sababu imeibeba nchi. Kama ulivyokuwa kule Misri viongozi mbalimbali wa nchi ambazo timu zao ziko pale wapo wanatia hamasa timu zao ili ziweze kufanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini timu yetu hapa Tanzania tunamwona Waziri wa Michezo yuko hapa na Naibu wake yuko hapa nchini, sasa katika hali ya kawaida kisaikolojia wachezaji wakiona viongozi wao wakubwa wako pamoja nao bila fedha, bila nini wanapata hamasa. Naomba mwongozo wako ni kwa nini uongozi wa Wizara ya Michezo hauko Cairo kuwaunga mkono wale vijana wetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii vilevile kukupongeza wewe kuonesha mfano pamoja na Wabunge wako katika kuhakikisha kwamba Timu ya Taifa imefanya vizuri. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Sugu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kulizungumzia suala hili, kwa kweli linaumiza sana, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba niendelee. Katika mikoa inayolima pamba msimu umeanza kwa bei elekezi ya Serikali shilingi 1200. Kwa muda mrefu sana hili zao la pamba limekuwa na matatizo mengi wakati wa ununuzi msimu unapokuwa umefika. Kwa sasa wakulima wote wa pamba hasa Wilaya ya Bunda na Jimbo la Bunda watu wanapeleka pamba kwenye vituo vya kununulia pamba lakini hakuna wanunuzi, bei ya pamba haljulikani mara shilingi 1200, mara waambiwe tunakupa shilingi 850. Tatizo hili la ununuzi wa pamba limekuwa kubwa na linaendelea kuwa kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tamko la Serikali wanataka wakulima wafanye nini ili kuza pamba yao au nini kinafanyika? Sasa hivi wakulima wanaenda kununua pamba hakuna hela wala wanunuzi. Tunaomba kupata majibu ya Serikali nini kifanyike sasa kwenye zao la pamba?

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ni mambo matatu yamejitokeza, la kwanza la Mheshimiwa Chacha kuhusu upande wa CHADEMA mtu mmoja tu kuuliza maswali natumaini wamesikia, watagawana gawana kidogo huko tunakoenda, inaelekea wengine labda wanaogopa kuuliza maswali, kwa hiyo wamesikia.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu pamba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pia amesikia, muda sio mrefu nitampa nafasi Naibu Waziri, Mheshimiwa Mgumba kuanza kuchangia masuala yanayohusiana na bajeti hapa, natumaini atatumia dakika zake saba pamoja na mambo mengine kuongelea

pamba pia. Kwa hiyo, nakuomba vile ulivyojipanga utagusia pia na suala la pamba.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu *AFCON* nimsemee kidogo Mheshimiwa Waziri, kwa kweli tumekuwa tukiwasiliana naye muda wote kabla, wakati na hata tukiwa Misri. Hakubaki hapa nchini kwa sababu ya kubaki tu amekuwa akifanya kazi kubwa sana ya kusukuma mambo kule. Kama na yeze angekuwa kule, nina hakika baadhi ya mambo mengi sana yangeweza kukwama. Kwa hiyo, ilikuwa ni muhimu sana awepo hapa nchini ili kuweza kusukuma baadhi ya mambo mengi sana ambayo ameweza kuyafanya akiwa hapa nchini. Hata hivyo, kwa vile yeze mwenyewe yupo, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe kama utapenda kutumia dakika tatu sio mbaya, nakupa Mheshimiwa, tafadhali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuongea.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitumie nafasi kuwapongeza Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiongozwa na wewe Mheshimiwa Spika kwa kuiwakilisha nchi kwenye mashindano makubwa ya *AFCON* nchini Misri tena kwa uzito stahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu ushiriki wetu sisi kwa mara ya kwanza baada ya miaka 39, tulikuwa hatuwezi kabisa hata kubajeti kwa ajili ya Timu ya Taifa kwa sababu tulikuwa hatuwezi kufika huko. Kwa hiyo, unaweza kufikiria tu mwaka jana ningeweza kuomba pesa hiyo ningonekana kichaa lakini kwa mara ya kwanza tumeingia huko na ndiyo maana uliniona pamoja na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikabidi tuitishe hata harambee kuhakikisha kwamba timu yetu isiadhirike zaidi. Siyo kwamba ilikuwa hakuna pesa kabisa, hapana, pesa ya kwenda na kukaa, posho ya kawaida ilikuwepo lakini huu ni ushindani mkubwa ambao tulihitaji tuwape vijana wetu motisha na ndiyo maana chochote tunachopata sasa hivi

kinagawanywa kwa wachezaji wetu 23 na kuingizwa kwenye akaunti zao, ndiyo tunachokifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kuna maneno mengi yanasemwaa kuhusu kocha, mimi napenda tuwe na mjadala mpana baada ya mashindano haya ili tuisiwakatishe tamaa hawa vijana wetu kama ulivyo sema mwenyewe Mheshimiwa Spika. Ila kuna kitu kimoja ambacho watanzania na sisi lazima tuijangalie.

Mheshimiwa Spika, miaka miwili iliyopita uongozi wa *TFF* ulivyobadilisha kanuni ya kuruhusu wachezaji wa nje zaidi ya watano (5) wakawa 10 na wote 10 wanaweza wakacheza ndani ya uwanja kazi yetu Watanzania sisi kuvunja matawi na kushangilia tumeshinda, niliwaambia hilo lilihitaji mjadala kwa sababu linagusa sera za kitaifa za ajira. Mpira ni kiwanda, ni ajira kama ajira zingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulichokuwa tumeomba ni kwamba tuwe na mjadala mkubwa kitaifa ili tuwe na mpango mkakati kuhusu soka la nchi. Ndiyo maana leo hii timu zetu kubwa Yanga na Simba ambazo ndizo zinazalisha wachezaji zinategemea wachezaji wa nje kwa ajili ya *midfielder* ndiyo shida hiyo.

**WABUNGE FULANI:** Kwa hiyo?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, la mwisho.

**MBUNGE FULANI:** Siyo kweli.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, naona Mheshimiwa anataka kuongea yeye.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri atufafanulie.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:**

Mheshimiwa Spika, nimalizie, kwenda kwangu mimi siyo kitu muhimu sana lakini la msingi ni kwamba Taifa letu liliwakilishwa na mmoja wa viongozi waandamizi wa nchi hii, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi ndiyo maana nikaona niwakilishwe na mjumbe wa CAF na Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa ambaye mchango wake ulikuwa mkubwa zaidi kuliko hata wa kwangu kwa sababu ulikuwepo Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niwapongeze sana vijana wetu wa Taifa Stars kwa matokeo yaliyotokea kwa sababu tumecheza na timu ambayo ni namba moja katika Bara la Afrika, ni namba 22 katika dunia na hatujaweza kuingia kwenye AFCON kwa zaidi ya miaka 30. (*Makof*)

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, namuona Mheshimiwa Susan amesimama, Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumpa taarifa mzungumzaji ambaye ni Waziri wa Michezo kwamba kule ingekuwa bila jitihada za watu binafsi hakuna bendera, hakuna chochote cha uhamasishaji na ye ye ndiyo Waziri wa Michezo na Utamaduni, hali ni mbaya mno tukitofautisha na mataifa mengine hakuna jitihada zozote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa pamoja na kuwa mhimili wa Bunge ukiongozwa na wewe Spika wetu tulikwenda lakini ye ye alistahili kusaidia shamrashamra ili Spika wetu upambwe na Wizara hii. (*Makof*)

**SPIKA:** Sasa naomba tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri tumalizie ili tuendelee na ratiba ya leo. Mheshimiwa Waziri kama unataka ku-*wind up*.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba basi wenzetu upande  
wa pili wanisikilize wakati naongea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe na  
utulivu jamani.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**SPIKA:** Naomba utulivu jamani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri basi inatosha ili tuweze  
kuendelea.

Waheshimiwa Wabunge, natumaini tumeelewana  
kwa ujumla yaani kwamba wote kama Bunge tuna uchungu  
na nchi yetu na vijana wetu, si ndiyo?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo. (*Makof*)

**SPIKA:** Kwa hiyo, Serikali wamesikia, kwa kweli  
Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana mimi najua jinsi  
ambavyo umekuwa ukipambana na naamini wakati  
mwingine jambo hili linakufanya hata unakosa usingizi. Hata  
hivyo, tumwombe basi Mheshimiwa Waziri Mkuu vyovyyote  
itakavyokuwa kama Waziri wa Michezo anaendelea kuwa  
hana, Naibu anaendelea kuwa hapa haitoi picha nzuri.  
(*Makof*)

Tumsaidie Waziri wetu kwa yale ya hapa nchini tuyafanye sisi, Waziri aondoke kwenda *AFCON*, itapendeza zaidi. Hili jambo ni la kitaifa linagusa vijana wetu wengi sana, ni jambo kubwa mno, kwa hiyo, ni vizuri liende hivyo. Wabunge wanaondoka kesho kama nilivyosema, wakienda peke yao wakarudi tena peke yao halitoi pitcha nzuri. (*Makof!*)

Waziri wa Fedha, hili jambo hili, tulikwambia wakati wa Kamati ya Bajeti. Wale Wajumbe wa Kamati ya Bajeti hamkumbuki jamani?

**WABUNGE FULANI:** Tunakumbuka.

**SPIKA:** Hamkuwepo siku ile ya Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Mukasa hayupo leo. Walimwambia Waziri wakati tunaangalia namna ya kumalizia hii miezi mitatu, si mnakumbuka, kwamba hakuna fedha kwa ajili ya Timu ya Taifa wakajibu kwamba fedha zipo. Wakasema hapana hizi ni za *Under 17* siyo za *National Team* lakini pakawa na, tungeweza katika ngazi ile tukarekebisha kidogo hili pia.

Kwa hiyo, Waziri wa Michezo jamani mtamnyonga bure wakati mwingine na yeye hawezikusema kila kitu. Sasa tunataka kwa mwakani Waziri wa Fedha tusifike hapa tena tulipofika, kama safari ijayo tutakuwa tume-*qualify* kwa vyovyote vile Timu za Taifa ni timu za Serikali. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, ndio Timu ya Taifa ni ya Serikali. Haliwezi kuwa jambo la kitaifa halafu Serikali haipo, haiwezekani. Kwa hiyo, ni vizuri Wizara ya Fedha mkajua Timu ya Taifa Serikali mbele, wadau wanasadida, wanaunga mkono, wapambe nini lakini Serikali yenyewe inashika bango kwa sababu ni timu yake. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana, tumefika pazuri wala haina shida. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mpenzi namba moja wa michezo, yeye mwenyewe ni *coach*, anatamani hata angekuwa kule ai-*coach* yeye mwenyewe hakuna haja ya Amuneke wala nini. (*Kicheko*)

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu tunajua unatusaidia sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda ulipofika sasa tuendelee, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku muhimu sana ambapo kikatiba na kikanuni tunapaswa jioni ya leo saa 11 kamili kila mmoja wetu awe amekaa hapa Bungeni kwa ajili ya kupitisha bajeti ambapo tutaitwa jina Mbunge mmoja mmoja na kupiga kura yake ya kukubali, *ku-abstain* au kukataa. Kwa hiyo, nawaombeni saa jioni 11 kamili wote kabisa tuwe hapa ili tuweze kupiga kura hiyo muhimu kikatiba na kikanuni, ni siku muhimu sana leo.

Kwa hiyo, hapa tulipofikia sasa ni mahali ambapo tutamsikiliza mto hoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mpango, Dkt. Mpango ili aweze kutoa majibu ya hoja zenu mlizozitoa wiki nzima pia apate kuhitimisha hoja yake aliyoiweka mezani. Kabla ya Mheshimiwa Dkt. Mpango hajaongea kuna Mawaziri au Naibu Mawaziri ambao watatangulia kuongea kidogo kupunguza angalau sehemu fulani ya maelezo yake. Yeye mwenyewe tutampa saa moja lakini watakaomtangulia watasaidia kupunguza sehemu ya maelezo ambayo atakuwa anapaswa kuyatoa.

Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Mgumba una dakika 7 na wengine watafuata kadiri nitakavyowataja.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii muhimu ilio mbele yetu kuhusu bajeti ya Serikali na hali ya uchumi. Nichukue nafasi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya na uzima nimepata nafasi hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja asilimia 100 kwa sababu ya mambo mazuri yaliyokuwepo ndani ya suala hili. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara ya Fedha na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, nianze kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwenye hoja zile zinazohusu sekta ya kilimo na nitatoa ufanuzi wa hoja chache lakini tuwaahidi kwamba michango yao yote ina umuhimu mkubwa kwa mustakabali wa kilimo chetu nchini lakini kwa maendeleo ya Taifa letu. Michango yote tutaifanyia kazi na wale ambaeo hoja zao nitakuwa zijazigusa kutokana na muda basi Wabunge wote mtazipata kwa maandishi ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa hoja ya pamba uliyosema maana muda wenyewe ni mchache nisije nikamaliza kabla sijagusa suala hilo. Kwanza, ni kweli soko la pamba haliendi mwendo mzuri na tumefungua msimu tangu tarehe 2 Mei lakini mpaka sasa mwenendo wake sio mzuri. Tulishatoa bei elekezi ya Sh.1200 lakini kwa bahati mbaya wakati bei ile inatoka soko la dunia bei zilianza kushuka hasa kutokana na vita vya kibashara katika ya nchi ya China na Marekani, kwa sababu nchi ya China ndiyo watumiaji na wanunuzi wakubwa wa pamba na nchi ya Marekani pamoja na kuwa ni wazalishaji wakubwa wa pamba nao wanawauzia China lakini pia ndiyo wanunuzi wakubwa wa nguo kutoka China.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutokana na msuguano wao na kuwekeana vikwazo, huyu amekataa kununua nguo za kutoka China mwingine amekataa kununua pamba

kutoka nchi ya Marekani. Kwa hiyo, wanapogombana mafahari wawili nyasi zinaumia na sisi huku nchi za Afrika ndiyo tunaumia ikiwemo Tanzania na bei imeendelea kushuka mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, wakati tunapanga bei pamoja na wadau na wanunuzi bei katika soko la dunia ilikuwa ni zaidi ya dola senti 0.75, leo hii tunapozungumza ni dola senti 0.66 zaidi ya dola senti 0.9 imepungua. Kwa hiyo, wanunuzi kama tunavyofahamu ni wafanyabiashara wameshindwa kuingia sokoni na wameshindwa kupata mikopo kwenye taasisi za fedha hasa mabenki kwa sababu mabenki wamekataa kuwapa mikopo kwa sababu wanassema huwezi kuwapa mikopo wakati kwenye biashara hii anaenda kutengeneza hasara.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali tumefanya vikao mbalimbali na kikao cha mwisho kimefanyika siku tatu zilizopita Dar es Salaam na wanunuzi wote tumekubaliana kwamba wataingia sokoni kununua kwa bei ileile Sh. 1200 na Serikali tumeweza kudhamini mikopo yao kutoka kwenye benki na tumewaelekeza kwamba wasiuze pamba hiyo mpaka mwezi Agosti, kama watauza pamba hiyo kwa hasara Serikali tutafidia hilo *gap* la hasara lakini bei iendelee kuwa Sh.1200. Kwa hiyo, sasa hivi wako kwenye harakati mbalimbali za ku-*finalize* na benki ili wapate hela wataingia sokoni muda siyo mrefu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo imezungumzwa na watu wengi ni kuhusu bajeti ndogo ya sekta ya kilimo. Kwanza, tunavyofahamu bajeti yetu ni *cash budget* tunakwenda kutumia kutohana na tulichokipata lakini kama Serikali kila mwaka tumeendelea kuiongeza bajeti hii. Mwaka uliopita 2018/2019 katika Wizara ya Kilimo bajeti ilikuwa ni shilingi bilioni 204 lakini mwaka huu tumewekewa zaidi ya bilioni shilingi 254, kuna ongezeko la shilingi bilioni 50 kwa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, pia sekta ya kilimo ni mtambuka, usiangalie tu kwamba Wizara ya Kilimo. Tumesema mapinduzi

ya kilimo yataongozwa zaidi na *ASDP* // ambaayo inatekelezwa na Wizara zaidi ya name. Kwa hiyo, ni vema kuangalia na bajeti hizo za Wizara zingine ambazo zote zinakwenda kusherehesha suala la kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la bajeti ya Wizara ya Viwanda, Wizara ya Ardhi, kwa sababu kilimo huwezi kulima kwenye angani, unatakiwa kulima ardhini. Kwa hiyo wanapoenda kupima mashamba na maeneo ya kilimo wanatekeleza *SDP* // . Kuna Wizara ya Uvuvi na Mifugo, Wizara ya TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, zote hizi bajeti zao pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii upande wa misitu ambao ndiyo kilimo chenyewe, zote zinatatekeleza *SDP* // mapinduzi makubwa ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika sisi Wizara ya Kilimo tuna taasisi zaidi ya 22, bajeti zake haziko hapa kwenye billoni 254, hizi bajeti zake ziko kwenye Mfuko wa Hazina kwa sababu hizi taasisi zetu nyingine zinarioti kwenye Mfuko wa Hazina. Tuna bajeti zaidi ya bilioni 69 kuanzia Bodi za Mazao pamoja na taasisi nyingine. Pia tuna makusanyo mbalimbali, mapato mbalimbali kwenye Bodi zetu, kama wanavyofahamu kule kwenye pamba tuna Sh.100 kwa kilo kwa ajili ya Mfuko wa Pembejeo na Bodi nyingine ziko kama hivyo. Zote hizi zinakwenda kutekeleza bajeti ya kilimo, kwa hiyo kwa bajeti ya kilimo ni pana sana huwezi kuiona tu kwenye Wizara moja hii Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, la tatu, wamechangia Wabunge wengi kwenye suala la uwekezaji kwenye kilimo cha umwagilaji kwamba ni kweli na wengine wamefika mbali, wanasema kwamba Serikali hajifanya jambo lolote kabisa, si kweli Waheshimiwa Wabunge. Kama wanakumbuka huko nyuma Serikali katika baadhi ya mikoa tulikuwa tunapeleka chakula cha msaada, upungufu wa chakula.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jafo, dakika tano.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuunga mkono hoja hii ambayo imeletwa na kaka yangu Mheshimiwa Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango. Kulikuwa na mambo kadhaa yamejitokeza yanayohusu Ofisi ya Rais, TAMISEMI na suala zima la bajeti kwa ujumla na hasa hoja kubwa iligusa suala la *TARURA* bajeti ni ndogo. Tulijadili hapa kwa kina na niseme wazi kwamba ni kweli, hata hivyo fedha nyingi zilizotengwa kwa ajili ya kuimarisha miundombini zaidi shilingi bilioni 284.7 ambayo kwa imani yangu ni kwamba kwa usimamizi wetu mzuri tutahakikisha tunafanya mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Bodi ya Mfuko wa Barabara sasa hivi wanapitia ile *formula* ya 30% kwa 70% kwa lengo kubwa nini kifanyike kuhakikisha kwamba mtandao wa barabara wapo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao unahudumiwa na *TARURA* ambao takribani kilomita 127 ziweze kuwezeshwa vizuri, zikafanye kazi vizuri. Kwa hiyo naomba niwahakikishe Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali inafanya kazi hii ndiyo maana mkiona sehemu mbalimbali kazi kubwa inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa elimu katika bajeti yetu niliyowasilisha hapa ni zaidi ya shilingi bilioni 58.24. Hii ni program ya *EP4R* kwa ajili shule za sekondari ambayo naona kwamba huko tuna mafanikio makubwa sana. H

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika pia Mradi wa Kuboresha Mpango wa Elimu ya Sekondari kupitia *SEDP* tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 48.99 katika bajeti ya mwaka huu. Hali kadhalika mpango wa *EP4R* kwa ajili ya shule za msingi tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 31.84 ambayo Waheshimiwa wataona ni kwa jinsi gani tunaenda kuitekeleza mipango hiyo katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa afya, naomba tuseme wazi kwamba tunaona juhudhi kubwa ya Serikali, tumesikia hoja mbalimbali hapa lakini Serikali imefanya kazi kubwa sana. Ukiachia ujenzi wa hospitali 352 katika bajeti iliyopita, lakini mwaka huu tunaona kwamba tuna ujenzi wa vituo vya afya 352, lakini mwaka huu tuna vituo vya afya tena karibuni 52. Tunaendelea na ujenzi wa hospitali za wilaya 67, lakini hali kadhalika tuna hospitali mpya takribani 27. Kwa hiyo Waheshimiwa wataona katika mpango wa miaka miwili ujenzi wa hospitali 94 kwa mara ya kwanza ni *outstanding performance* kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambalo hili lazima tuna kila sababu ya kujisifu kama toka uhuru mpaka 2015 tulikuwa na hospitali 77 peke yake, lakini mpango wa miaka miwili, hospitali 94, tumevunja rekodi ambayo haijawahi kutokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba nizungumze wazi, kwa mfano unaona kwamba kila mjambe alikuwa anazungumza kwamba bajeti hii ilikuwa inajali vitu, mimi niseme kwamba bajeti hii inajali watu. Katika hospitali tulizojengwa kila moja ilikuwa inachukua takribani wataalam ambao wameajiriwa katika eneo siyo chini ya 20. Leo hii tunapozungumza hospitali hizi 97, vituo vya afya 52, ukizidisha mara 20 unaona jinsi gani watu huko wanaenda kuguswa katika soko la ajira, lakini hata katika utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika upande huu wa sekta ya elimu ambayo tuna miundombinu na tunatumia *force account*, unaona kwamba bajeti hii inaenda kuwagusa watu kwa kiwango kikubwa sana. Ndiyo maana nimesema kuwa bajeti hii ukisema ni ya vitu hapana, bajeti hii kwa ajili ya watu kwa sababu inaenda kutengeneza miundombinu, lakini hali kadhalika inawagusa watu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba bajeti hii ambayo safari hii imekuja kujibu hasa matatizo ya Watanzania na imani yangu kubwa kwamba sisi Wabunge kwa umoja wetu tunaweka historia kwamba kutengeneza bajeti ya kihistoria

ambayo haijawahi kutokea katika miaka hii ya karibuni, inawezekana. Lengo letu kubwa ni tuipe *support* bajeti hii, tulunge mkono, halafu katika utekelezaji wa bajeti hii twende tukaisimamie vizuri kwa mustakabali mpana wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ajenda ya mwisho ilikuwa ni suala zima la vitambulisho vya wajasiriamali wadogo. Hili tumepokea changamoto mbalimbali hasa kero zinazotokea kule *site*, japokuwa maelekezo yalikuwa yamekuwa wazi kwamba lazima mfanyabiashara yule mdogo mauzo yake yasizidi milioni nne. Hata hivyo, katika utekelezaji wa jambo hili kila mtu alitafsiri kivyake, ndiyo maana unaona mikoa mingine imetulia, mikoa mingine ina changamoto. Jukumu letu ni kuangalia wapi kuna matatizo ili tuweze kuyarekebisha na lengo kubwa ni kwamba kila mfanyabiashara ambaye ni mdogo aweze kushiriki vizuri lakini hali kadhalika kutoa kadhia mbalimbali ambazo wananchi wetu zinawakabili.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache kwa sababu dakika zangu ni tano, naomba nikushukuru sana na naomba kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia yote mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, una dakika saba.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu ili niweze kuchangia bajeti kuu ya Serikali. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kama Waziri wa Viwanda na Biashara naomba uniongezee dakika moja ya kushukuru. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuendelea kuamini vijana kwamba tunaweza kuweka mchango mkubwa katika Taifa hili. Mheshimiwa Rais Mwenyezi Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru Makamu wa Rais, Waziri Mkuu pamoa na wewe, pamoa na Bunge kwa *support*

ambayo mnaendelea kunipa katika kutumika wananchi na kutumia Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru sana kwa michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa katika kuchangia hii bajeti kuu ya Serikali. Michango mikubwa ambayo inahusu Wizara yangu imejikita zaidi kwenye masoko ya uhakika kwa mazao ya wakulima wetu na nitatumia muda mwingu kuzungumzia hili kwa sababu ya umuhimu wake. Mheshimiwa Rais wetu amekuwa akizungumzia nia ya kuunganisha kilimo na viwanda kwa sababu tukifanya hivyo tutawainua wakulima wengi nchini kwenda kwenye uchumi wa kati, kwa hiyo hoja yangu imejikita zaidi kwenye *industrialization agriculture*.

Mheshimiwa Spika, nikianza na mazao ya kimkakati, hata leo imetolewa mwongozo kuhusu zao la pamba. Pamoja na jitihada nzuri za Serikali kusaidia *Ginners* nchini, lakini wakulima wetu wamehamasika kwenye upande wa zao la pamba, uzalishaji umetoka tani 222,000, msimu huu tunategemea kuvuna tani zisizopungua 400,000.

Kwa hiyo kuendelea kutegemea *Ginners* peke yao kama soko la wakulima wa pamba hatutaweza kutoka kwenye mkwamo wa bei kushindwa kupanda. Kwa hiyo katika hili Serikali tumeazimia kuhakikisha *textiles* ambazo zilibinafsishwa lakini hazifanyi kazi, baada ya Bunge hili naanza nao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, *Textiles* nchini zilikuwa 32, sasa hivi zimebakia tano ambazo zinafanya kazi, wengi wamekiuka mikataba ile ambayo walisaini kwa mujibu wa ubinafsishaji. Sasa Serikali tunataka kuhakikisha *textiles* hizi zinafanya kazi ili wakulima wa pamba wanapolima, tusitegemee tu kwamba *Ginners* liwe soko peke yake. Ile sera ya *C to C* (*Cotton to Cloth*) sasa tunaanza kwenda kwa vitendo kuhakikisha mkulima anapovuna shamba, soko lingine linaenda kwa *Ginners* lakini soko lingine linaenda kwenye *textiles* ili ziweze kutengeneza *garments*, ziweze kutengeneza pamba nyuzi na wakulima wetu wapate soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, nitumie nafasi hii kutoa *clarification* kuhusu zao la korosho. Kumekuwa kuna upotoshaji mkubwa sana na upotoshaji huu umepelekea dunia kuamini kwamba korosho yetu imeoza kumbe siyo kweli. Baada ya kuapishwa nimetumia wiki nzima nikienda ghalia kwa ghalia kwenye mikoa inayolima korosho, korosho yetu iko katika hali nzuri.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge niwaombe tuweke utaifa mbele na uzalendo mbele, hakuna korosho ambayo iko *reject* hata moja, korosho yote ni *grade I* na *grade II*. Sasa tunapowasiliana na wanunuzi duniani kuna watu bado wanaendelea kupotosha kwamba msinunue korosho ya Tanzania siyo safi.

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge hili kuwaambia wananchi, Serikali *is open for business*, korosho yetu ina ubora, Waheshimiwa Wabunge wanaotoka kule wanajua. Tuwe wamoja, tushirikiane Taifa moja kuhakikisha tunawasaidia wakulima wa korosho, tutoe hii korosho lakini msimu unaokuja tukijipanga vizuri hata zao la korosho bado lina *potential* kubwa ya kuwasaidia wakulima wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sababu ya muda niseme kwamba kuhakikisha viwanda vilivyobinafsishwa vinaanza kufanya kazi, lakini pia tunafungua fursa za masoko za kimataifa kwa kushiriki katika *forum* za kimataifa kama *World Economic Forum*, kuhakikisha tunashirikiana na Balozi zetu, kuwa na mkakati mzuri wa kutafuta masoko ya uhakika. *TANTRADE* tunai-reform upya ili iweze kujikita katika kuhakikisha inakuwa *interface* ya nchi na dunia kutafuta masoko ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Mheshimiwa Mpina, Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Mheshimiwa Japhet Asunga, Waziri wa Kilimo tumejipanga katika kuhakikisha tumejipanga katika kuhakikisha tunafungamanisha hizi sekta na kuhakikisha tunaongoza Serikali na Watanzania kwenda kwenye uchumi wa viwanda kuititia *value adding*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu ya muda kutotosha nimalizie na suala la *blueprint*.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri mpya wa Viwanda na Biashara anayechangia kwamba hivyo viwanda vilivyobinafsishwa anavyozungumzia kwamba baada ya Bunge atarudi kuanza navyo ili avirudishe kazini, nataka nimpe taarifa kwamba vingi hata ile mitambo hakuna ilishang'olewa. Kwa hiyo anaona kiwanda ni kama *godown* tu lakini ndani mitambo hakuna tena, kwa hiyo kama kilikuwa kiwanda cha *textile* ndani ya hicho kiwanda hatakuta mitambo kwenye maeneo mengi sana. Naomba alijue hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa ya ndugu yangu Mheshimiwa Sugu siipokei kwa sababu sisi viwanda vilivyobinafsishwa hata *infrastructure* bado ni *value* na tunataka tukae na wawekezaji wale ambao wako *serious* tukae nao tuingie *joint venture*, waingie kwenye mpango kazi wa kusaidia kuhakikisha tunachakata mazao ya wakulima kwa ajili ya soko la ndani. Tanzania ni *member* wa East Africa tunalipa *fees* kila mwaka kushiriki katika hiyo *membership*, ni *member* wa *SADC*, hayo yote ni masoko ambayo tungependa nchi yetu iwe ni *production hub* kwa ajili ya hayo masoko pamoja na maeneo mengine ya dunia. Kwa hiyo, katika hili niwape tu *confidence* kwamba Serikali tukihakikisha vile viwanda vilivyobinafsishwa vinafanya kazi wakulima wetu hawawezi kupata shida katika masoko ya mazao yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka kumalizia na suala la *blueprint*, Serikali tumeanza katika bajeti hii kodi kero 54 zimeondolewa na tayari tuna *action plan*. Kwa hiyo ni kukuomba wewe pamoja na Wabunge tushirikiane katika

kuhakikisha tunaondoa *unnecessary red tapes* ambazo zimekuwa zikiwakumba wafanyabiashara nchini. Serikali katika hili nia yetu na tumejipanga vizuri katika kuhakikisha tunafanikisha katika hilo. Kikubwa ni *change of mindset* yaani Watanzania tuichukulie biashara kama ni fursa ya kutengeneza ajira kwa vijana na akina mama nchini lakini *Private Sector Development* ndio injini ya kusaidia uchumi wetu ukue katika namna ambayo ni *sustainable*.

Kwa hiyo Watanzania ile *mindset* ya ku-frustrate biashara tutoke huko tu-*facilitate* kila mmoja katika nafasi yetu ili *private sector* iweze kukua na kutengeneza ajira kwa vijana na akinamama. Tutafanikiwa katika hili kama tutashirikiana kuhakikisha *blueprint* na *action plan* yake wote tunashirikiana kwa pamoja kuhakikisha inatekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu tutahakikisha sera za viwanda ambazo ni za mwaka 2003 nilizokuta, tunafumua zote na ku-*update* kwa sababu ukitegemea kwenda kwenye uchumi wa viwanda kwa kuwa na injini ya *Vits* inayovutu *Semi-trailer* hatuwezi kufika. Kwa hiyo pa kuanzia ni kuhakikisha sera hizi za zamani za 2003 tunazi-*overhaul* ili ziweze ku-*reflect priority* ya nchi ya kwenda kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makof*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na sisi tunakupongeza pia kwa heshima kubwa uliyopewa na Mheshimiwa Rais na Taifa. Tunajua mzigo uliobeba ni mkubwa sisi kama Bunge tutakupa kila aina ya ushirikiano.

Kwenye *blueprint* kazi nzuri imefanyika na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nzuri sana na naamini inaendelea kufanyika. Ambacho ningependa kushauri, kulikuwa na mikwamo upande wa kisheria, kulikuwa na mikwamo upande ambao ni *administrative*, vitu vimewekwa tu kiutawala lete hiki, lete

hiki. Mtu anajaza fomu utafikiri anaandika mtihani wa Chuo Kikuu, halafu yanajirudia ukienda *TBS* yale yale, ukienda huku yale yale, ukienda *EWURA* yale yale, ukienda *NEMC* yale yale, lete hiki, lete kile. Sasa haya ya *administrative* na yenewe piga kalamu kama yameulizwa mahali fulani huku isirudie tena na kule na kule, vitu viwe vichache mtu anapeleka hasa anayeanza biashara aanze biashara. Hasa yale ya *administrative* ndiyo na yenewe yanapaswa kufanyiwa kazi sana *administrative* na ndiyo yanaudhi kuliko hata hayo ya kisheria. (*Makof!*)

Nashukuru sana. Mheshimiwa Mpina Waziri wa Mifugo, dakika saba.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi ili nami niweze kuchangia hii hoja iliyoko mbele yetu kwa kujadili hali ya uchumi pamoja na mpango wa maendeleo. Nianze kwa kupongeza sana Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na timu nzima kwa kazi nzuri walioifanya ya kutayarisha hii bajeti ya nchi na kuflikia hii hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa muda huu mfupi nianze moja kwa moja kuchangia baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge walismama hapa. Wengine walijaribu kuzungumza suala la kwamba tozo nyingi sana kuhusu uvuvi na imeonekana tozo za mifugo peke yake ndizo ambazo zimeweza kushughulikiwa na Serikali lakini tozo za uvuvi hazijaweza kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hivi kwa kifupi kwamba, moja tuliamua baada ya kuona changamoto za wavuvi tukaamua kufanya marekebisho ya Sheria ya Kanuni ya Uvuvu ya mwaka 2009 kwa Tangazo la Serikali 383, tukaweza kuondoa kigezo kilichokuwa kinalazimisha Ukanda wa Pwani kuvua dagaa kwa kutumia milimita 10 na badala yake ikiwa ni milimita nane, jambo ambalo lilikuwa ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wa maeneo ya Pwani. Hili lilitanyika na tayari kila kitu kiko sawasawa, sasa wanavua kwa milimita nane. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye hili eneo hili la kwa nini tozo, ukweli ni kwamba hotuba ya Waziri wa Fedha isingeweza kuchukua mambo yote tuliyyashughulikia mwaka huu kuyaonesha kwenye taarifa. Nataka niseme kwamba ni kweli kabisa kwamba dagaa walikuwa wanatozwa dola 1.5. Sasa nataka niwaambie hivi, tumerekebisha, Serikali imekubali kilio cha wavuvi na imekubali pia ushauri wa Wabunge, tumeponguzza kutoka 0.5 mpaka 0.3 dola za Kimarekani, lakini Ukanda wa Ziwa Nyasa vilevile tumeponguzza kutoka 0.5 dola za Kimarekani mpaka 0.3 dola za Kimarekani na Ziwa Tanganyika tumeponguzza kutoka dola 1.5 mpaka dola moja.

Mheshimiwa Spika, sababu nyiningine ni kwamba kwa nini hizi tozo zinatozwa tofauti tofauti kila eneo; tunatoza tofauti kila eneo kwa sababu Waheshimiwa Wabunge tozo hizi zinapangwa kulingana na thamani ya zao hilo la uvuvi linalozungumziwa. Kwa hiyo dagaa wa Ziwa Tanganyika huwezi kuwalinganisha na dagaa wa Ziwa Victoria, huwezi kuwalinganisha na dagaa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala hili la mauzo ya nje; kwamba mauzo ya nje yanaporomoka sana katika sekta hii ya uvuvi kwamba tunauza kidogo. Nataka niseme kwamba ni kweli takwimu zinaonesha na hali ya uchumi katika ukurasa wa kama sikosei wa 72 imeonesha kwamba mauzo yetu ya nje mwaka 2018 yalikuwa dola za Kimarekani milioni 158, lakini mwaka 2017 ilikuwa milioni 193 dola za Kimarekani. Miaka mingine yote kule inacheza kwenye milioni 160, milioni 195, lakini nataka niwaambie Wabunge tumeefanya kazi kubwa mambo haya yalisababishwa na vitu vingi. Moja, uvuvi haramu wa kutumia mabomu, wa kutumia nyavyu harama ambao tumeushughulikia kwa kiwango kikubwa lakini pia na mambo mengine.

Niwaambie mpaka sasa hivi tunavyozungumza mwaka huu wa fedha 2019, mauzo yetu ya nje mpaka leo hii tunavyozungumza yamefikia milioni 284.7, sawa na bilioni 654, hajjawahi kutokea katika awamu nyiningine yoyote ile katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala hapa Wabunge wamesisitiza sana la uvuvi wa bahari kuu kwamba tuwekeze kwenye bahari kuu. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Serikali ya Awamu ya Tano imefanya. Moja, mpaka sasa hivi tunavyozungumza *consultant* wetu anayefanya *feasibility study* anakabidhi ripoti tarehe 30 Juni, 2019 ya kukamilisha kuanza ujenzi wa bandari yetu ya uvuvi na baada ya tarehe 30 Juni tutaendelea na hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi mazungumzo kat i ya Tanzania ya nchi ya Korea kuhusu kujenga hii bandari ya uvuvi yako kwenye hatua nzuri. Kwa hiyo, tunategemea baada tu ya kupata hiyo taarifa ya *consultant* tutaingia sasa kwenye hatua za ujenzi wa bandari hii ya uvuvi ambayo nayo kwa miaka mingi haikuweza kufanikiwa lakini Serikali hii ya Awamu ya Tano imeweza na hatimaye tunaenda kuwa na bandari yetu ya uvuvi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia Wabunge wameshauri Serikali ikubali kununua meli na kuvua majini. Nataka niwape taarifa nzuri kwamba mpaka sasa hivi tumejipanga vizuri kwamba maandalizi mazuri sana yanafanyika ya kununua meli zetu na kuingia kuvua katika ukanda wetu wa bahari kuu. Mwaka huu wa fedha matarajio yetu makubwa tutakuwa tumenunua meli na tumeingia majini. Taasisi zetu zote mbili, *TAFICO* na *ZAFICO* kwenye maandalizi mazuri ya kuingia uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata Wabunge walipochangia wanasema Serikali hii inaenda kutoza *wigna kadhalika*, Waziri wa Fedha amesema bayana kwa mara ya kwanza tunaenda kuingia kwenye uvuvi wa bahari kuu na mipango yote ile imekaa vizuri na tumejipanga vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la 0.4 zinazotozwa watu wanapovua katika ukanda wetu wa bahari kuu limelalamikiwa na Wabunge, imeonekana ni changamoto. Kesho tunakutana mimi na Waziri mwenzangu wa Zanzibar anayeshughulikia mambo ya uvuvi tuweze kuliamua jambo

hili. Kwa hiyo, maamuzi yatakayotoka katika kikao kile yatakuwa ndiyo maamuzi ya Serikali juu ya jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la ngozi limezungumza na Wabunge, kwanza wakiomba asilimia 10 ya *export levy* kwa ngozi ya *wet blue* nje ya nchi iondolewe au ipunguzwe. Pia wakaomba asilimia 80 inayotozwa malighafi yetu kuiiza nje ya nchi na yenyewe iondolewe au ipunguzwe.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kifupi kwamba...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, malizia.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kwamba jambo hili Serikali imeshindwa kulifikisha mwisho katika kipindi hiki kwa sababu changamoto za sekta hii ya uvuvi ni nyingi.

Kwa hiyo, nachotaka kuliahidi Bunge lako Tukufu ni kwamba watuachie Serikali tushughulikie hizi changamoto za ngozi hapa nchini kwa kuangalia *parameters* zote ambazo zinakwamisha biashara hii ambapo tumeshakubaliana Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Fedha na mimi mwenyewe kuhakikisha kwamba hili jambo linafika mwisho sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvu, Mheshimiwa Luhaga Mpina. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa January Makamba, Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, una dakika 10.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha na Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kukupongeza kwa uongozi wako mahiri wa Bunge letu kama ulivyojidhihirisha pia hivi karibuni ulipotuongoza kwenda Misri pamoja na mambo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha pamoja na timu nzima ya Wakurugenzi, Kamishna wa Bajeti na wengineo kwa kuandaa bajeti hii ya Serikali ambayo imesomwa vizuri na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, yamezungumziwa masuala mbalimbali ya Muungano katika michango hii na mimi nitapenda kujikita katika mambo kadhaa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika kujibu hoja atajibu mahsus kuhusu miradi iliyotajwa na iliyochangiwa na Wabunge ambayo walipenda kupata maelezo, mradi wa Bandari ya Mpigaduri, jengo la uwanja wa ndege, barabara ya Chake na miradi mingineyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha anayo maelezo mazuri na atayatoa. Mimi niongee kwa ujumla tu kuhusu masuala ya Muungano na hasa namna tulivyozungumzia Muungano humu ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, wewe unafahamu kwamba Tanzania na sisi sote tuliomo ni nyumba na ni nyumba ya urithi kwa kweli kwetu sisi sote kwa sababu imejengwa na watu wengine na sisi tumeirithi, tunaishi katika Tanzania iliyojengwa na watu wengine na viongozi wetu walioijenga wametangulia mbele ya haki. Namna tulivyozungumzia Muungano katika michango hii kwa baadhi ya Wabunge maneno yanajenga lakini maneno pia yanabomoa. Baadhi ya maneno yaliyotumika, baadhi ya lugha zilizotumika hazichangii kujenga nyumba yetu hii tuliyorithi kwa viongozi wetu waliotangulia mbele za haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya maneno humu yametuhumu, yametusi na kwa kweli yameleta fadhaa kubwa. Mimi naomba kwa heshima ya Bunge lako, nchi yetu na kwa dhana nzima ya kuimarisha umoja, mshikamano na upendo mionganoni mwetu, baadhi ya maneno kwa kweli ifike

mahali yasiruhusiwe kutumika ndani ya Bunge lako Tukufu hasa maneno ambayo yanachangia kuweka ufa katika Muungano wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilipata bahati ya kwenda kuhudhuria bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati inasomwa siku ya Alhamisi wiki iliyopita na niliisikia bajeti imesomwa na Waziri Balozi Ramia. Baadhi ya mchango humu ndani katika bajeti yetu hii kuu ya Serikali ya Muungano imenkuu kwamba bajeti iliyosomwa Zanzibar ilirejea na kuzungumza na kwamba Waziri Mpango na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina roho mbaya, haina nia njema kwa Zanzibar ina hasada, wivu, chuki na kwamba Waziri Mpango na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamegoma kufanya masuala ambayo yataleta maendeleo kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwepo kwenye bajeti ile, hayo maneno yaliyonukuliwa kwamba yamezungumzwa na Waziri wa Fedha wa Zanzibar hayakunukuliwa hivyo, siyo sahihi. Bajeti ile ilisomwa kwa staha, kwa ustaarabu na ilieleza mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mimi napenda nimpongeze Waziri wa Fedha wa Zanzibar pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuandaa na kusoma bajeti nzuri na ya kujasiri ambayo ina nia ya kuleta maendeleo ya Zanzibar. Kwa hiyo, tuisiwatие maneno midomoni viongozi wa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kusukuma ajenda zetu za kuleta mgawanyiko katika Muungano wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi kama nchi tumeweka utaratibu wa kushughulikia masuala ya Muungano, yanapojitokeza tunayazungumza na tunayafanyia kazi. Napenda niseme kwa taarifa kwamba kuna ndugu yangu kutoka Pemba alizungumza jana nadhani Mheshimiwa Mohamed Amour na sisi tunaotoka Tanga watu wa Pemba tuko karibu nao, ni ndugu zetu kwa sababu unapanda mashua tu unavuka, unafika Pemba. Ndugu yangu alitumia lugha ngumu kidogo kumsema Waziri Mpango na kuwasema viongozi wa Serikali na kakisema Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ilichukua uvumilivu kwa baadhi yetu kutohamaki na ilikuwa inazungumzwa ni barabara kwamba kuna barabara ya kilometra 20, kilometra 40 imechelewa kujengwa kwa hiyo basi kwa sababu hiyo watu wote huku wana chuki, wivu, hasada. Kuna masuala mengi sana ya maendeleo ya Zanzibar, yanapojitokeza na mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unapohitajika kuna utaratibu mzuri uliowekwa ambao unatumika katika kuyawasilisha na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilipata bahati ya kuwa Msaidizi wa Rais Kikwete, mwaka 2005 – 2006 kulikuwa na changamoto ya umeme Pemba, kulikuwa na shida kubwa likaletwa kama suala kwamba Pemba kuna shida kubwa ya umeme katika utaratibu tulioweka hayakutumika matusi, kejeli wala kudhalilishana. Lilivyochukuliwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikatafuta msaada Norway dola milioni 88 ukawekwa waya chini ya bahari kutoka Tanga kwenda Pemba kupeleka umeme. Huo ni msaada ambao Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliutafuta. Umeme ukapatikana Pemba bila matusi, kejeli au kudhalilishana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya katika miaka ya hivi karibuni ule umeme umeleta changamoto. Mimi ni kiongozi ninayetoka Tanga, watu wenye viwanda Tanga walikuja kutulalamikia mbona Tanga mnasema tujenge viwanda lakini umeme hautoshi? Tukaenda kuwaliliza TANESCO jamani mbona umeme Tanga hautoshi? Wakasema, jamani eeh mtuwie radhi, tumewapelekea wenzetu Pemba *line* moja ya umeme kwa sababu kuna tatizo. Hilo limefanyika bila matusi, kejeli au kudhalilishana. Kwa hiyo, Serikali hizi zinafanya kazi pamoja vizuri, zinashirikiana, hakuna haja ya kuja hapa Bungeni na kusema watu wana chuki, hasada, wanafiki na kadhalika. Maneno hayo yanabomoa nyumba yetu hii ya Tanzania ambayo sisi tumeirithi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la Sheria ya Mikopo kwamba mabadiliko yameleta changamoto. Naomba niwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wiki iliyopita suala hilo imelileta rasmi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na limeingizwa katika utaratibu wetu wa kawaida wa kushughulikia masuala ya Muungano. Hapa Bungeni siyo kwamba ndiyo linaletwa kwa mara ya kwanza na Wabunge, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenyewe imelileta na tayari Serikali zote mbili zinalifanya kazi na litatolewa taarifa kuhusu namna linavyoshughulikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais na Rais Shein kwa kazi kubwa waliyofanya katika kipindi hiki cha miaka mitatu kuimarisha Muungano wetu. Mimi nakuomba na nakusihi sana Mzee wangu unayenipenda, naomba utusaidie Bunge lako lisiwe chanzo cha kuweka ufa katika Muungano wetu wacha watu wengine huko barabarani wafanye lakini siyo Wabunge, tena wakiwa ndani katika nyumba hii Tukufu na kula kiapo cha kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utakumbuka mwaka 1992 ndani ya Bunge lilijitokeza kundi la Wabunge 55 amba walitaka kuchukua hatua ambayo ingesababisha kuvunjika kwa Muungano wetu (G55), wakasema kuwepo na Serikali ya Tanganyika jambo ambalo kwa hakika lingesababisha kuvunjika kwa Muungano. Mwalimu Nyerere muasisi wa Muungano na baba wa Taifa letu aliingilia na akakaa na Wabunge pamoja na Wajumbe wa NEC, sisi tunafundishwa kwamba ni mara chache Mwalimu Nyerere ametoa chozi hadharani ni pale alipopokea mwili wa Sokoine, alipokuwa anamuelezea Mheshimiwa Kawawa na alipokuwa anataka Muungano huu udumu kwa kuwazua wale watu 55 wasichukue hatua waliyokuwa wanataka kuichukua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tusingependa kauli hizi zinazotoka humu zikataka kuleta hisia kama zile za mwaka 1992. Tunaomba utuongozee, ninyi ndiyo wazee mliobaki, mwalimu hayupo. Baadhi ya kauli zinazotoka humu zitafanya miili ya

waasisi wetu ndani ya makaburi yao ianze kuzunguka kutokana na maneno yanayotoka ya kutaka kuivunja nchi yetu. Tunaomba sana utuongoze, uhodari wa kuwasema wengine ili kupata mtaji wa kisiasa, uhodari wa kuunajisi Muungano kwa maneno machafu ili kupata umaarufu wa kisiasa usikubalike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni jambo ambalo linakubalika kabisa kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina bajeti yake, ina Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na kuna llani ya Chama cha Mapinduzi kwa upande wa Zanzibar. Tunafahamu kabisa kwamba vyote hivyo vinahitaji rasilimali ili kutekelezwa na tunafahamu kabisa kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayo nafasi katika kuhakikisha kwamba Zanzibar inapata uhakika wa rasilimali hizo. Hilo linafahamika na viongozi wetu wanalifahamu na wanalifanyila kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimalize kwa kusema kwamba tumechagua viongozi mahiri kwa pande zote; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar, tuwaamini kwamba dhamira yao ni kufanya yote yanayopaswa kufanyika kuimarisha Muungano wetu. Tusishindane kwenye uhodari wa kuusema Muungano kama namna ya kuulinda. Tuwachie viongozi wetu na sisi kwa kauli zetu na kwa matendo yetu tuwasaidie katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inabaki moja ili kizazi hiki kiirithishe nchi yetu kwa kizazi kijacho bado ikiwa inaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Naomba nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa uliyoyasema. Niungane nawe moja kwa moja, wengine hatukupata bahati ya kusikia hasa ni nini kilisemwa lakini tutafuatilia kwa ukaribu lakini nikubaliane nawe asilimia 100, hatutaruhusu Bunge letu kuwa ni sehemu ya kuanzisha cheche zinazoweza kuwashaa moto unaoweza kuunguza nchi yetu Tanzania ikaishia kuwa

vipande vipande, hatuwezi kuruhusu hilo. Kwa hiyo, tutaongeza umakini katika kufuatilia na kusikiliza ili tuhakikishé mambo kama haya hayajitokezi tena katika siku zijazo.

Usia uliotupatia tunauchukua na tutauzingatia kabisa kabisa kwa sababu umoja wa nchi ndiyo jambo la kwanza tulilonalo na sisi hapa ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bila hiyo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hata Bunge lenyewe hili haliwezi kuwepo, kama likiwepo ni la aina nyingine siyo hili. Kwa hiyo, kazi yetu ya kwanza ni kulinda kile tulichonacho kwanza sisi wenyewe Wabunge maana tunatokana na Muungano wenyewe. Nakushukuru sana kwa kutukumbusha na tutazingatia ushauri wako. (*Makof*)

Sasa nimuite Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, karibu mbele, karibu sana. Jitahidi utumie hizi dakika 20 zillizopo. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema aliyetufikisha katika hatua hii asubuhi hii ya leo ikiwa ni kuhitimisha hotuba ya bajeti ya nne ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru sana wazazi wangu wawili kwa kuendelea kuniweka kwenye maombi mtoto wao ili niweze kuwatumikia Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuendelea kuniamini kwa mwaka wa nne huu nikiwa ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango, hakika imani hii ni kubwa kwangu na naomba kumhakikishia kwamba sitamuangusha yeye wala Wanakondoa walioniamini kunileta katika Bunge hili tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nikushukuru sana wewe kama kiongozi wa Bunge hili Tukufu kwa jinsi unavyoliendesha Bunge hili kwa viwango na kwa jinsi ambavyo upo imara kusimamia maendeleo ya Taifa letu. Nikushukuru sana ukiwa kama kaka yangu kutoka Mkoa wa Dodoma kwa miongozo na malezi yako kwangu hakika unaendelea kunijenga. Nakushukuru sana na nakuombea kwa Mwenyezi Mungu baraka tele na afya njema. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia shukrani hizi nizielekeze kwa kiongozi wetu wa Serikali ndani ya Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa kwa miongozo na maelekezo yake anayoendelea kutupatia kama Wizara na kama Serikali. Nina hakika Watanzania wanaiona kazi nzuri unayoifanya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mwenyezi Mungu aendelee kukujalia busara na afya njema ili uendelee kuwatumikia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Philip Mpango, kwangu mimi kufanya kazi na huyu Mheshimiwa Waziri ni fursa kubwa sana, najifunza mengi, mazuri kutoka kwake. Hakika naendelea kuwa mwanafunzi mzuri kwake na nam wahidi kuendelea kuwa msaidizi wakw wa karibu ili aweze kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru sana familia yangu, mume wangu Dkt. Muhamadri Kachwamba na rafiki yangu wa karibu kwa miaka 20 sasa. Hakika nafasi aliyonipa ni kubwa sana kwenye maisha yake na mchango wake kwenye mafanikio yangu ni mkubwa sana. Namshukuru sana kwa kuendelea kuniamini, kuendelea kunisaidia niweze kutenda majukumu yangu. Kwa watoto wangu pia nawashukuru sana, najua wamekuja likizo, lakini mama anarudi saa tano, saa sita usiku wanaendelea kunivumilia, nasema waendelee kunivumilia kwa sababu niliiomba nafasi ya kuwatumikia Watanzania na nimeipata nafasi hii waendelee kunivumilia, nitarejea kukaa nao pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za mwisho lakini si kwa umuhimu, ni kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kondoa, hakika waliniamini mwaka 2015, wakiwa wananjua kidogo sana, lakini sasa wamenijua kwa utendaji wa kazi katika Jimbo la Kondoa, lakini kwa kuwatumikia Watanzania. Naomba niwaambie Watanzania, Wanakondoa kwamba, sitawaangusha, nitaendelea kulisimamia Jimbo la Kondoa, liko imara na nawahakikishia Chama cha Mapinduzi mwaka 2019 Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa tutashinda kwa asilimia 100 na mwaka 2020, mimi Mbunge wao nitarejea ndani ya Bunge hili kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kuchangia hotuba hii iliyowekwa mezani na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na naomba nianze kwa kulisemea jambo la biashara, hali ya biashara ndani ya Taifa letu, ambalo yalisemwa maneno makali sana dhidi ya Waziri wa Fedha na Mipango, dhidi yangu mimi msaidizi wake kwamba sisi tunashangilia ufungwaji wa biashara ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tukaambiwa, Kariakoo imekufa kwa sababu ya Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu wake kwa sababu tumeshindwa kusimamia. Pia ikasemwa kwamba, kwa nini tumechelewa kufanya maamuzi ya kuzuia ufungaji wa biashara, hadi mwaka wa nne ndiyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango anakuja kuzuia ufungaji wa biashara.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kuanzia hotuba ya bajeti ya mwaka wa kwanza, Mheshimiwa wa Fedha aliyewasilisha ndani ya Bunge lako tukufu, mwaka 2016/2017, aliwaelekeza watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ni marufuku kufunga biashara ya mfanyabiashara ye yote yule bila kufuata utaratibu na sheria zinazowaelekeza hivyo.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo yalisemwa ndani ya Bunge lako Tukufu, kwa hiyo kuja leo kumlaumu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, siyo sahihi hata kidogo na amechukua jithada za kutosha Mheshimiwa Waziri wa Fedha

kuhakikisha biashara hazifungwi kwa sababu tu ni watumishi wa Mamlaka ya Mapato wanataka kufunga, hapana, zipo sheria zinazowaelekeza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme jambo la pili, katika soko huria, moja ya sifa za uchumi wa soko huria ni uhuru wa kuanzisha biashara na uhuru wa kufunga biashara, yaani tunasema kuna *free entry and exit from the market*. Kwa hiyo, tukiangalia sana wengi waliofunga biashara siyo kwa sababu wamelazimishwa kufunga biashara na watumishi wetu wala na viongozi wa Serikali yetu wala na Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, kwenye uchumi wa soko huria ambao Taifa letu lipo, ifahamike kwamba biashara pia zinaweza kufungwa kwa sababu mbalimbali. Sababu ya kwanza, yaweza kuwa ni kubadilisha alna ya biashara, mfanyakibashara ambayo amekuwa akiifanya, lakini pia yaweza kuwa kwa sababu ya ushindani mkali katika biashara husika, hiyo inaweza kupelekea pia mfanyakibashara akabadilisha biashara yake. Vile vile yawezekana, ni kushindwa kuisimamia biashara yake husika, lakini yawezekana pia biashara ambayo wamekuwa wakiifanya, walikuwa kwenye *shareholding* na wameshindwa kuelewana, wanaamua kui-dissolve biashara yao ili waweze kufanya biashara nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika sababu hizi, hajiaachwa nje pia hata sababu ya kwamba mfanyakibashara huyu ana mzigo mkubwa wa madeni, aidha kwenye benki za biashara au kwenye taasisi zozote za kibenki, lakini pia hata yawezekana ana madeni ya kikodi na kama tunavyofahamu, kodi hukusanywa kwa kufuata sheria.

Mheshimiwa Spika, hizi zaweza kuwa ni sababu zilizopelekea baadhi ya biashara kufungwa. Nipende kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, zipo tafiti ambazo zimefanya duniani na zote zikabainisha kwamba, zaidi ya asilimia 50 ya biashara za ukubwa wa kati na ukubwa mdogo, hufa kabla ya kusherekeea *birthday* yao ya mwaka wa tano. Kwa hiyo,

yawezekana hii pia ikawa ni hali ile ya kawaida ya biashara hizi za saizi ya kati na saizi ya ukubwa mdogo ambazo zinaweza kuwa zinakufa ni kwa sababu ya sababu hizi nilizotaja na hii si kwa Tanzania tu, hii ni kwa dunia nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, kwamba, nilituhumiwa pia kwamba nimekuwa nikijisifu kwa kuzifunga biashara hizi ndani ya Taifa letu. Naomba nikiri ndani ya Bunge lako Tukufu, kitu ambacho nimekuwa nikikisimamia kama Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ni kuhakikisha sheria zinafuatwa ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nikitoa mfano, wakati nachangia hotuba ya Viwanda na Biashara, liliongelewa sana tatizo la kufungwa kwa biashara na zikatolewa takwimu ambazo siyo sahihi ndani ya Bunge lako Tukufu. Ilinillazimu kueleza ukweli, kuwaeleza Watanzania, nini uhalisia ndani ya Taifa lao ili waweze kufahamu.

Mheshimiwa Spika, ukiniruhusu naombakunukuu nilichokisema. Siku ya tarehe 15 mwezi wa tano mwaka 2019 nilisema maneno yafuatayo:-

*"Kwamba ni kweli zipo biashara zinazofungwa na zipo biashara zinazofunguliwa. Nikasema, kwa Tanzania kwa mwaka huu mmoja biashara zilizofungwa ni 16,252 na biashara zilizofunguliwa ni 147, 817."*

Mheshimiwa Spika, nililazimika kutoa takwimu hii kwa sababu ilihojiwa ndani ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Hata hivyo, siyo sahihi, tukiangalia takwimu hizi siyo sahihi kusema ndani ya Taifa letu biashara nyingi zinafungwa kuliko zinazofunguliwa. Kisayansi kinachotakiwa kufanyika, baada ya kujiridhisha na biashara zinazofungwa na kufunguliwa, ni kwenda kufanya utafiti sasa wa kisayansi, tuweze kujiridhisha biashara zinazofunguliwa ni za ukubwa gani, ni katika sekta zipo na sababu zipo zinazopelekea kufungwa kwa biashara hizi. Wizara ya Fedha na Mipango kuititia Kitengo chake cha Utafiti na Sera kinaendelea

kufanya utafiti huu ili tuweze kujiridhisha, nini kinasababisha biashara hizi kufungwa na ni zippi zinazofunguliwa na sababu zinazosababisha zifunguliwe ili tuweze kama Serikali kuzilea biashara hizi.

Mheshimiwa Spika, pia nilisema kwenye Bunge lako Tukufu siku hiyohiyo kwamba, ni muhimu tukajiuliza maswali, kama kweli yanayosemwa, tunayotaka kuamisha Watanzania, kwamba biashara nyingi zinafungwa kuliko zinazofunguliwa, nilihoji maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nilisema na leo naomba nirudie kuyahoji maswali haya; swalii la kwanza nikasema; kama ni kweli biashara nyingi zinafungwa, je Serikali ingeweza wapi kuongeza ukusanyaji wa mapato tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani, kwa mwezi kwa zaidi ya asilimia 75, kama biashara kweli zinafungwa? Tumetoka shilingi bilioni 870 kwa mwezi na sasa tunakusanya triliuni 1.3, kama biashara zinazofungwa ni nyingi zaidi kuliko zinazofunguliwa wapi tungeyapata mapato haya.

Mheshimiwa Spika, lakini swalii la pili la kujiuliza, kama kweli biashara nyingi ambazo ni chanzo kikubwa cha mapato ya Serikali yetu, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tano, isingiweza kulipa mishahara ya watumishi wetu ndani ya tarehe 20 kila mwezi zaidi ya bilioni 580 kila mwezi, kama kweli chanzo hiki cha mapatao kimefungwa, wapi tunazipata fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, vile vile nikasema, ni vizuri tukajiuliza, zaidi ya asilimia 85 ya bajeti iliyokwenda kwenye miradi ya maendeleo kwa mwaka huu wa fedha, ni fedha zetu wenywewe za ndani. Kama biashara zinafungwa, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli inatoa wapi fedha hizi kwenda kugharamia zaidi ya asilimia 85 ya miradi ya maendeleo inayotekelzwa!

Mheshimiwa Spika, ni vizuri pia tukafahamu kwamba Wiraza ya Fedha na Mipango, hatuwezi kukaa kimya tunapoona watumishi wetu wanaendelea kuvunja sheria na

hatuwezi kukataa, wapo baadhi ya watumishi wetu, ambao siyo waaminifu wakishirikiana pamoja na wafanyabiashara ambao siyo waaminifu kulinyima Taifa letu mapato. Hili hatuwezi kulivumilia, tunapogundua mfanyabiashara anakwepa kodi kwa makusudi, hatuwezi kulivumilia, kwa sababu tumeaminiwa ili kuhakikisha Taifa hili linapata mapato yake, lazima tusimame imara.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja wa jinsi tunavyoshughulikia, kwa mfano, katika ya mwezi Mei, 2017 hadi mwezi Aprili, 2019, zaidi ya watumishi 30 wa Mamlaka ya Mapato Tanzania walismamishwa kazi kutokana na utovu wa nidhamu katika kazi zao za kila siku, hili hatuwezi kulivumilia, tutasimamia kwa watumishi wa Mamlaka ya Mapato, tutasimamia kwa wafanyabiashara ambao siyo waaminifu kuhakikisha kwamba biashara zinaendelea kufanya, biashara halali kwa ajili ya mapato halali ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitoe mifano miwili ili tuweze kuelewa na Watanzania waelewe Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi nini inataka. Tarehe 19 Aprili, nilipokea wageni ofisini kwangu, walikuwa ni vijana watatu wakiwa wametoka Mkoa wa Kagera na kutoka Mkoa wa Mwanza, wamekuja ofisini kwangu wakija kulalamika, wanakuja kulalamika kwamba wamepewa *assessment* kubwa ya kodi.

Mheshimiwa Spika, nilianza kuifuatilia ile kesi, nilipoifuatilia ile kesi yaliyojiri, ndiyo maana nasema, tunao baadhi ya watumishi wetu ambao siyo waaminifu na baadhi ya wafanyabiashara ambao siyo waaminifu. Kilichojiri, zilikuwa ni malori manne ya tani 10 yaliyobeba vitenge vilivyotoka China, maroli haya manne yalikuwa yametoka wapi, maroli manne haya yalikuwa yamepita Bandari ya Dar es Salaam yakiwa ni *transit*, ni mizigo inayokwenda nchi jirani. Malori yale yanaonekana yamepita mpaka katika mpaka wetu wa Mtukula, yalipopita Mtukula hayakwenda Uganda yakageuza kurudi Tanzania tena. Yalipofika mpakani tukawa tumepata taarifa hizi, yakasimamishwa, kuangalia hawana

*document* hata moja inayoonyesha malori hayo yamekwenda Uganda na kwa nini yanarudi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuja kufuatilia, tayari kuna mfumo, kati ya watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoka Bandari ya Dar es Salaam, Makao Makuu na mipaka yote mpaka yalipoingia Uganda. Walipokuja wale vijana, hawakuwa wenye mizigo, wale vijana waliokuja walikuwa ni madalali ambao wanakusanya kodi halali kutoka wa wafanyabiashara, lakini wao madalali wanalipa kiwango kidogo sana cha fedha waki-*collude*na watumishi wetu. Kwa jambo kama hili, hakika tumeaminiwa, lazima tulismamie, lazima walipe kodi na lazima mfanyabiashara wa aina hii kulingana na sheria, zile lori zote nne zilitaifishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili lazima tulismamie, kwa sababu tunahitaji mapato illi tuweze kuwashudumia Watanzania, kwenye afya zao, Watanzania kwenye shule zao na Watanzania kwenye, watoto wetu kulipiwa ada na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, kama hilo ndilo linalotafsiriwa, Ashatu anakuja kushangilia kufungwa kwa biashara, hilo naomba nimwambie Rais wangu, nitaendelea kusimamia. Hilo naomba niwaambie Watanzania, sitoruhusu waibiwe, nikiwa Naibu Waziri wa Fedha, sitofanya hivyo. Lazima nitasimama imara na kodi zote zitakusanya kulingana na sheria tulizopitisha ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye hoja ya pili, hoja ya pili ambayo ningependa kuisema mbele ya Bunge lako tukufu, nikiwa nachangia hotuba hii ya Bajeti Kuu ya Serikali, ni kuhusu kufutwa kwa kodi ya ongezeko la thamani kwenye tauzo za kike.

Mheshimiwa Spika, hata nisipo-*declare interest* mimi ni mwanamke, mimi ni mwanamke na mimi nina mchango wangu kwenye kila kinacholetwa na Waziri wa Fedha ndani ya Bunge lako Tukufu. Yameongeleta maneno magumu sana, ambapo, nikamwambia Mheshimiwa Waziri wa Fedha

jambo hili naomba nilibebi mwenyewe. Naomba niwaeleze Watanzania, mimi nikiwa kama mwanamke, naijua adha hii na halipendezi hata kidogo Waheshimiwa Wabunge, naomba tu niseme, haipendezi hata kidogo kwa maneno aliyoiezwa Waziri wa Fedha ndani ya Bunge hili Tukufu na lazima tufahamu Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Fedha anapoleta hoja hapa ndani ya Bunge hili, inakuwa ni hoja ya Serikali, siyo hoja ya Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapotoa tuhuma hizi, hasa zile ambazo ni *personal attack*, naomba tufahamu ana moyo, hakuondolewa nyongo Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anaumia kama mwanadamu, lazima tujitafakari, lazma tuvae viatu vyake, lazima tujilize ningekuwa ni mimi nikaelezwa maneno haya ningejisikiaje. Inakera na inaumiza, lakin naomba niwaambie Watanzania, dhamira ya Serikali yao ni njema sana. Kama ambavyo nimekuwa nikisema siku zote kwenye Bunge hili Tukufu, kodi ina mchango mdogo sana kwenye bei ya mwisho ya bidhaa. Hili limejidhihirisha, Bunge lako Tukufu kwa dhamira njema, kama ambavyo Serikali yetu ililetu ndani ya Bunge lako Tukufu, tulipitisha kuondolewa kwa kodi hii ya ongezeko la thamani kwenye tauzo za kike.

Mheshimiwa Spika, yamesemwa maneno mengi sitaki kuyasikia, kwamba bajeti hii *is gender insensitive!* Nikasema nirudi pale ofisini kwangu nikaangalie, hivi ni kipi kinachosababisha bajeti ya Serikali, Serikali iliyoaminiwa na wananchi kuliongoza Taifa hili, kwamba iambiwe bajeti yake ni *insensitive*, hivi kweli, ni tauzo ya kike ya Sh.2,500 tu! Nikajuliza maswali mengi, nikarudi kuangalia *what is gender budgeting. Gender budgeting* haimaanishi *item* moja na *item* hii mchango wake ni upi katika uchumi wa mwanamke, katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nikarudi kikasema nianze na afya ya mwanamke, Serikali ya Awamu ya Tano imefanya nini, Serikali ya Awamu ya Tano imefanya makubwa kwenye afya ya mwanamke. Nikisema kwa mikoa michache, nikianza na

vituo vya afya, hospitali za wilaya tulizojenga katika mikoa yetu, tunakwenda kum-target mwanamke. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikiongelea Mkao wa Simiyu peke yake tumepeleka bilioni 4.5 kwa ajili ya kujenga hospitali kwenye halmashauri zake ili wanawake waweze kupata huduma bora za afya.

Mheshimiwa Spika, Mkao wa Geita tumepeleka bilioni tatu; hii ni kwa mwaka mmoja tunaangalia afya ya mwanamke.

Mheshimiwa Spika, tukiichukua Kanda ya Ziwa yote tumepeleka kwa mwaka mmoja bilioni 22.5 kwa ajili ya afya ya Watanzania ambapo mtu wa kwanza tunayemwangalia ni mwanamke wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wanajua; katika vitabu vya Wizara ya TAMISEMI vya bajeti tulionesha nini tumepeleka. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inamjali sana mwanamke, na sisi kwa pamoja tumekiri hapa mwanamke wa Tanzania akiwa kijiji, akiwa mjini ndiye anayelilisha taifa hili. Nikajiuliza sana, kwamba huyu Mwanamke anayelilisha taifa ndiye anashindwa kuwa na shilingi 3,000 kwa ajili ya kununua tauko ya kike kwa mwezi? Hili lazima tuliangalie katika uwanda mpana ili tuweze kuelewa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme, baada ya kuwa tumeondoa kodi hii ya ongezeko la thamani kwenye tauko hizi za kike nini kimetokea; Serikali yetu haikukaa kimya tukasema tulifuatilie jambo hili, kwamba je, kuna athari yoyote iliyokwenda kwa wanawake? Ikafanywa *study* katika Wizara ya Viwanda na Biashara, Mamlaka ya Mapato Tanzania na *Fair Competition Commission*. Nini kilijiri mpaka leo tuje tuseme kwamba bajeti hii haikumuangalia mwanamke kwa jicho la pekee? Kilichojiri ni kwamba tuligundua kwamba kuondolewa kwa kodi hii; kwanza wanawake wengi hawajui kama kodi hi imeondolewa. Hili lilikuwa jambo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwenye Bunge lako ikasemwa wapo kwamba watu walioalikwa mpaka mikutano ya kimataifa kwenda kupongezwa kwa ajili ya kuondolewa kwa kodi hii; unapongezwa kwa ajili ya jambo gani?

Mheshimiwa Spika, nilishaona watu wanapewa tuzo kwa ajili ya wanawake lakini unaulizwa umefanya nini kupewa tuzo hiyo? Unaitwa kwenda mataifa mbalimbali kwenda kupongezwa wakati ndani ya taifa lako hujasimama kuwaambia wanawake kwamba kodi hii imeondolewa kwa ajili yenu. Kwahiylo hili lazima tiliangalie kwa jicho pana ili tuweze kuelewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujuu wanawake wengi hawajui pia tukakuta jambo la pili. Kwamba athari iliyopatikana bei haijapungua kule ambako tulidhamiria bei ipungue. Bado taulo iliyouzwa shilingi 2,500 leo hili bado inauzwa shilingi 2,500, taulo iliyouzwa 5,000 bado leo hii inauzwa shilingi 5,000.

Mheshimiwa Spika, badaa ya kuondolewa kwa kodi hii nini kilitokea kwenye viwanda vyetu vya ndani? Kilichotokea kwa viwanda vyetu vya ndani ni viwanda vyetu vya ndani kupunguza uzalishaji wa bidhaa hii. tunapopunguza uzalishaji nini tunajifunza? Tukipunguza uzalishaji tunakwenda kuondoa ajira za vijana walioajiriwa kwenye viwanda hivi vya ndani. Hizi ni athari hasi baada ya kuondoa kodi hii ya ongezeko la thamani kwenye taulo za kike.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu haikuishia hapo; tukakaa chini tukatafakari nini cha kufanya? Tukasema jambo la la kwanza ni kuendelea kuodoa asilimia 10 ya *import duty* (ushuru wa forodha) kwenye mali ghafi zote zinazozaloisha taulo za kike. Hii iliondolewa tangu mwaka 2012, lakini ilisemwa kwenye Bunge hili kwamba haijaondolewa. Naomba niwaambie Watanzania tunawajali sana wanawake. Tuliondoa uhuru huu wa forodha wa asilimia 10 tangu mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili tukasema; ukiangalia bidhaa hii ya taulo za kike ni bidhaa ya muhimu ambayo *whether* bei imepanda au haijapanda lazima itatumika tu. Unapokuwa na bidhaa ya namna hii wachumi tunaiita ni *necessity goods*, haiwezi kutibiwa kwa ajili ya *measures* za kikodi peke yake. Unapokuwa na bidhaa ya aina hii lazima uwe na *measures* za kikodi Ipamoja na *measures* za kibajeti na *measures*nyingine za kiutawala ili uweze kuwasaidia hawa wanaotakiwa bidhaa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi inamjali mwanamke wa Tanzania, baada ya kuondoa asilimia 10 ya ushuru wa forodha tukasema tunaondoa asilimia tano ya kodi ya mapato ya viwanda vipyta vitakavyoanzishwa kwa ajili ya kutengeneza taulo hizi za kike.

Mheshimiwa Spika, hii tumeiondoa kwa muda wa mikaa miwili. Hata hivyo, Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge wakasema hii haitoshi na Serikali yenu ya Chama cha Mapinduzi inawasiliza, imekubali kwamba tunaondoa tena asilimia tano kwa ajili ya kodi ya mapato kwa viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hii kwa miaka miwili mfululizo. Kwahiyao mwanzo tulisema viwanda vingine hatuna uhakika kama vitakuwa lakini sasa tunaondoa kwa viwanda vya ndani ambavyo tayari vinazalisha, tunawapunguzia asilimia tano ili waweze kuionyesha kama ina athari hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimsema *measures*za kikodi pake yake haziwezi kujibu jambo hilli. Serikali yenu ya Chama cha Mapinduzi iliyoaminiwa na Watanzania tumekuja na suluhisho pia la aina nyingine, nayo ni kuanzishwa viwanda vinavyotumia *PPP* ambavyo vimefika kwenye hatua kubwa ambayo tunaamini ndani ya mwaka huu wa fedha viwanda hivyo vitakuwa vimekamilika.Ni kiwanda kinachojengwa katika Mkoa wa Simiyu ambacho kinajengwa na *NHIF* na kinajengwa na *Workers compensation* pale Bariadi-Simiyu ili kiweze kuzalisha taulo hizi za kike. Kitakapozaalisha taulo hizi za kike kwa sababu Serikali ina mkono wake, Serikali sasa

itakuwa na uwezo wa ku-control/bei za bidhaa inayozalishwa na kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, tukiweza ku-control/bei nini maana yake; hata wazalishaji wengine sasa wakiona viwanda vyetu hivi vimezalisha bidhaa za kutosha nao watashusha bei. Hiyo ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikiwa inawaangalia Watanzania wote kwa ujumla wake pamoja na kuangalia makundi mbalimbali ili yaweze kufanya majukumu yao ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, tukiacha kiwanda hiki cha Simiyu kuna kiwanda kingine kinajengwa Pwani. Kiwanda hiki kinajengwa Pwani na MSD ambao nao wako katika hatua ya mwisho na mkataba unasainiwa ndani ya siku hizi mbili. Ndani ya mwaka huu mmoja kiwanda hiki pia kitakuwa kimeanza kuzalisha bidhaa hii na hatimaye tutaiuza kwa bei ya chini na tutamfikia mwanamke kule alipo.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo ambayo tumesema tuyaseme kama Serikali kwa ajili ya bidhaa hii kwa kuwa sisi ni wasikivu tumesikia na tunakuja na suluhisho za aina tatu ili kiukweli tuweze kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme jambo moja la mwisho nalo ni kuhusu miradi ya *PPP*, kwanini Serikali haitaki kutekeleza;

Mheshimiwa Spika, Serikali inalishukuru Bunge lako tukufu...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa Waziri, dakika moja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, Serikali inalishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuwa iliruhusu kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya *PPP* na tukisoma kwenye mipango yetu ya maendeleo, Mpango wa

Maendeleo wa Miaka Mitano na pia Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja, Serikali iko tayari kushirikiana na wadau binafsi katika kuwekeza kwenye maeneo muhimu kwa ajili ya uchumi wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba niseme naunga mkono hoja na nashukuru kwa kunipa fursa hii.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Dkt. Ashatu Kijaji kwa kujitahidi kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge na kusaidia kupunguza masuala ambayo yalikuwa yameelekezwa kwenu pamoja na Mheheshimiwa Waziri wa Fedha.

Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mpango, mtoa hoja karibu sana ili uweze kuhitimisha hoja yako na pia kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge; ninakupa dakika 50.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba radhi sauti yangu ina shida kidogo lakini nitajitahidi ili Waheshimiwa Wabunge waweze kusikia majumuisho.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimshukuru Mungu kwa Baraka ya upendeleo kwa siku nyingine ya leo ambayo nimepewa kwa ajili ya kutumikia.

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Juni, 2019 niliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Mwaka 2018, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2019/2020 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2019/2020; na kwa muda wa siku saba za kazi tangu tarehe 17 hadi leo tarehe 25 Waheshimiwa Wabunge wamepata nafasi ya kuzipitia hotuba hizo pamoja na viambatisho vyake na kutoa maoni na ushauri juu ya namna bora ya kujenga uchumi unaogusa wananchi wengi na kufanikisha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi lakini pia Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuendesha mjadala huu vizuri na kwa kweli unatarajiwa kuhitimishwa leo hii kwa kura ya wazi ya kila Mbunge kama ulivyosema.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Wabunge 236 wamechangia hoja niliyowasilisha, na kati ya hao 189 wamechangia kwa kuzunguza, 41 kwa maandishi. Aidha, Waheshimiwa Mawaziri wanenye, Naibu Mawaziri wawili akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango wamechangia kwa kutoa ufanuzi kwa baadhi ya hoja zinazogusa sekta wanazosimamia, ninawashukuru sana. Vile vile nina washukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu, hakika mmetekeleza wajibu wenu wa Kibunge vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, na kipekee napenda kutambua na kupongeza uchambuzi na ushauri wa Kamati ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe.

Mheshimiwa Spika, lakini pia namshukuru Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mombasa kwa maoni na ushauri aliousoma kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala wa hituba nilizowasilisha, Waheshimiwa Wabunge wengi walimpongeza Mhehsimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi makini na kwa kusikiliza kero za makundi mbalimbali ya jamii na kuelekeza ufumbuzi wa kero hizo. Aidha, walipongeza na kuunga mkono bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha kwa maelezo kwamba bajeti ikaakisi matarajio ya Watanzania na inazingatia maslahi ya taifa na wadau wengi. Kwa niaba ya Serikali nimepokea kwa unyenyekevu shukurani na pongezi zote zilizotolewa kutoka ndani na nje ya Bunge juu ya bajeti hii. napenda niahidi kwamba baada ya bajeti

hii kuitishwa rasmi na Bunge, Serikali itafanya kila linalowezekana kuitekeleza kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, yako aadhi ya maeneo mapya ambayo yaliungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wengi nitasema machache tu:-

i. Kwanza ni hatua ya Serikali kufuta au kupunguza ada na tozo 54;

ii. Serikali kukutana na wafanya biashra na kuanza utekelezaji wa *blueprint*;

iii. Kuanza na kuendeleza ujenzi wa miradi mikubwa ya kimkakati

iv. Kutopandisha ushuru wa bidhaa kwa mazoea na hususani sigara na bia;

v. Kuielekeza *TRA* kubadilika ili kuwa na urafiki na walipa kodi na kupunguza utegemezi wa kibajeti na pia hatua za kikodi kulinda viwanda vyatia ndani.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wameishauri Serikali iyawekee msukumo wa kipekee katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha na bajeti zinazofuata. Naomba napo nitaje machache tu:-

i) Ni kuweka mkazo zaidi kwenye kilimo hususani utafiti, mbegu bora, huduma za ugani, pembejeo, kuongeza thamani, kutafuta masoko na kilimo cha umwagiliaji

ii) Kuwezesha upatikanaji wa taulo za kike kwa gharama nafuu

iii) Kukwamua upatikanaji wa mikopo ya kugharamia miradi muhimu ya maendeleo Zanzibar; na

iv) Uanzishwaji wa wa mfuko wa pamoja wa fedha za Muungano.

Mhehsimiwa Spika, haya tu ni baadhi lakini yako mengi sana; na kwa kuwa tutaleta majibu kwa maandishi ili kila Mheshimiwa Mbunge asome tutayaorodhesha yote ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuona mamambo makubwa ambayo tuliachukua.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuanza kutolewa ufanuzi hoja na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kama nilivyotangulia kusema mjadala wa siku saba ni vigumu kuutolea ufanuzi kwa dakika 50; kwahiyo tutaleta ufanuzi wa hoja zote na kila Mheshimiwa Mbunge atapata ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza, naomba nianze na hiiambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameieleza kwa kirefu, kwamba msamaha wa kodi wa ongezeko la thamani uliokuwa unatolewa kwenye taulo za kike zinazotambulika kwa *HS code 9619.00.10* kwamba urejeshwe na Serikali ichukua hatua za maksudi kuhakikisha wafanya biashara wa bidhaa hiyo wanashusha bei au wanawekewa bei elekezi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetafakari sana juu ya mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu hitaji hili muhimu kwa mtoto wa kike na wanawake kwa ujumla. Kwa kuzingatia maoni na ushauri uliotolewa, napendekeza mambo matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kama vile ambavyo nilileza kwenye Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali tarehe 13 Juni, 2019; kwamba ni kupunguza kiwango cha kodi ya mapato ya makampuni (*Corporate Income Tax*) kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 25 kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka ujao wa fedha hadi mwaka 2020/2021 kwa wawekezaji wapya wa viwanda vya kuzalisha taulo za kike. Lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji katika uzalishaji wa hii bidhaa muhimu sana pamoja na kuongeza ajira na mapato ya Serikali

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hatua ya uwekezaji inaweza kuchukua muda kiasi, na ni nia ya Serikali kuhakikisha kuwa hatua hii inaleta manufaa kwa haraka, Serikali pia imeamua kupunguza kiwango cha kodi ya mapato ya makampuni (*Corporate Income Tax*) kutoka asilimia 30 hadi asilimia 25 kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka ujao wa fedha hadi mwaka 2020/2021 kwa viwanda vilivyopo vinavyozalisha bidhaa hiyo hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, narudia tena. Serikali pia imeamua kupunguza kiwango cha kodi ya mapato ya makampuni (*Corporate Income Tax*) kutoka asilimia 30 hadi asilimia 25 kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka ujao wa fedha hadi mwaka 2020/2021 kwa viwanda vilivyopo hivi sasa hapa nchini ambavyo vinavyozalisha bidhaa hii. Aidha, ni matumaini ya Serikali kuwa hatua hii itasaidia viwanda hivyo kuongeza uzalishaji wa taulo za kike na kupunguza bei ya taulo hizo. Kwa upande mwingine itaongeza matumizi ya pamba inayozalishwa hapa nchini, na pia itaongeza ajira, na hii ni pamoja na hatua nydingine ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezieleza; kwa maana ya ujenzi wa viwanda kimoja na *MSD* na kingine kule Simiyu kwa ajili ya kuzalisha bidhaa hii muhimu kwa ajili ya watoto wetu wa kike na wakina Mama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatua ya tatu inabaki ileile kwamba tunafuta msamaha wa *VAT* uliokuwa unatolewa kwenye taulo za kike kwa kushindwa kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hiyo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa badala yake kuwanufaisha wafanyabiashara. Kwa kweli lengo la Serikali ni kumnufaisha mtoto wa kike na sio wafanyabiashara kujilimbilikizia faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kusisitiza kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba bidhaa hiyo muhimu inapatikana kwa bei nafuu na hivyo kuwawezesha watoto wa kike na wanawake kuinunua. Kwa msingi huo tutaingia mkataba wa makubaliano yaani *performance agreement* na kila mwekezaji atakayenufaika na punguzo hili la kodi ya mapato ambaa utaainisha wajibu

wa kila upande, lakini sasa Serikali itafuatilia pia mwenendo wa bei za hizo taulo za kike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kwamba Serikali iboreshe maslahi ya Watumishi wa Umma. Serikali inathamini sana mchango wa watumishi wa umma katika maendeleo ya nchi yetu na si kweli kwamba Serikali imewasahau watumishi kama ilivvyozungumza na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha kuwa maslahi ya Watumishi wa Umma yanaboreshw. Katika mwaka 2016/2017 Serikali ilipunguza kodi kwenye mishahara yaani *payee* kutoka *digit* mbili mpaka *digit* moja. Aidha, mpaka kufikia bei mwaka 2018/2019, Serikali imelipa madai mbalimbali ya watumishi jumla ya shilingi billioni 64.97 na pia ilipandisha madaraja watumishi wote waliokuwa wanastahili, ambapo jumla ya shillingi billioni 14.55 zilitumika kufika Mei, 2019.

Mheshimiwa Spika, naomba nilitaarifu Bunge lako kuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi iko pale pale kama alivyoahidi wakati wa kuadhimisha Sherehe za Mei mosi mwaka huu 2019 kule Jijini Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kupunguza kodi kwenye mishahara ya watumishi, naomba nilitaarifu niwaatarifu Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikifanya maboresho ya mifumo ya kodi, tozo na ada mbalimbali ili kuongeza mapato; kuboresha mazingira ya kufanya biashara lakini pia mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii yanayoguswa na mfumo huo. Hata hivyo muundo wa uchumi (*economic structure*) umebadilika sana tangu miaka ya 90. Aidha, mahitaji ya fedha za kugharamia matumizi ya kawaida ya Serikali na ya miradi ya maendeleo kwa ustawi wa jamii yetu umeongezeka, lakini pia gharama za maisha kwa wananchi na hususani wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla

kwamba, Serikali inakusudia kuunda timu maalum ya kufanya uchambuzi wa kina utakaohusu kupitia mfumo wa viwango vya kodi, tozo, ada na matumizi ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa lengo la kuvivianisha au kuvibadili ili viendane na wakati. Kazi hiyo pia itapendekeza marekebisho ya sheria na miundo ya taasisi husika. Kazi kama hiyo ilifanyika mara ya mwisho mwaka 1991, miaka 28 iliyopita. Aidha, kwa kuwa kazi hiyo itahusisha kupitia mfumo mzima wa kodi na namna inavyogusa wafanyakazi na makundi mbalimbali ya jamii, wawakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi watashirikishwa kikamilifu katika zoezi hilo. Mapendekezo mengine ambayo yanaweza kutekelezwa kwa taratibu za kiutawala yatakekelezwa kupitia nyaraka mbalimbali zinazotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kwamba deni la Serikali limeendelea kuwa kubwa mwaka hadi mwaka na hivyo kuathiri uchumi wetu na maisha ya wananchi kwa ujumla. Katika kipindi cha mwaka ulioishia Aprili, 2019, deni la Serikali liliongezeka kutoka trilioni 49.86 na kufikia shilingi trilioni 51.03 Aprili, 2019, ambayo ni ongezeko la asilimia 2.35. Pia ikumbukwe kuna utaratibu madhubuti wa kuhakikisha kuwa mikopo inayochukuliwa inazingatia vigezo vyote vya uhimilivu, makadirio ya fedha zitakazotokana na chanzo hiki yanaidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la deni limetokana na mikopo mipya kama nilliyosema kwenye Bajeti Kuu ya Serikali na imetumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo bomba la gesi, ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli na mitambo ya kufua umeme na kadhalika. Hata hivyo, mwenendo wa deni katika nchi zenye mazingira karibu sawa na Tanzania nao unaonesha kuwa nako madeni yanaendelea kuongezeka hususan kutokana na mahitaji makubwa ya kujenga miundombinu na huduma muhimu za jamii. Ukiangalia takwimu za Ghana, Ethiopia, Uganda, Kenya na Rwanda unaona, mwenendo ni kama huu wa kwetu.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba Serikali kukopa ndani kinawaathiri sana wananchi hasa wajasiri amali

na kushindwa kupata mikopo kwenye mabenki na taasisi za fedha na ilidaiwa kwamba ni kutoka kwenye taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Naomba kutoa maelezo kwamba Serikali inakopa katika soko la fedha la ndani kwa utaratibu wa kutoa hatifungani na dhamana za Serikali kwa muda mfupi kuititia minada. Amano hizo zinanunuliwa na watu binafsi, mabenki, mifuko ya hifadhi ya jamii, mashirika ya bima pamoja na taasisi mbalimbali. Kiwango cha kukopa katika soko la ndani kinazingatia uwezo wa soko, kiwango cha ukwasi katika uchumi pamoja na kuhakikisha kuwa haipunguzi uwezo wa taasisi hizo kukopesha sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, sekta ya benki imeendelea kuwa imara na benki zina ukwasi wa kutosha ambao unakadirwa kuwa takribani asilimla 30% ya mahitaji ya malipo mbalimbali ikilinganishwa na ukomo wa chini wa asilimia 20%. Kiwango hiki kinatosha kutoa mikopo kwa wateja na kuwekeza katika maeneo mengine ya uzalishaji, lakini pia Benki Kuu imeshusha kiasi cha amana ambacho mabenki yanatakiwa kuweka Benki Kuu (*statutory minimum reserve*) kutoka asilimia 10% mpaka asilimia 7.5% na hiyo imeongeza ukwasi katika mabenki kwa ajili ya kukopesha na kuwekeza katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ilikuwepo hoja kwamba Serikali kuititia Wizara ya Fedha imekuwa ikifanya mabadiliko kwenye bajeti iliyopitishwa na Bunge kimya kimya bila kuomba ridhaa ya Bunge, *this is very serious allegation*. Mpaka kufika Machi 2019 Serikali ilitoa mgawanyo wa matumizi ya kawaida kwa Wizara na Idara Zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri kiasi cha shilingi bilioni 355.815 zaidi ya bajeti iliyokuwa imepitishwa na Bunge ya shilingi trilioni 20.468 na kufanya jumla ya fedha iliyotolewa kuwa shilingi trilioni 20.824 na kwamba hii inakiuka sheria ya bajeti kwa kubadili matumizi ya fedha tofauti na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya Bajeti ya Serikali kuidhinishwa na Bunge ikiwa ni pamoja na kuidhinisha sheria ya matumizi ya mwaka (*Appropriation Act*) hatua inayofuata ni utekelezaji wa bajeti ambapo Waziri mwenye dhamana ya fedha amepewa mamlaka ya kusimamia na kudhibiti utekelezaji, ufuutiliji na tathmini kwa mujibu wa kifungu cha 10(2)(b) cha Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015. Kifungu hiki kinasomeka kwamba nanukuu:

*"The Minister shall be responsible for controlling and supervising the preparation, execution and monitoring of the budget including adjustment to the budget".*

Mheshimiwa Spika, vilevile Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015 imetoa Mamlaka kwa Waziri wa Fedha na Maafisa Masuuli kufanya marekebisho ya bajeti iliyopitishwa na Bunge wakati wa utekelezaji wabajeti. Marekebisho haya hufanywa ili kuwezesha Mafungu kutekeleza baadhi ya shughuli ambazo makadirio hayatoshelezi kwenye vifungu vilivytengwa wakati wa maandalizi ya bajeti. Kwa upande wa Maafisa Masuuli ni kifungu cha 27(1) cha Kanuni za Sheria ya Bajeti ambacho kinawapa Mamlaka ya kufanya uhamisho wa ndani ya mafungu yao kwa kiwango kisichozidi asilimia 7% ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 28(2) cha Kanuni za Sheria ya Bajeti kinampa Waziri wa Fedha Mamlaka ya kufanya uhamisho wa bajeti kati ya Mafungu kwa kiwango kisichozidi asilimia 9% ya bajeti yote ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mpaka kufikia mwezi Aprili uhamisho wa fedha ndani ya mafungu umefikia shilingi bilioni 964.6 ambayo ni sawa na asilimia 2.7 ya bajeti ya Serikali iliyopitishwa na Bunge kwa mwaka huu wa fedha. Aidha, uhamisho wa Fedha kati ya mafungu ni shilingi bilioni 660.78 sawa na asilimia 2.03 ya bajeti ya Serikali iliyopitishwa na Bunge kwa mwaka 2018/2019, hivyo marekebisho ya bajeti yaliyofanywa kwa mwaka huu wa fedha yako ndani ya wigo unaoruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, Bunge huwa linapewa taarifa ya uhamisho wa fedha kwa mafungu namba moja na namba mbili kwa mujibu wa kifungu cha 41(8) cha Sheria ya Bajeti. Katika mwaka 2018/2019, taarifa hizo za uhamisho wa nusu mwaka yaani Julai mpaka Disemba, ziliwasilishwa kwenye kikao cha Bunge cha mwezi Januari 2019 na nimebeba hapa nakala ya *statement of reallocation between vote, reallocation* namba moja ya mwaka 2018/2019 ambayo ilishagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba tuanze sasa kutumia mfumo wa uchumi wa soko jamii hapa nchini na kwamba mfumo huu umefanikiwa kuziimarisha na kuendeleza nchi mbalimbali duniani na wakati huo kuwaondoa wananchi wa nchi hizo kwenye umaskini na kuwapatia fursa za ajira zenyе uhakika. Nafikiri hapa Waheshimiwa Wabunge naomba waniazime masikio kidogo kwa sababu nataka kutoa darasa kidogo. Mfumo wa uchumi wa soko jamii yaani *social market economy* ni mfumo wa uchumi ambao unaendeshwa kwa kuchanganya misingi ya uchumi wa soko pamoja na dola kutoa huduma za jamii bure kwa wazee, wagonjwa, wasiojiweza, maskini na wasio na kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mfumo huu uliasisiwa Ujerumani na Australia ukijulikana kwa jina la Kijerumani, sasa bahati mbaya sijui Kijerumani. Baadhi ya nchi za Ulaya na zilifanyika hivyo kushughulikia hifadhi ya jamii, huduma za afya kwa makundi ya jamii kama hao niliovataja. Sasa msingi wa uchumi wa soko jamii ni soko huria lakini pia utoaji wa *social safety net* na ili mfumo wa uchumi jamii uweze kufanya kazi ipasavyo, yapo walau masharti matatu ambayo ni lazima yatekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kwamba Serikali iwe na uwezo wa kukusanya mapato ya kutosha kuendesha Serikali, kugharamia miradi, shughuli za maendeleo na matumizi ya umma na hususan miundombinu ya msingi ya usafirishaji, nishati, afya na kadhalika, lakini mapato ya ziada kuweza kugharamia progam za jamii yaani *welfare programmes*, hilo

ndio sharti la kwanza. Sharti la pili ni lazima nchi iwe na usimamizi madhubuti wa fedha za umma na sharti la tatu lazima pawepo utaratibu wa wazi na wa haki katika kugawa rasilimali na mapato ya nchi kwa makundi ya nchi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo hayo kuhusu huo mfumo wa uchumi wa soko jamii ni wazi kuwa mazingira ya mfumo huo ili ufanye kazi ipasavyo, bado yanahitajika kujengwa hapa nchini na Serikali ya Awamu ya Tano imeweka nguvu kubwa katika kujenga misingi hiyo. Serikali ya Awamu ya Tano imemelekeza nguvu kupanua wigo wa mapato kuitia ajenda ya kujenga uchumi wa viwanda na kuongeza ukusanyaji wa mapato sambamba na kuziba mianya ya uvujaji wa mapato. Pia Serikali imeweka mkazo katika kusimamia matumizi ya fedha za umma. Serikali pia imechukua hatua kuhimiza kila mtu afanye kazi na kulinda rasilimali za nchi ili ziwanufaishe Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hivyo nawasihi wenzetu upande wa pili wasikimbilie kuiga yaani *copy and paste* bila kujenga misingi ya mfumo huo kuweza kufanya kazi katika mazingira na tamaduni za Mtanzania. Ni vyema pia kutambua kwamba mfumo huo una upungufu na athari zake, kwa mfano watu wanaoishi kwa kutegemea *social protection* huko kwingine, wanadharauliwa na kuonekana ni wavivu, wenyе akili ndogo na wanaishi kwa jasho la wengine. Pia mfumo huo unaweza kuuwa kabisa utaratibu wetu mzuri wa jamii au familia kusaidiana (*social capital*) kwa mfano katika kusomesha watoto wa kaka au wa wadogo zetu. Kwa hiyo ni muhimu kidogo tuwe waangalifu, tusiende tu kubeba kilichofanikiwa Ujerumani tukakileta hapa kwetu sasa hivi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba nihamie kwenye hoja moja nzito ambayo ilisemwa sana na ndugu zetu kutoka Zanzibar na hususan ikihusu kucheleva kusainiwa kwa mkataba wa mkopo wa Saudi na *BADEA* kuhusu ujenzi wa barabara ya Wete Chakechake, kucheleva kusainiwa kwa mkataba wa mkopo kati ya Serikali ya Muungano na *Exim Bank of China* utakaogharamia mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume, *Terminal Two*, lakini pia

kuchelewa kusainiwa kwa mkataba wa mkopo kati ya Serikali ya Muungano na *Exim Bank* ya China kugharamia ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duru.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na mkataba wa mkopo wa Saudi na *BADEA* kuhusu ujenzi wa barabara ya Wete Chakechake. Kwanza mradi huu unajumuisha ukarabati wa barabara ya Wete hadi Chakechake ambayo ina urefu wa kilomita 22.1. Mradi huu unategemea kufadhiliwa kwa fedha za mkopo kutoka *BADEA* dola za Marekani milioni 10, Saudi *Fund* dola za Marekani milioni 11.4, Serkali ya Mapinduzi Zanzibar dola za Marekani milioni 3,000,000 na hivyo kufanya jumla ya dola kuwa milioni 24.4. Licha ya Serikali kusaini mkatana na *BADEA*, mkataba wa Saudi *fund* umekwamishwa na kifungu katika mkataba kinachoitaka Serikali kuweka mali zake kama dhamana ya mkopo, mali zilizotajwa katika kifungu hicho ni pamoja na mali za Jeshi la Wananchi wa Tanzania, mali za Benki Kuu ya Tanzania, Malikale (*cultural heritage*), mali za kihistoria (*historical objects*) na mali za Ubalozi, lakini pia mali nyingine zilizoainishwa katika sheria ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri sharti hili ni kinyume cha sheria za nchi na nasema kweli siwezi kusaini mkataba kwa niaba ya Watanzania kwa sharti hili. Wanaosema nina roho mbaya sana, sawa ni maoni yao, lakini mimi Philip Mpango kamwe sahihi yangu haitatumika kuuza nchi. Pia miradi ya Bara inayosemekana imesainiwa kwa sharti hilo kwa hakika haikukopewa kwa sahihi yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na miradi ya Bara inayosemekana imesainiwa kwa sharti hilo kwa hakika haikukopewa kwa saini yangu.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua mkwamo huu Serikali inaendelea na mazungumzo ya kidiplomasia na Serikali ya Saudi Arabia kama iliyoshauriwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili waweze kuondoa sharti hili. Napenda niwakumbushe pia kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Waziri wa Fedha na Mipango

anashauriwa na kamati mbili; Kamati ya Kitaalam (*TDMC*) na Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Madeni (*National Debt Management Committee*) ambazo zote zina wajumbe kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hakuna mradi hata mmoja wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao kamati hizi zilinishauri nikope kwa niaba ya Serikali nikakataa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, Mkataba wa Mkopo Kati ya Serikali ya Muungano na *Exhim Bank of China* kugharamia ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Amani Abeid Karume, *Terminal Two*. Serikali imekuwa ikifanya majadiliano na Benki ya Exhim ya China ili kupata mkopo kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume, (*Terminal Two*) kwa kiasi cha Dola za Marekani milioni 60. Majadiliano ya kwanza na benki hiyo yalifanyika Disemba, 2018. Exhim ilialika Tanzania kwa majadiliano ya pili ili yafanyike China mwezi Aprili, 2019.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, majadiliano hayo hayajafanyika kwa vile Serikali bado inafanya kazi masharti hasi kwenye rasimu ya mkataba. Na tunachotaka sisi ni kurekebisha kifungu cha mkataba ambacho kama ilivyo kwenye mradi nilitangulia kuuelezea nacho kinaitaka Serikali kuweka dhamana baadhi ya mali zake zikiwemo mali za Jeshi la Wananchi wa Tanzania, mali za Benki Kuu ya Tanzania, mali kale, mali za kihistoria, mali za ubalozi na mali nyiningine ambazo zimeainishwa katika sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumewataka waondoe sharti la kuhusisha mkopo huu na deni la kiwanda cha urafiki. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na majadiliano ya kidiplomasia, ili kitatua mkwamo huo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa tatu ni Mkataba wa Mkopo kati ya Serikali ya Muungano na *Exhim Bank of China* kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Mradi huu unatarajiwa kugharimu kiasi cha dola za Marekani milioni 200 ambazo zitakuwa ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Exhim ya China; na Serikali ya Muungano iliomba

ipatiwe nakala ya upembuzi yakinifu ya mradi huu ili ufanyike uchambuzi na vyombo husika.

Mheshimiwa Spika, hatua ya Serikali kufanya uhakiki imekuwa ikifanyika kwa miradi mbalimbali inayofadhiliwa kwa mikopo nafuu ili tujiridhishe kabla ya kusaini mikataba husika; na hii tunafanya kwa miradi yote. Lengo letu ni kuepuka kuingia gharama kubwa zisizoendana na thamani ya mradi ili tuhakikishe kuwa Serikali inanufaika vyema na mkopo wa masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, taarifa zote hizi nilizozieleza tulizitoa kwenye kikao cha kujadili changamoto za muungano kilichoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mkamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutolewa maelekezo kuwa kila linalowezekana lifanyiwe kazi ili tufikie mwisho haraka iwezekanavyo. Taarifa za kikao hicho zipo tena kwa maandishi, kwa hiyo inashangaza kweli kwa nini wenzetu hawakupewa hiyo taarifa yake na badala yake ninavikwa roho mbaya sana, naomba tu Mwenyezi Mungu awabariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia kwamba Sera za Uchumi na Fedha za Tanzania Bara zina athari za moja kwa moja kwenye uchumi wa Zanzibar bila Zanzibar kuwa na *intervention* yoyote, lakini pia kwamba hadi sasa Serikali hajiaunda Kamati ya Pamoja ya Fedha ya Muungano na hivyo kuvunja Katiba na pia kwamba mapato ya Zanzibar ni asilimia mbili na mapato ya Bara ni asilimia 98, asilimia 68 mapato yote yanatumika Tanzania Bara wakati asilimia 32 yanatumika kwenye taasisi za muungano; na kwa hiyo Zanzibar inatakiwa ilipwe trilioni 4.6 kutoka kwenye mapato ya muungano kwa kutumia *formula* ya mgawo wa asilimia 4.5.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo kwamba, Sera za Uchumi na Fedha za Jamhuri ya Muungano ni jumuishi na zinazingatia mahitaji ya Zanzibar na Tanzania Bara. Sera hizo zinahusisha hali halisi ya uchumi ya pande zote mbili za muungano. Sera ya Uchumi na Bajeti inapitishwa na Bunge

la Jamhuri ya Muungano ambalo linajumuisha Wabunge wa pande zote za muungano. Aidha, Sera ya Fedha hupitishwa na Kamati ya Sera ya Fedha (*Monetary Policy Committee*) ambayo ina uwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuhusu akaunti ya pamoja; ni kweli lbara ya 133 ya Katiba inazungumzia uwepo wa akaunti hiyo ya pamoja ambapo zitawekwa fedha zote zitakazochwngwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa sheria iliyyotungwa na Bunge kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Mungano kwa mambo ya muungano.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa pamoja hivi sasa zinaandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri na hilli ni agizo kutokana na kile kikao tulicho fanya mwezi Februari chini ya Mheshimiwa Makamu wa Rais; kuhusu utaratibu wa kuchangia gharama za muungano na kugawana mapato ya muungano ili kuwezesha kuwepo utaratibu wa kudumu wa kuchangia gharama za muungano na kugawana mapato ya muungano.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huo wa pamoja utakapofikiwa utawezesha kufunguliwa kwa akaunti ya fedha ya pamoja na kwa kuwa, mapendelekezo ya uanzishwaji wa akaunti ya pamoja yapo katika ngazi ya uamuzi makubaliano yaliyopo ni kwamba mapato yanayotokana na utekelezaji wa mambo ya muungano yanayokusanywa Zanzibar yatumike Zanzibar kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa shughuli za maendeleo kule visiwani.

Mheshimiwa Spika, aidha, mapato ya muungano yanayokusanywa Tanzania Bara yatumike kugharamia mambo ya muungano na yasiyo ya muungano Tanzania Bara. Kutokana na makubaliano hayo pande mbili za muungano zimeendelea kunufaika na mapato ya muungano yatokanayo na kodi yanayokusanywa na *TRA*. Mapato hayo ni kodi ya mapato, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa

zinazozalishwa ndani ya nchi. Pia kila upande wa muungano umeendelea kunufaika na mapato yanayotokana na misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo pamoja na gawio la Benki Kuu. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa inarejesha mapato ya kodi yanayotokanayo na mishahara ya watumishi (*pay as you earn*) wa muungano wanaofanya kazi upande wa Zanzibar. Maeleozo yote haya yapo kwenye kumbukumbu za mikutano ambayo tunafanya kwenye vikao rasmi kabisa baina ya Serikali zote mbili kuhakikisha kwamba muungano wetu unadumu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa nchi (Mazingira) ameелеza vizuri; maana palikuwa na hoja kwamba bajeti hii ya Serikali hajaeleza utekelezaji wa miradi ya maendeleo upande wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kusisitiza miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa nchini inatokana na hatua za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambaao ni sehemu ya Mpango Elekezi wa Miaka 15 wa kutekeleza Dira ya Taifa. Kwa upande wa Zanzibar kuna dira ya maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020 ambayo inatekelezwa na SMZ kupitia Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umasisikini (MKUZA), na sasa ni MKUZA III. Hivyo, utekelezaji wa miradi ya maendeleo upande wa Zanzibar unaainishwa na kutekelezwa kupitia MKUZA III na Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Miradi ya maendeleo kwa upande wa Zanzibar inatekelezwa baada ya kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwamba hoja ni nyingi sana, nitazileta kwa maandishi. Naomba uniruhusu niweze kuhitimisha.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Dokta John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anavyotuambia mara kwa mara, kwamba, maendeleo hayana chama. Tena ameendelea kusisitiza kwamba Tanzania ni nchi yetu wote. Hivyo naomba

nihitimishe kwa kusema kuwa bajeti ni nyenzo muhimu ya kufikia matarajio ya wananchi wetu. Na ninawaomba kila mmoja wetu, Waheshimiwa Wabunge, aipigie bajeti hii ya nne ya Serikali ya Awamu ya Tano kura ya ndiyo ili tukaitakeleze kwa manufaa ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kukushukuru tena na pia kuwashukuru viongozi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, bila kumsahau Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ambaye pia ni *Care Taker Minister*, Dkt. Ashatu Kijaji na viongozi wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha, Wakurugenzi, Wataalam, Watumishi wenzangu wote kwa kujitoa kunisaidia katika kulitumikia taifa letu na wananchi wake usiku na mchana hadi kufikia hatua hii; ninamuomba Mungu awabariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, asante sana kwa fursa hii ya kuhitimisha mjadala huu na asante sana kwa Mungu kwa baraka na nguvu na uwezo alionikirimia kufanya kazi yake mpaka dakika hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Philip Mpango, ahsante sana kwa kuhitimisha hoja yako na kujibu hoja za Wabunge.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mwongozo.

**SPIKA:** Enhee. Nimekuona Mheshimiwa.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), lakini kwa maelekezo yako na ridhaa yako, Kanuni ya 5 ya Kanuni za Kudumu za

Bunge; kwa kuwa jambo hili halijatokea Bungeni, lakini ni jambo la dharura; na kwa kuwa, Jumuiya za Kimataifa zinaendelea kuungana na kuvunja mipaka ya kiutawala kwa kushirikiana pomoja; na kwa kuwa sasa Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki ikipiga hatua za kimahusiano na kuimarisha umoja wetu kufikiri katika kuondoa mipaka iliyopo.

Mheshimiwa Spika, jana kuna *video* imesambaa iliyosambazwa na Bwana Charles Njagua Kanyi, Mbunge wa Starehe nchini Kenya, akitoa ushawishi wa *xenophobia* kuwashawishi Wakenya kuwafukuza Watanzania na kwamba ametoa saa 24 kwa Watanzania wanaoishi nchini Kenya kuondoka vinginevyo amewashawishi wananchi wake wa Starehe pale mjini kuchukua hatua kali dhidi ya wageni na Watanzania wakiwemo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Muongozo wako kuhusu usalama wa Watanzania wetu wanaoishi nchini Kenya, lakini pia kwa kuzingatia matakwa ya Muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Serikali inachukua hatua gani kutokana na matamko haya ambayo ni mabaya kabisa kutokea katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki?

**SPIKA:** Kwa kuwa jambo hili ndio ninalisikia kutoka kwako Mheshimiwa, naomba tupati muda Serikali walichukue. Naamini kwa jinsi ulivyoliweka hapa lazima lipate maelezo ya Serikali leoleo kwa sababu, endapo hivyo ndivyo liliyuo tumepewe saa 24, kwa hiyo lazima tupate neno. Na Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa naamini jioni ya leo wakati muafaka anawenza akalisemea jambo hili, tutakuwa tumejipanga ili kuweza kupata maelezo ya Serikali kuhusu usalama wa Watanzania. (*Makofii*)

Basi, Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema asubuhi, nawaombeni sana Saa 11:00 kamili kila mmoja wetu awe amekaa mahali pake, ili tuweze kutekeleza jambo hili la kikatiba. Maelezo ya tutafanyaje jambo hilo la kupiga kura jioni tutayatoa jioni mara tutakapowasili hapa. Kwa jinsi hiyo basi naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi Saa 11:00 Jioni ya leo.

(Saa 06:54 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba tukae. Waheshimiwa Wabunge kwa kweli lazima tujipongeze angalau kupiga makofi maana yake leo ni *full House*. Naona kwa kweli kila Mbunge yupo na kiti unachokiona wazi basi kuna udhuru mkubwa, siyo hivi hivi tu maana nina watu walioniomba vibali kidogo lakini kwa kweli leo ni *full House*. Ingekuwa hivi kila siku ingependeza zaidi. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tano, Kikao cha Hamsini na Mbili.

Waheshimiwa Wabunge, nitalazimika kutoa maelezo kidogo kabla hatujaanza zoezi letu, lakini maelezo yangu yatanguliwe na maelezo mengine kwanza kidogo. Yupo rafiki yetu mmoja amekuwa hajipangi kidogo kwenye kuzungumza na ukisikiliza hotuba ile unaweza ukaona kwamba wanaosemwa ni Wabunge hasa waliotoka Misri. Niseme kwamba Wabunge hawa wamefanya walicheweza, hakuna mahali popote Wabunge wetu wamewalaumu wachezaji wetu wa Timu ya Taifa, hakuna mahali popote. (*Makofi*)

Tuliposhuka uwanja wa ndege, Wabunge hawa waliwaomba sana Waandishi wa Michezo ambao walikuwa pale wakiwa wengi kwamba iandikeni vizuri Timu yetu ya Taifa, hakuna mahali, tuwatie moyo wachezaji wetu, ule ndiyo ulikuwa ujumbe kamili.

Haya mengine yanayochukuliwa liliuzwa swali kwa kuwa tumeshiriki na tunategemea kushiriki huko mbele ya safari tufanye nini kuimarisha michezo katika nchi yetu ndiyo yakatoka mawazo mengi kwamba tuwekeze zaidi katika michezo, tuanzishe *academies* na *academies* nydingi zinaanzishwa na makampuni binafsi au klubu na kadhalika.

Tuishauri Wizara ya Elimu ili michezo iwe ni sehemu ya mitaala muhimu ya nchi yetu, tuhakikishe kwamba kuanzia

kwenye Kata, Wilaya na nini lishe kwa wachezaji wetu inakuwa nzuri, tuhakikishe uongozi wa michezo unakuwa ni mzuri katika ngazi zote na tunavyosema michezo tuna maana michezo yote; riadha, *boxing*, *football* na kadhalika, hizo ndizo zilikuwa *comments* za Waheshimiwa Wabunge katika namna gani tujipange zaidi kwa mbele ya safari, siyo kuisema timu yetu hata mara moja. Kwa hiyo, ningeomba Watanzania waelewe hivyo na tuendelee kuwa tunasamehe ndugu zangu, njia hiyo itatusaidia kufika mapema zaidi.

Sasa natoa taarifa yangu ambayo naomba tusikilizane. Kwa kuwa tumehitimisha mjadala wa Makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, amehitimisha hoja yake. Tunatakiwa sasa katika hatua hii kufanya maamuzi kwa kuyapitisha au kutoyapitisha Makadirio hayo.

Kanuni ya 107(2) inaeleza kuhusu utaratibu wa kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Serikali na inasomeka kama ifuatavyo:-

*"Uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kutaja jina la Mbunge mmojammoja."*

Narudia tena; uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutopitisha Bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kutaja jina la Mbunge mmojammoja.

Ibara ya 94(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni ya 77(1) ya Kanuni za Bunge pamoja na mambo mengine zinalekeza kwamba akidi ya Kikao cha Bunge wakati wa kufanya maamuzi ni nusu ya Wabunge wote na hata ninyi wenyewe mkiangalia tu hapa tuna nusu ya Wabunge wote, lakini baadaye Katibu atatuambia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa idadi ya Wabunge wote ni 393, hivyo kabla ya kuanza zoezi la kupiga

kura tunatakiwa kuwa na Wabunge wasiopungua 196 ambayo idadi hiyo ndiyo nusu ya Wabunge wote. hivyo, Katibu wa Bunge atatumia utaratibu unaofaa kutuhakkishia kama tunazidi idadi inayotakiwa kikanuni.

Kanuni ya 79(1) inafafanua kuwa mambo yote yanayohitaji kuamuliwa na Bunge yataamuliwa kwa kufuata maoni ya Wabunge walio wengi waliohudhuria na kupiga kura Bungeni. Hivyo, katika zoezi letu la leo, tutafuata utaratibu ufuata:-

Kwanza, kengele itapigwa ili Waheshimiwa Wabunge walio nje ya ukumbi waingie ndani. Pili, Katibu atawahesabu Wabunge ili kuona kama akidi inatimia kwa maana ya kwamba tunafikia na kuzidi 196. Tatu, zoezi la kupiga ambapo Katibu atasoma majina ya Wabunge mmoja baada ya mwininge na kila anayeitwa atatoa uamuzi wake kwa kusema ndiyo au hapana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, kura zitahesabiwa kisha tutapatiwa matokeo kuhusiana na makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namkaribisha Katibu wa Bunge ili atupatie idadi yetu tuweze kuendelea na zoezi hili, lakini kabla ya Katibu kwanza naomba *Sargent-at-Arms* sasa ugonge hiyo kengele yako na kama kuna Wabunge wowote *canteen* au mahali pengine tunaomba waahairishe wanachokifanya waweze kujunga nasi hapa ndani.

Mheshimiwa dakika mbili, halafu nitakupa nafasi, nimeshakuona. Sawa, sasa nipo tayari kukusikiliza Mheshimiwa Zitto, nilikuona.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ambalo naomba nipate ufanuzi wako.

Mheshimiwa Spika, muda mfupi uliopita umeelezea jambo ambalo limetokea nje ya Bunge ambapo mmoja wa viongozi wa Serikali mbele ya Kiongozi Mkuu wa nchi amewabagaza Wabunge ikiwemo wewe mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maelezo ambayo umeyatoa umetoa maelezo kana kwamba siyo Mkuu wa Mhimili. Umetoa maelezo kana kwamba unajitetea mbele ya kiongozi huyo, kitu ambacho nadhani tunapaswa tupate mwongozo wako kwa sababu kwa maelezo ambayo umeyatoa, atatoka mwingine atawasema Wabunge kwa lolote na hatutakuwa na chochote cha kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunakufahamu kwamba wewe ni mtu ambaye hauruhusu Mhimili huu wa Bunge kuchezewa, kutomaswatomaswa na kudharauliwa. Ni nini kimecupata leo unaongea kana kwamba lile lilloongeleta ni jambo dogo, unasamehe kabla hujachukua hatua yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba usimame kulinda hadhi ya Bunge kwamba Wabunge hawajawasema wachezaji, Wabunge wanaunga mkono wachezaji na utoe maelekezo kama Mhimili wa Bunge, kama Mkuu wa Mhimili na siyo kama mtu ambaye unajitetea mbele ya viongozi wadogo wa Serikali ambao wanaona sasa ni hali ya kawaida kulitomasatomasa na kulidharau Bunge. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ningombwa Waheshimiwa Wabunge tusilikuze sana jambo hili, kabisa na ndiyo maana nikamalizia hivyo nilivyomalizia. Kama Wabunge wangkuwa na mawazo ya kwamba timu ya wachezaji, wachezaji wetu wana matatizo hivi wangeondoka Wabunge 30 kesho kwenda kwa ajili ya timu yetu hiyo hiyo, lingewezekana wapi jambo kama hilo? Lisingewezekana, hayo ni mawazo ya mtu mmoja ambaye kidogo ndiyo hivyo na sisi tusije tukateleza tukajikuta tumekwenda kushoto kidogo. (*Makofi/Kicheko*)

Niseme maoni yangu na kama Spika, ni bahati mbaya sana kwamba tuna viongozi wa Serikali wanadiriki

kumdanganya Rais hadharani. Kiongozi wa Serikali unapoongea mbele ya Rais jipange, ongea ukweli mtupu wa Mwenyezi Mungu unaoujua. Usisingizie mtu, usimuonee mtu; hatufanyi hivyo, lakini sasa bahati mbaya ndiyo hiyo. (*Makofi*)

Na sisi hatusemi kila kitu hapa, natamani ningefunguka kidogo kuhusu... (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Funguka.

**SPIKA:** Inatosha, inatosha. Huyu... inatosha jamani. Nasema wazi mbele ya Mwenyezi Mungu bahati mbaya Kijana wetu huyu hajitambui, hajielewi na kwa sababu ana nguvu aliyonayo, ana makundi ya vijana kwenye mitandao anaweza akamtukana Spika, wakafanya hivi kwa hiyo *he thinks he is above everyone*, si vizuri namna hiyo; unawasingizia Wabunge wamekosa nini? (*Makofi*)

*Actually*, kama kuna mtu ana deni la kufanya kidogo kuhusu hawa wachezaji nasema sitaki kusema, ni yeye. Kama kuna mtu akitaka niseme kwa nini ni yeye... (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Apeleke milioni 10.

**SPIKA:** Lakini kwa leo inatosha hapa tulipofika. (*Makofi*)

Katibu tupatие idadi. (*Makofi*)

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, idadi kamili ya Wabunge waliopo ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa sasa ni 345 na inawezekana ikaongezeka kwa kuwa baadhi ya Wabunge bado wanaendelea kuingia. Kwa kuwa idadi hiyo ni zaidi ya nusu ya Wabunge wote na inatosha kuendelea na zoezi la kupiga kura, naomba uridhie tuendelee na hatua inayofuata.

**SPIKA:** Sasa tunaendelea na hatua inayofuata, kuna neno lolote natumaini hakuna neno ili tuanze.

Waheshimiwa Wabunge, Katibu alikwishaandaa kijitabu hiki chenyé kila kitu na namna majina yatakavyoitwa. Kwa hiyo, nitawaomba Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane, tutashindwa kufanya tofauti na kitabu hiki kinavyoélékeza ili kazi ya kuhesabu na kadhalika kufanya *tallying* iwe nyepesi zaidi ili tuweze kupata majibu kwa uharaka.

Kwa hiyo, naomba tusikilize majina yetu vizuri na kura zetu ni tatu kama kawaida ni kura ya ndiyo, kura ya hapana na kura ya kunyamaza au inaitwa ku-*abstain*; kura ya ndiyo, hapana na kunyamaza au ku-*abstain*.

Sasa Katibu naomba wote tusikilizane ili tuanze kupiga kura.

### **KUPIGA KURA**

#### **NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

Mhe. Dkt. Tulia Ackson	- Ndiyo
Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa	- Ndiyo
Mhe. Mussa Azzan Zungu	- Ndiyo
Mhe. Andrew John Chenge	- Ndiyo
Mhe. Najma Murtaza Giga	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Adelardus Lubango Kilangi	- Ndiyo
Mhe. Selemani Saidi Jafo	- Ndiyo
Mhe. Capt. Mst. George Huruma Mkuchika	- Ndiyo
Mhe. January Yusuf Makamba	- Ndiyo
Mhe. Jenista Joakim Mhagama	- Ndiyo
Mhe. William Vangimembe Lukuvi	- Ndiyo
Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe	- Ndiyo
Mhe. Angella Jasmine Kairuki	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango	- Ndiyo
Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga	- Ndiyo
Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako	- Ndiyo
Mhe. Ummy Ally Mwalimu	- Ndiyo
Mhe. Prof. Paramagamba Aidan John Kabudi	- Hakuwepo

Mhe. Luhaga Joelson Mpina	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Medard Matogoro Kalemani	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla	- Ndiyo
Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwelwe	- Ndiyo
Mhe. Kangi Alphaxard Lugola	- Ndiyo
Mhe. Doto Mashaka Biteko	- Ndiyo
Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga	- Hakuwepo
Mhe. Innocent Lughwa Bashungwa	- Ndiyo
Mhe. Joseph Sinkamba Kandege	- Ndiyo
Mhe. Antony Peter Mavunde	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa	- Ndiyo
Mhe. William Tate Ole Nasha	- Ndiyo
Mhe. Abdallah Hamis Ulega	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji	- Ndiyo
Mhe. Angeline Sylvester Mabula	- Ndiyo
Mhe. Elias John Kwandikwa	- Ndiyo
Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile	- Ndiyo
Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni	- Ndiyo
Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye	- Ndiyo
Mhe. Subira Khamis Mgalo	- Ndiyo
Mhe. Jumaa Hamidu Aweso	- Ndiyo
Mhe. Juliana Daniel Shonza	- Ndiyo
Mhe. Stella Ikupa Alex	- Ndiyo
Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo	- Ndiyo
Mhe. Omar Tebweta Mgumba	- Ndiyo
Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Damas Danieli Ndumbaro	- Ndiyo
Mhe. Mussa Ramadhan Sima	- Ndiyo
Mhe. George Boniface Simbachawene	- Ndiyo
Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa	- Ndiyo
Mhe. Jasson Samson Rweikiza	- Ndiyo
Mhe. Peter Joseph Serukamba	- Ndiyo
Mhe. Vedasto Edgar Ngombale	- Hapano
Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni	- Ndiyo
Mhe. Moshi Selemani Kakoso	- Ndiyo
Mhe. Dunstan Luka Kitandula	- Ndiyo
Mhe. Emanuel Adamson Mwakasaka	- Ndiyo
Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq	- Ndiyo
Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa	- Ndiyo

Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka-	Hapana
Mhe. Abdallah Dadi Chikota	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma-	Ndiyo
Mhe. Kemilembe Julius Lwota	- Ndiyo
Mhe. Mwanne Ismail Mcchemba	- Ndiyo
Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri	- Ndiyo
Mhe. William Mganga Ngeleja	- Ndiyo
Mhe. Juma Selemani Nkamia	- Ndiyo
Mhe. Salum Mwinyi Rehani	- Ndiyo
Mhe. Zaynabu Matitu Vulu	- Ndiyo
Mhe. Khalfan Hilaly Aeshi	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga	- Ndiyo
Mhe. Hawa Mchafu Chakoma	- Ndiyo
Mhe. Freeman Aikaeli Mbowa	-Hapana ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Tundu Mughwai Lissu	- Hakuwepo
Mhe. John John Mnyika	- Hapana
Mhe. Raphael Japhary Michael	- Hapana
Mhe. Ruth Hiyob Mollel	- Hapana
Mhe. Ally Saleh Ally	- Hapana
Mhe. Ester Amos Bulaya	- Hapana
Mhe. Halima James Mdee	- Hakuwepo
Mhe. James Francis Mbatia	- Hakuwepo
Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa	- Hapana
Mhe. Juma Hamad Omar	-Ndiyo ( <i>Makofi/Vigelegele</i> )
Mhe. Godbless Jonathan Lema	- Hakuwepo
Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare	- Hapana
Mhe. Esther Nicholas Matiko	- Hapana
Mhe. Antony Calist Komu	- Hapana
Mhe. Susan Anselm Lyimo	- Hapana
Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi	- Hapana
Mhe. Hamidu Hassan Bobali	- Hapana ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Yussuf Kaiza Makame	- Hakuwepo
Mhe. David Ernest Silinde	- Hapana
Mhe. Qambalo Willy Qulwi	- Hapana
Mhe. John Wegesa Heche	- Hapana
Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi	- Hapana
Mhe. Masoud Abdallah Salim	- Hapana
Mhe. Cecilia Daniel Paresto	- Hakuwepo
Mhe. Cecil David Mwambe	- Hapana
Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf	- Hapana

Mhe. Zubeda Hassan Sakuru	- Hakuwepo
Mhe. Devota Mathew Minja	- Hapana
Mhe. Peter Ambrose Lijualikali	- Hapana
Mhe. Rashid Ali Abdallah	- Hapana
Mhe. Maida Hamad Abdallah	- Ndiyo
Mhe. Hamida Mohamed Abdallah	- Ndiyo
Mhe. Munde Tambwe Abdallah	- Ndiyo
Mhe. Bahati Ali Abeid	- Ndiyo
Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood	- Ndiyo
Mhe. Khadija Hassan Aboud	- Ndiyo
Mhe. Lameck Okambo Airo	- Ndiyo
Mhe. Ajali Rashid Akbar	- Ndiyo
Mhe. Abdallah Haji Ally	- Hapana
Mhe. Jamal Kassim Ali	- Ndiyo
Mhe. Khadija Nassir Ali	- Ndiyo
Mhe. Khamis Mtumwa Ali	- Ndiyo
Mhe. Mbarouk Salim Ali	- Hapana
Mhe. Hussein Nassor Amar	- Ndiyo
Mhe. Wanu Hafidh Ameir	- Ndiyo
Mhe. Zainab Mndolwa Amir	- Ndiyo ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Ussi Salum Pondeza Amjadi	- Ndiyo
Mhe. Saul Henry Amon	- Ndiyo
Mhe. Jaku Hashim Ayoub	- Ndiyo
Mhe. Omary Ahmad Badwel	- Ndiyo
Mhe. Nuru Hawadh Bafadhili	- Ndiyo ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Faida Mohamed Bakar	- Ndiyo
Mhe. Zainab Mussa Bakar	- Hapana
Mhe. Hussein Mohamed Bashe	- Ndiyo
Mhe. Mbarak Salim Bawazir	- Ndiyo
Mhe. Innocent Sebba Bilakwate	- Ndiyo
Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba	- Ndiyo
Mhe. Abdallah Majura Bulembo	- Ndiyo
Mhe. Halima Abdallah Bulembo	- Ndiyo
Mhe. Selemani Said Bungara	- Hapana
Mhe. Felister Aloyce Bura	- Ndiyo
Mhe. Jerome Dismas Bwanausi	- Ndiyo
Mhe. Marwa Ryoba Chacha	- Ndiyo
Mhe. Josephine Tabitha Chagula	- Ndiyo
Mhe. Lathifah Hassan Chande	- Hapana
Mhe. Mary Pius Chatanda	- Ndiyo

Mhe. Sikudhani Yassini Chikambo – Ndiyo  
Mhe. Eng. Christpher Kajoro Chiza – Ndiyo  
Mhe. Dkt. Rashid Mohamed Chuachua – Ndiyo  
Mhe. Cosato David Chumi – Ndiyo  
Mhe. Mbaraka Kitwana Dau – Ndiyo  
Mhe. Dkt. David Mathayo David – Ndiyo  
Mhe. Makame Mashaka Foum – Ndiyo  
Mhe. Tauhida Cassian Galoss – Ndiyo  
Mhe. Alex Raphael Gashaza – Ndiyo  
Mhe. Pauline Philipo Gekul – Ndiyo  
Mhe. Josephine Johnson Genzabuke – Ndiyo  
Mhe. Boniphace Mwita Getere – Ndiyo  
Mhe. Anna Joram Gidarya – Hapana  
Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia – Ndiyo  
Mhe. Seif Khamis Gulamali – Ndiyo  
Mhe. Haji Ameir Haji – Ndiyo  
Mhe. Mwantumu Dau Haji – Ndiyo  
Mhe. Othman Omar Haji – Hapana  
Mhe. Khatib Said Haji – Hapana  
Mhe. Azza Hillal Hamad – Ndiyo  
Mhe. Juma Kombo Hamad – Hapana  
Mhe. Paschal Yohana Haonga – Hapana  
Mhe. Joseph Leonard Haule – Hapana  
Mhe. Juma Othman Hija – Ndiyo  
Mhe. Mansoor Shanif Hiran – Ndiyo  
Mhe. Augustine Vuma Holle – Ndiyo  
Mhe. Joram Ismael Hongoli – Ndiyo  
Mhe. Yussuf Salim Hussein – Hapana  
Mhe. Khalifa Mohamed Issa – Hapana  
Mhe. Zacharia Paulo Issaay – Ndiyo  
Mhe. Asha Mshimba Jecha – Ndiyo  
Mhe. Emmanuel Papian John – Ndiyo  
Mhe. Asha Abdullah Juma – Ndiyo  
Mhe. Juma Ali Juma – Ndiyo  
Mhe. Mwantakaje Haji Juma – Ndiyo  
Mhe. Hamoud Abuu Jumaa – Ndiyo  
Mhe. Jafar Sanya Jussa – Ndiyo  
Mhe. Ritta Enespher Kabati – Ndiyo  
Mhe. Risala Saidi Kabongo – Hapana  
Mhe. Mgeni Jadi Kadika – Hapana

Mhe. John Peter Kadutu	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Dalali Peter Kafumu	- Ndiyo
Mhe. Alfredina Apolinairy Kahigi	- Ndiyo ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Haji Khatib Kai	- Hapana
Mhe. Joseph George Kakunda	- Ndiyo
Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala	- Ndiyo
Mhe. Vicky Paschal Kamata	- Ndiyo
Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli	- Ndiyo
Mhe. Maria Ndila Kangoye	- Ndiyo
Mhe. Constantine John Kanyasu	- Ndiyo
Mhe. Sebastian Simon Kapufi	- Ndiyo
Mhe. Rukia Ahmed Kassim	- Ndiyo ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Katani Ahmad Katani	- Hapana ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Zainab Athuman Katimba	- Ndiyo
Mhe. Hassan Seleman Kaunje	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa	- Ndiyo
Mhe. Kanali Mst. Masoud Ally Hamis	- Ndiyo
Mhe. Yussuf Haji Khamis	- Hapana ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Sadifa Juma Khamis	- Ndiyo
Mhe. Ali Salim Khamis	- Hapana
Mhe. Fakharia Shomar Khamis	- Ndiyo
Mhe. Mohamed Juma Khatib	- Hapana ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Munira Mustapha Khatibu	- Ndiyo
Mhe. Aida Joseph Khenani	- Hapana
Mhe. Omari Abdallah Kigoda	- Ndiyo
Mhe. Mendrad Lutengano Kigola	- Ndiyo
Mhe. Omari Mohamed Kigua	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe	- Ndiyo
Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete	- Ndiyo
Mhe. Salma Rashid Kikwete	- Ndiyo
Mhe. Ali Hassan Omar King	- Ndiyo
Mhe. Elibariki Immanuel Kingu	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa	- Ndiyo
Mhe. Mariam Nasoro Kisangi	- Ndiyo
Mhe. Jumanne Kibera Kishimba	- Ndiyo
Mhe. Jesca David Kishoja	- Hapana
Mhe. Boniventura Destery Kiswaga	- Ndiyo
Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga	- Ndiyo
Mhe. Allan Joseph Kiula	- Ndiyo
Mhe. Susan Limbweni Kiwanga	- Hapana ( <i>Makofi</i> )

*(Hapa baadhi ya Wabunge waizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tusikilizane kidogo; Katibu hajamsikia Susan, arudie.  
Katibu endelea. (*Makofii/Kicheko*)

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

Mhe. Grace Sindato Kiwelu	- Hapana
Mhe. Silvestry Francis Koka	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Susan Alphonse Kolimba	- Ndiyo
Mhe. Leah Jeremia Komanya	- Ndiyo
Mhe. Yosepher Ferdinand Komba	- Hapana
Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma	- Ndiyo
Mhe. Saed Ahmed Kubenea	- Hapana
Mhe. Zuberi Mohamedi Kuchauka	- Ndiyo
Mhe. Rhoda Edward Kunchela	- Hapana
Mhe. Julius Kalanga Laizer	- Ndiyo
Mhe. George Malima Lubeleje	- Ndiyo
Mhe. Riziki Said Lulida	- Hakuwepo
Mhe. Anna Richard Lupembe	- Ndiyo
Mhe. Livingstone Joseph Lusinde	- Ndiyo
Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge	- Ndiyo
Mhe. Hamad Salim Maalim	- Hapana
Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Ndiyo
Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula	- Ndiyo
Mhe. Khamis Yahaya Machano	- Ndiyo
Mhe. Lucy Simon Magereli	- Hapana
Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe	- Ndiyo
Mhe. Catherine Valentine Magige	- Ndiyo
Mhe. Sonia Jumaa Magogo	- Ndiyo ( <i>Makofii</i> )
Mhe. Esther Alexander Mahawe	- Ndiyo
Mhe. Almas Athuman Maige	- Ndiyo
Mhe. Ezekiel Magolyo Maige	- Ndiyo
Mhe. Kunti Yusuph Majala	- Hapana
Mhe. Salome Wycliffe Makamba	- Hapana
Mhe. Makame Kassim Makame	- Ndiyo
Mhe. Eng. Ramo Mataala Makani	- Ndiyo
Mhe. Joel Mwaka Makanyaga	- Ndiyo

Mhe. Amina Nassoro Makilagi	- Ndiyo
Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	- Ndiyo
Mhe. Tunza Issa Malapo	- Hapana
Mhe. Anne Kilango Malecela	- Ndiyo
Mhe. Angelina Adam Malembeka	- Ndiyo
Mhe. Ignas Aloyce Malocha	- Ndiyo
Mhe. Issa Ali Mangungu	- Ndiyo
Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi	- Ndiyo
Mhe. Sixtus Raphael Mapunda	- Ndiyo
Mhe. Agness Mathew Marwa	- Ndiyo
Mhe. Gimbi Dotto Masaba	- Hapana
Mhe. Hassan Elias Masala	- Ndiyo
Mhe. Stephen Julius Masele	- Ndiyo
Mhe. Augustino Manyanda Masele	- Ndiyo
Mhe. Susanne Peter Maselle	- Hapana
Mhe. Yahaya Omary Massare	- Ndiyo
Mhe. Janeth Maurice Masaburi	- Ndiyo
Mhe. Flatei Gregory Massay	- Ndiyo
Mhe. Aisharose Ndogholi Matembe	- Ndiyo
Mhe. Aisharose Ndogholi Mattembe	- Ndiyo
Mhe. Silafu Juma Maufi	- Ndiyo
Mhe. Lucy Thomas Mayenga	- Ndiyo
Mhe. Kiza Hussein Mayeye	-Ndiyo ( <i>Makofi/Vigelegele</i> )
Mhe. Mussa Bakari Mbarouk	- Hapana
Mhe. Prosper Joseph Mbena	- Ndiyo
Mhe. Janet Zebedayo Mbene	- Ndiyo
Mhe. Richard Philip Mbogo	- Ndiyo
Mhe. Taska Restituta Mbogo	- Ndiyo
Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki	- Hapana
Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria	- Ndiyo
Mhe. Neema William Mgaya	- Ndiyo
Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa	- Ndiyo
Mhe. Godfrey William Mgimwa	- Ndiyo
Mhe. Suzana Chogisasi Mgonukulima	- Hapana
Mhe. Joseph Kizito Mhagama	- Ndiyo
Mhe. Mboni Mohamed Mhita	- Ndiyo
Mhe. Esther Lukago Midimu	- Ndiyo
Mhe. Rehema Juma Migilla	- Ndiyo ( <i>Makofi/Vigelegele</i> )
Mhe. James Kinyasi Millya	- Ndiyo
Mhe. Desderius John Mipata	- Ndiyo

Mhe. Nimrod Elrehema Mkono	- Hakuwepo
Mhe. Joseph Maiko Mkundi	- Ndiyo
Mhe. Martha Moses Mlata	- Ndiyo
Mhe. Goodluck Asaph Mlinga	- Ndiyo
Mhe. Lucia Michael Mlowe	- Hapana
Mhe. Ester Michael Mmasi	- Ndiyo
Mhe. Timotheo Paulo Mnzava	- Ndiyo
Mhe. Ally Keissy Mohamed	- Ndiyo
Mhe. Twahir Awesu Mohammed	- Hapana
Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali	- Ndiyo
Mhe. Amina Saleh Mollel	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel	- Ndiyo
Mhe. Justin Joseph Monko	- Ndiyo
Mhe. Mpakate Daimu Iddi	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda	- Ndiyo
Mhe. Maryam Salum Msabaha	- Hapana
Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi	- Ndiyo
Mhe. Martin Mtonda Msuha	- Ndiyo
Mhe. Shamsia Aziz Mtamba	-Ndiyo ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Abdallah Ally Mtolea	- Ndiyo
Mhe. Daniel Edward Mtuka	- Ndiyo
Mhe. Maulid Said Mtolia	- Ndiyo
Mhe. Muhammed Amour Muhammed	- Hapana
Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo	- Ndiyo
Mhe. Joyce John Mukya	- Hapana
Mhe. Phillipo Augustino Mulugo	- Ndiyo
Mhe. Mary Deo Muro	- Hapana
Mhe. Benardetha Kasabago Mushashu	- Ndiyo
Mhe. Mussa Hassan Mussa	- Ndiyo
Mhe. Joseph Kasheku Musukuma	- Ndiyo
Mhe. Hawa Subira Mwaifunga	- Hapana
Mhe. Frank George Mwakajoka	- Hapana
Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda	- Hapana
Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata	- Ndiyo
Mhe. Fredy Atupele Mwakibete	- Ndiyo
Mhe. Edward Franz Mwalongo	- Ndiyo
Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa	- Ndiyo
Mhe. Venance Methusalah Mwamoto	- Ndiyo
Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi	- Ndiyo
Mhe. Charles John Mwijage	- Ndiyo

Mhe. Hasna Sudi Mwilima	- Ndiyo
Mhe. Abbas Ali Mwinyi	- Ndiyo
Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma	- Ndiyo ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu	- Ndiyo
Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	- Ndiyo
Mhe. Suleiman Masoud Nchambi	- Ndiyo
Mhe. Dkt Mwigulu Lameck Nchemba	- Ndiyo
Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki	- Ndiyo
Mhe. Richard Mganga Ndassa	- Ndiyo
Mhe. Deogratias Francis Ngalawa	- Ndiyo
Mhe. Eng. Edwin Amandus Ngonyani	- Ndiyo
Mhe. Ahmed Juma Ngwali	- Hapana ( <i>Makofi</i> )
Mhe. Oran Manase Njeza	- Ndiyo
Mhe. Dua William Nkurua	- Ndiyo
Mhe. Nape Mosses Nnauye	- Ndiyo
Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwanko	- Ndiyo
Mhe. Albert Obama Ntabaliba	- Ndiyo
Mhe. Musa Rashid Ntimizi	- Ndiyo
Mhe. Nassor Suleiman Omar	- Hapana
Mhe. Lucy Fidelis Owenya	- Hapana
Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo	- Ndiyo
Mhe. Upendo Furaha Peneza	- Hapana
Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed	- Ndiyo
Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab	- Ndiyo
Mhe. Shally Josepha Raymond	- Ndiyo
Mhe. Catherine Nyakao Ruge	- Hapana
Mhe. Dkt. Gertrude Pangalile Rwakatare	- Ndiyo
Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza	- Hapana
Mhe. Machano Othman Said	- Ndiyo
Mhe. Magdalena Hamis Sakaya	- Ndiyo ( <i>Makofi/Vigelegele</i> )
Mhe. Mattar Ali Salum	- Ndiyo
Mhe. Ahmed Ally Salum	- Ndiyo
Mhe. Salum Khamis Salum	- Ndiyo
Mhe. Saada Mkuya Salum	- Ndiyo
Mhe. Deo Kasenyenda Sanga	- Ndiyo
Mhe. Edwin Mgante Sannda	- Ndiyo
Mhe. Njalu Daudi Silanga	- Ndiyo
Mhe. Joseph Roman Selasini	- Hapana
Mhe. Oliver Daniel Semuguruka	- Ndiyo
Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby	- Ndiyo

Mhe. Rashid Abdallah Shangazi	- Ndiyo
Mhe. Shaabani Omari Shekilindi	- Ndiyo
Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla King	- Ndiyo
Mhe. Margaret Simwanza Sitta	- Ndiyo
Mhe. Joyce Bitta Sokombi	- Hapana
Mhe. Jitu Vrajlal Soni	- Ndiyo
Mhe. Rose Kamili Sukum	- Hapana
Mhe. Khalifa Salum Suleiman	- Ndiyo
Mhe. Sabreena Hamza Sungura	- Hakuwepo
Mhe. Grace Victor Tendega	- Hapana
Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest	- Hapana
Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka	- Ndiyo
Mhe. Dkt Charles John Tizeba	- Ndiyo
Mhe. Fatma Hassan Toufiq	- Ndiyo
Mhe. Salim Hassan Turky	- Ndiyo
Mhe. Rose Cyprian Tweve	- Ndiyo
Mhe. Martha Jachi Umbulla	- Ndiyo
Mhe. Ally Seif Ungando	- Ndiyo
Mhe. Khamis Ali Vuai	- Ndiyo
Mhe. Anastazia James Wambura	- Ndiyo
Mhe. Selemani Jumanne Zedi	- Ndiyo
Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto	- Hapana

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama kuna Mbunge  
yejote ambaye hajaitwa jina naomba asimame pale alipo  
ili aweze kupiga kura pande zote. Katibu tuko sawa?

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**  
Mheshimiwa Spika, tuko sawa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Hakuna aliyeachwa hata  
mmoja?

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**  
Hakuna.

**SPIKA:** Basi sasa tuendelee na zoezi la kuhesabu kura.

Waheshimiwa Wabunge, wakati Katibu anaendelea  
na zoezi la kuhesabu kura, asubuhi Mheshimiwa Mchengerwa

aliomba Mwongozo kuhusiana na matamshi yale ya Mbunge wa Kenya, yale matamshi ya ajabu sana, ya hovyo sana, nimeduwa nikilifikiria jambo hili napata tabu kuitaka Serikali iseme chochote kwa sababu matamshi yale sijui ushauri wenu Waheshimiwa Wabunge, matamshi yale yametamkwa na Mbunge huko mtaani, naona kama Serikali kumjibu kama tunampa hadhi vile, sijui mnavyoshauri wenzangu, lakini nadhani alitakiwa apate Wabunge wasema hovyo tu wamjibu yule. (*Makofii*) (*Makofii*)

Yule ni wa kujibiwa tu wala hana hadhi ya kujibiwa na Serikali, ingekuwa Serikali ya Kenya kuna kiongozi wa Serikali amesema kitu hapo kwa kweli, sijui ushauri tutakaopata toka kwa Serikali, lakini mimi nilikuwa naona hivyo, baada ya kulifikiria, anatakiwa Mbunge tu aseme akipigwa Mtanzania mmoja kesho asubuhi tunakunywa chai Nairobi, majibu tayari Watanzania watakuwa pale tayari na majibu mengine ambayo ninyi mnajua zaidi kuliko mimi. Kwa hiyo, nawaaminia Wabunge wangu kwamba...

Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani unataka kushauri? Tafadhalii karibu.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, hili jambo ni kubwa na ni zito siyo la kupuuza, alichokizungumza Mbunge wa Kenya nilikiona tangu jana usiku na nina marafiki Kenya ambao ni viongozi nikawatumia meseji, nikawauliza wana kauli gani kuhusiana na hizi kauli za *xenophobia* zinazohubiriwa na Mbunge wao. Wengi walikana zile kauli kwamba siyo kauli nzuri, lakini sisi kama Watanzania ambao tumetajwa *specifically* kwenye ile kauli tunahitaji majibu na sidhani kama tuna sababu ya kupuuza, ukasema ni Mbunge amezungumza mtaani.

Mheshimiwa Spika, nashauri Bunge hili litoe kauli ya kukemea na kulaani kauli ile na kauli ya Bunge letu itambue kwamba hatuna ugomvi na Jamhuri ya Kenya na wananchi wa Kenya na Serikali ya Kenya, lakini tuitake Serikali ya Kenya ichukue hatua za makusudi na za dharura, kudhibiti viongozi

wanasiasa kutoa kauli kama hizi ambazo zinaweza zikachafua mahusiano yetu ya Afrika Mashariki na mahusiano ya watu na watu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika nchi za Afrika, Kusini mwa Sahara, hakuna nchi ambayo wananchi wake wametawanyika kwenye nchi za wengine kuliko Kenya.

Mheshimiwa Spika, ukienda Sychelles, ukienda Mauritius, ukienda Middle East kwa maana ya Dubai, ukienda Abu Dhabi ukienda Oman ukija Tanzania, ukienda Zimbabwe, ukienda Uganda, ukienda Rwanda, ukienda South Africa, Wakenya ni nchi ya Afrika ambayo imesambaza *labour force* yake katika maeneo mengi sana katika nchi imbalimbali. Nchi hizi zikiamua ku-*react* dhidi ya wananchi wa Kenya walio kwenye nchi zao itakuwa ni hatari na ni mahusiano mabaya duniani. Ni vema tabia kama hizi zikemewe na zikemewe na Bunge ambalo ni chombo kikubwa sana katika nchi yetu, ni muhimili muhimu ili tabia hizi zikome *once and for all*, naomba kabisa tusizipuuze ile kauli imetutaja Watanzania na tunaweza kujikuta Watanzania kesho wanapoteza maisha kwa sababu tumekaa kimya, tutoe kauli katika jambo hili. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Naendelea kuchukua ushauri. Waheshimiwa napaswa ku-*balance* kidogo, Mheshimiwa Tizeba tafadhalii, nakupa dakika tuongee kifupi kifupi.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli katika mazingira ya kawaida yule Mbunge unaweza ukamdharaun na tukaachana nalo, lakini kwa sababu mambo haya yamekwishatokea hapa Afrika kwa uchochezi mdogo mdogo wa namna hiyo, watu wamepoteza maisha South Africa Watanzania wakiwamo. Kwa hivyo hapa hatuichukulii Jamhuri ya Kenya kwa maana ya Serikali na nchi nzima kwa ujumla, kwamba ndiyo yenye mawazo haya, lakini Serikali ya Kenya inalo jukumu la kukana hiyo kauli yaani kama nchi wanao wajibu wa kusema sisi hatuko naye yule, hayo ni mawazo yake binafsi na hiyo itakuwa inatutosha sana. Ni kwamba Serikali ya Kenya iji-*distance* tu na hayo maneno, basi jambo linakuwa

limekwisha. Kwa maana hiyo nasi tunakuwa na uhakika kwamba Watanzania watakuwa *protected* huko Kenya na Serikali ya Kenya, basi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa tafadhali dakika mbili.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi wiki iliyopita ubalozi wa Marekeni unalitoa tahadhalii ya usalama, ambalo ni jambo zuri, na Balozi wa Marekani aliiwa Wizarani. Sasa mimi ushauri wangu, hapa tunayo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; jambo hili si la kupuuza. Mimi niombe Bunge liiagize Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wawasiliane na wenzao wa Kenya kuona jambo hili linakaa vizuri. Kwa sababu kama tunatajwa Watanzania , na aliyezungumza ni Mbunge, sisi kama Bunge hapa hatuwezi kukaa kimya.

Mheshimiwa Spika, wazo langu ni hilo na ushauri wangu ni huo, kwamba Bunge sasa liiagize Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutafuta ukweli wa jambo hili na watuletee taarifa hapa Bungeni. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante kule mwisho kabisa kule kwenye nguzo kule.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Lusinde hapa.

**SPIKA:** Kule mwisho kabisa.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Lusinde na Mollel.

**SPIKA:** Baadae, baadae, mwisho kule kwenye nguzo kule.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana. Ukifuatilia mazungumzo ya kwanza....(*Kicheko*)

**SPIKA:** Hebu tulia tulia Mheshimiwa Lusinde, aaaaah! yule aliyesimama Lusinde?

**WABUNGE FULANI:** Eeeeeeh.

**SPIKA:** Ninayemtaja ni Millya si Lusinde, ndiye niliyemuona Millya, Lusinde rudi kwako kama unataka kuongea.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, karibu na Kenya watu wetu wanaheemea Kenya, *all most* kila asubuhi. Kauli kama hii, tena inatajwa na Mbunge Mashuhuri Jaguar wa Jimbo la Starehe pale Jijini Nairobi ni kauli ambayo ikivumiliwa inawezekana kesho magari ya watu yanayoenda kufanya biashara Kenya yakaanza kuzuiwa na Watanzania wakazuiwa.

Mheshimiwa Spika, nikuombe kama Kiongozi wetu Mkuu wa Muhimili huu, Serikali yetu iwasiliane na Balozi wa Kenya kuanzia leo ikiwezekana ili kauli hii viongozi wa serikali ya Kenya wakatae kwamba wao hawapo na huo Mbunge kwa sababu hiyo hali ilianza kama mchezo kule Afrika kusini.

Mheshimiwa Spika, lakini unakumbuka Afrika Mashariki ilipovunjika kelele kama hizi zilianzia Kenya mwaka 1977 na akina Charles Njonjo.

Mheshimiwa Spika, nikuombe tuchukue jukumu hili la kuwalinda Watanzania ambao nchi Kenya n maeneo mengi. Kenya ni nchi ya pili kwa *interest* Tanzania, tukiamua sisi Watanzania *ku-react* watapata shida sana. Naomba tulivumilie hili ahsante sana.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Lusinde kwa sababu uliongea mwanzo na umerudi mahali pako nakupa nafasi kwa kifupi sana.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nimefanya kikao na wa Siha waliopo Kenya kuna jambo nitasema...

**SPIKA:** Hapana, hapana, Mheshimiwa Lusinde sasa.  
(*Kicheko*)

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, mimi naomba Bunge lako Tukufu lifikirie upya namna ya kuujadili huu mjadala unaohusu Mbunge mmoja wa Kenya aliyekuwa kalewa mtaani. Yule ni Mbunge mmoja leo tunatumia *time* ya Bunge zima kumjadili kama nchi ilhali majibu yanaweza yakatolewa na Mbunge mmoja?

Mheshimiwa Spika, nina Mkutano Jumatatu nami nitoa amri, Wakenya wanaofanya kazi hapa tutawapiga warudi kwao Kenya, jambo litakuwa limekwisha hilo. Tusitumie kauli ya Bunge zima kujadili vitu vya namna hii, huu ni uoga...

**MBUNGE FULANI:** Lusinde Kaa!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** ... na hili taifa itateketezwa na Wabunge wa namna hii. Tunambembeleza mtu mmoja na yeye anao wafanyabiasha wapo hapa wakitupiga tuwapige shughuli iieshe.

**MBUNGE FULANI:** Lusinde kaa, kaa, kaa

## TAARIFA

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa kwa Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. DKT. MARY A. NAGU:** Mheshimiwa Spika, naomba...

**SPIKA:** Naomba Waheshimiwa wote mkae...

**MBUNGE FULANI:** Taarifa kwa Mheshimiwa Lusinde.

**SPIKA:** Waheshimiwa nawaomba mkae, nawaona wote lakini naomba mkae, naomba mkae kila mtu mahali

pake, naomba mkae kidogo, tulieni kwanza kidogo, naomba mtulie kidogo. Mheshimiwa Mama Nagu nakuona lakini naomba mkae kidogo. Mheshimiwa Selasini nakuona lakini naomba mkae. Waheshimiwa Wabunge naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu aje hapa mbele azungumze nasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu sana tafadhali Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof!*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbewe Kiongozi wa Upinzani, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote na Watanzania wote kwa ujumla, kwanza nawasihi muwe watulivu juu ya jambo hili. Serikali tumelisikia tangu jana na Serikali hatukaa kimya, tumelifanyia kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hatua ambazo tumezipitia kwanza ni kutambua mzungumzaji ana mamlaka gani ndani ya nchi yao. Ni kiongozi wa eneo moja, na nchi ya Kenya wenzetu wameingia kwenye michakato ya uchaguzi, kwa hiyo inawezekana naye pia kwa matakwa, jazba za uchaguzi ilimpelekea huko. Si kauli nzuri, lakini Serikali yetu tunatambua kuwa nchi ya Kenya ni nchi rafiki, ni nchi jirani sana, hata viongozi wetu wakuu wanazungumza lugha moja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nchi hizi na hasa Kenya inapakana na mpaka wa Tanzania mrefu sana, kutoka Mkoani Tanga mpaka Mkoani Mara. Wananchi wa Tanzania na Kenya waniishi kama ndugu hato. Kwa hiyo jambo hili tuliliangalia kwa kina, na tulianza na mawasiliano na Serikali ya Kenya. Tumemwita Balozi wa Kenya nchi Tanzania, tumezungumza naye; lakini tumezungumza na Balozi wa Tanzania nchini Kenya atupe picha ya nini Serikali inapokea kauli ya Mbunge yule kwenye eneo kule nchi Kenya. Tumepata kauli zao wote wawili Balozi wa Kenya nchini Tanzania amekanusha kwamba kauli ile si kauli ya Serikali na wala si msimamo wa Serikali ya Kenya, na wala si msimamo wa wananchi wa Kenya ni jambo lake binafsi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tunatambua jambo binafsi linaweza likaleta madhara nchini; wametusihii Watanzania

tuwe watulivu na tuone kwamba kauli ile ni ya mtu mmoja na wao watachukua hatua mbalimbali kule nchini Kenya.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo sasa hivi tukiwa tunaendelea na Bunge hapa Bunge la Afrika Mashariki lilikuwa linaendelea jiji Arusha. Wabunge wa Wizara za Afrika Mashariki pamoja na Wabunge wenzetu wa Afrika Mashariki yote wapo pale. Mawaziri wamekutana wamejadili kauli hii na wameilaani kwa nguvu zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwamba kauli hii moja ijenga chuki kati ya mtu na mtu, kundi na kundi na vile vile nchi na nchi. Mbili kauli hii inapelekea kuparaganisha nchi zetu za Afrika Mashariki; na Mawaziri wale wamesema hawatatoa nafasi kwa yoyote ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kusababisha kuwa na mahusiano mabaya kati ya nchi na nchi ndani ya jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo Serikali ya Kenya wametuomba tuwe watulivu wanachukua hatua za ndani ya nchi kumpata mtamkaji/msemaji ili aieleze Serikali ya Kenya kauli hiyo kaitoa wapi na alikuwa ana amanisha nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi kama Tanzania na kama Serikali, na ninatambua mchango wenu Waheshimiwa Wabunge katika hili na maoni yenu ya awali; lakini nataka niseme baada ya kuwa tumeyasikia, na kwa kuwa kazi tumelfanya, sisi Watanzania maeneo yote tulipo kama tuna ndugu zetu wa Kenya tuishi nao kama kawaida ndani ya nchi. Hatuna chuki na Wakenya na ninaamini Wakenya hawana chuki na Watanzania ukimwondoa ye ye aliyetamka kwa matakwa yake binafsi kwa sababu Serikali imetuhakikishia kauli hiyo si kauli ya Serikali na si kauli ya Wakenya kwa ujumla wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba mridhie Serikali tuendelee kuzungumza kidiplomasia kwa sababu tunaheshimu mahusiano haya, tunaheshimu mahusiano ya viongozi wetu wakuu lakini pia nchi yetu inafanya biashara na Watanzania wengi wapo kule na huku Wakenya wengi wapo hapo. Watanzania wote mnajua Wakenya nchi kwetu

wapo takriban hoteli zote za Tanzania. Wameingia kwenye sekta ya kilimo, na nchi ya Kenya ndiyo nchi inayoongoza kwa nchi zinazowekeza hapa Tanzania. Kwa hiyo tuna wa Kenya wengi wapo Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Watanzania muwe na amani, hatua zinaendelea ndani ya Serikali ya Kenya, na vile vile hatua za kidiplomasia zinaendelea pia ndani ya nchi yetu. Tunaendelea kuzungumza na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaendelea kufanya kazi hiyo kwa ukaribu zaidi. Pale ambapo kutakuwa na mwafaka au kutokuwa na mwafaka wa namna yoyote ile tutawahabarisha katika hali ya kawaida. Bado Tanzania na Serikali yetu tunatambua Wakenya ni ndugu zetu, marafiki zetu na tunaendelea kushirikiana na Serikali yake, viongozi wetu wanazungumza lugha hiyo. Muhimu zaidi Watanzania, Wakenya, Waganda kutoka Ruanda, Burundi na nchi zote za Jumuiya Afrika Mashariki kila mmoja awe makini na kauli yake ili kuogopa kuvurugha mahusiano ya ndani ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nirudie kuwataka Watanzania kuwa watulivu katika hili na Serikali inaendelea na hatua hizo za kidiplomasia, na sisi tunaamini kwamba hatuna tatizo lolote kati ya nchi hizi zaidi ya kauli ambayo imetoka. Ahsante sana kwa utulivu wenu. (*Makofii*)

**SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kauli thabiti ulioitoa mbele ya Bunge hili kuhusiana na jambo hili na kuwapa moyo Watanzania kwamba Serikali yao ipo macho na inafuatilia. Kwa taarifa zisizo rasmi naambiwa kwamba Serikali Kenya tayari imeshatoa tamko rasmi la kulaani hiki kilichofanywa na Mbunge wake. Kwa hiyo tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaona umetuwekea hali ya hewa imekuwa tulivu kabisa, ahsante sana.

Pia niwaambie Wabunge wangu nanyi kwa wakati wenu siwatumi lakini kwa wakati wenu za kuambiwa uchanganye...mmmh! nanyi msinyamaze sana mnanifanya

Spika wenu nakuwa mnyonge kidogo. Kwa nini Wabunge fulani wawaonee Wabunge wangu bwana! Haiwezekani! Kwa hiyo nanyi huko kwa wakati wenu. Kama *youtube* ni *youtube* huko huko, kama *twiter* huko huko kama *facebook* huko huko. (*Kicheko*)

Katibu bado anamalizia. Mheshimiwa William Ngeleja Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anaomba Waheshimiwa Wabunge ambao mtaondoka kesho kwenda *AFCON* Misri baada ya shughuli hizi mbaki hapa ukumbini ili kupewa a, b, c za mambo ya huko namna tunavyoenda. Wakenya ni ndugu zetu; tutatofautiana siku ya mechii ya Tanzania na Kenya *AFCON* hapo sasa tutakuwa tofauti kidogo. Vinginevyo ni wenzetu na ni ndugu zetu. Na wale wanaozungumza habari ya wachezaji na nini hawaelewi kidogo kule mfumo ulivyo.

Waheshimiwa Wabunge, hivi sasa timu zote zinazoshiri mashindano yale *including* ya kwetu zipo katika hoteli maalum hoteli za kitalii kwa kweli, ambazo gharama zao zote zinalipiwa na *CAF* (*Confederation of African Football*).

Kwa hiyo wachezaji wetu wapo katika hoteli maalum ile hoteli ya kitalii kwa *levelyake tulivyoilangalia* mambo yake yote ni mazuri. *Accommodation* safi, chakula ni safi hakuna mtu ambaye ange-*complain* habari ya chakula; na gharama zake wakati huu wa mashindano hatulipi sisi, wanalipa *CAF*. Kwa hiyo mengine yanasemwa na watu ambao hawajui kile kilichopo kule.

Hata hivyo si wote ambao wanajua kila kitu, hawakujua kwamba nilipokuwa ninakwenda kule sikwenda kama mimi nilikwenda kama mwakili wa nchi, na nilienda kule nikiwa na ujumbe maalum wa Rais Magufuli kwa Rais El-Sisi wa Misri. Mjumbe wa namna hiyo akitoka safari kama hiyo halafu wewe Mkuu wa Mkoa unamletea letea maneno. Ndiyo ile nilikuwa nasema haya mambo mengine Inabidi Mheshimiwa Maiga tumrudishe kwenye kazi yake ya diplomacy ili aweze kuwafundisha vijana diplomasia inasemaje. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge ndugu yetu Katibu wa Bunge anarudi sasa ninaomba utulivu wenu aweze kutusomea matokeo ya kazi yetu. Katibu nakuita sasa usome matoke kama yalivyo, naomba tusikilizane Waheshimiwa Wabunge.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

Mheshimiwa Spika, idadi ya Wabunge waliopo na ambao wamepiga kura ni 380, na Wabunge ambao hawakuwepo Bungeni wakati wa kupiga kura ni Wabunge 12, kwa hiyo Wabunge ambao hawakuamua ni zero. Waliosema hapana ni Wabunge 83, ambayo ni sawa sawa na 21.8% ya Wabunge waliopiga kura, Wabunge walio piga kura za ndiyo ni 297. (*Makof/ Vigelegele*)

**WABUNGE FULANI:** CCM! CCM! CCM! CCM! CCM!  
CCM! CCM! CCM! CCM! CCM! CCM! CCM! CCM!  
*(Makof/.)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana naomba tusikiizane. Naomba tuache kunyooosheana vidole tafadhalii, kila mtu amepiga kura kadiri alivyoona inafaa. Nawaombeni sana asilaumiwe mtu yoyote. Naomba tuwe na utulivu tusifanye hivyo, kila mtu amepiga kura kwa uhuru na kwa hiyo tusimlaumu mtu yoyote.

Naomba utulivu wenu, kwa hiyo ya waliopiga kura ya hapa ni 21.8% ya idadi ya walipiga kura si ya idadi ya Wabunge wote, nafikiri tumeelewa na eeeh, na waliosema ndiyo ni 78.2% ya idadi ya Wabunge waliopoga kura. (*Makof/*)

Kwa hiyo kura hizi za asilimia 78.2 ninatangaza rasmi kabisa kwa kura kwamba rasmi Bunge hili limekubali na kuyapitisha mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadilio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020. (*Makof/ Vigelegele*)

Naomba nichukue nafasi kuwapongeza sana kwanza ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge kwa kazi kubwa sana ambayo mmeifanya kuanzia Aprili mpaka hapa tulipofika leo, hongereni sana. Maana kazi hii ni matokea ya kufanya kazi kwa pamoja kati ya Serikali na Bunge katika mchakato mrefu ambao ni shirikishi kweli kweli, nasema hongeni sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofî*)

Pili, tumpongeze sana Kiongozi wetu Mkuu Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa vile tunafahamu kabisa mwelekeo wa bajeti hii pia *focus* na ilani ya Chama Cha Mapinduzi maana bajeti hii inaenda kuteleza muono huo. Niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri wote, Wizara zote zikiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu; mmekaa hapa mmekuwa nasi tangu tumeanza Aprili mpaka leo kazi kweli kweli, hongereni sana! Sana! Sana!

Pia kipekee kabisa Waziri Mpango na Naibu Waziri Ashatu Kijaji na timu yenu yote hongereni sana na poleni kwa yote. Waheshimiwa Mawaziri ninyi ukiwa Waziri wa Fedha shughuli hasa katika nchi za kwetu ambazo rasilimali ni chache; kwa hiyo kila mtu atakulaumu. Eeeeh ndivyo ilivyo, ni kama sisi Wabunge majimboni kwetu tunalaumiwa na kila mtu maana wananchi wanakuwa na matarajio kwamba shida yao ya maji utaimaliza, maji hayajaja unategemea wakusifie?

Shule yao sijui imefanyaje madarasa hayatoshi wanachoangalia wao ni Mbunge tu, barabara haipitiki kwa nini Mbunge, daraja hili limekatika tangu mwaka jana Mbunge unafanya nini huyu anakaa tu Bungeni. Kwa hiyo lawama ni sehemu ya uongozi nasi hapa Mpango yaani wewe tuvumilie tu huo msalaba utaubebea ukimtafuata Mkirene wa kukusaidia hayupo, Simon Mkirene yupo wapi, utaubebea mwenyewe na Ashatu akusaidie basi. Pole sana kwa yote usichukulie chochote kilicho sema huku *personally, no! don't!*. Ashatu usichukulie *personally*, hii ndio kazi yenye we ndivyo ilivyo, eeeh! tena Bunge letu lina naafuu kuliko lile la wasema hovyo au lile la Afrika Kusini si huwa mnalionia

jamani? Yule Spika sijui akitoka pale inakuwaje akipimwa presha wa South Africa hatari.

Kwa hiyo tunawapongezeni sana Wizara ya Fedha na wengine wote maana bajeti huhusisha kila mtu katika *budget cycle* hadi hapa tulipofika, ni afya ni hongera kwa wote. Hata hivyo bado kuna kazi chache zitaendelea na muda si mrefu tutapaswa kushugulikia *Appropriation Bill* 2019, niatakapomuita katibu hapa. Hii tu tutaipisha mfululuzo katika hatua zake zote bila kuwa na majadala wowote, kama ambavyo kanuni ya 108(1,2,3) zinavyoikeza utaratibu.

*The Appropriation Bill* haipelekwi kwenye Kamati yoyote ya Kudumu wala Kamati ya Bunge Zima; na masharti kuhusu miswada kusomwa kwa mara ya kwanza na kadhalika hayatatumika. Muswada huu huwa hatutangazi kwenye gazeti kabla haujawasilishwa Bungeni. Kuanzia kesho tutaanza kushughulikia *Finance Bill* ambayo na nayo tutaimaliza katika muda si mrefu sana, na baada ya hapa tuna ile miswada mingine ya hati ya dharua nayo tunaishughulikia. Basi kwa hatua hii tuliyofikia naomba nikuite sasa karibu kuhusu shughuli inayofuata.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuidhinisha Jumla ya Shilingi Triliioni Thelathini na Tatu, Bilioni Mia Moja na Tano, Milioni Mia Nne na Tisa, Lakini Nane na Kumi na Tano Elfu na Mia Moja Tisini na Tano kwa Matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa Mwaka Unaoshia Tarehe 30 Juni, 2020; Kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo [*A Bill for an Act to Apply some of Thirty Three Trillion, One Hundred and Five Billion, Four Hundred and Nine Million, Eight Hundred Fifteen Thousand One Hundred Ninety Five Shillings out of the Consolidated*

*Fund to the service of year end on the 30<sup>th</sup> day of June 2020 to appropriate the supply granted for that year to authorizes the allocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purpose]*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2019 yaani (*The Appropriation Bill, 2019*)

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Katibu tena.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuidhinisha Jumla ya Shilingi Trillioni Thelathini na Tatu, Bilioni Mia Moja na Tano, Milioni Mia Nne na Tisa, Lakini Nane na Kumi na Tano Elfu na Mia Moja Tisini na Tano kwa Matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2020. Kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo. [*A Bill for an Act to Apply some of Thirty Three Trillion, One Hundred and Five Billion, Four Hundred and Nine Million, Eight Hundred Fifteen Thousand One Hundred Ninety Five Shillings out of the Consolidated Fund to the service of year end on the 30<sup>th</sup> day of June 2020 to appropriate the supply granted for that year to authorizes the allocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purpose*]

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Naomba nitangaze basi rasmi tena kwamba Muswada huu ambaeo ni Muswada wa Sheria ya kuidhinisha

Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2019 (*The Appropriation Bill, 2019*) umeshapitishwa na Bunge. Tunaitakia Serikali utekelezaji mwema wa Muswada huu; na Sheria hii tunaitakia utekelezaji mwema na hasa mara baada ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kuwa ameshaweka sahihi kadiri atakavyoona inafaa.

Basi Waheshimiwa Wabunge ninawashukuru sana kwa mara nyingine kwa kazi kubwa hii ambayo tumekuwa tukiifanya. Hadi hapa tulipofika kwa kazi zilizopangwa hapa mezani zote zimekamilika. Ninawashukuru sana kwa uwepo wenu, nawashukuru sana wageni wetu mliopo katika *gallery*, mmeweza kuwa nasi mpaka jioni kabisa ya siku ya leo, nafikiri mmejionea na kujifunza jinsi namna gania Bunge linafanya kazi katika kupitisha bajeti; hatua ambao kikatiba ni muhimu sana, kikatiba ni muhimu sana na Bunge limeshatekeleza wajibu wake wa kikatiba na nimishatoa pongezi. (*Makof!*)

Kwa jinsi hiyo Waheshimiwa Wabunge, naomba kwa hatua hii sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho sasa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.28 Jioni Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumatano,  
Tarehe 26 Juni, 2019 Saa Tatoo Asubuhi)*